# Nipashe

Jumatano Aprili 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580100

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Utata waibuka Dar kijana akidaiwa kuuawa na Polisi

UKURASA 4




UKURASA 13

# VITA YA CORONA

**WAWILI** wapona, mbunge ataka JPM apite bila kupingwa, Sadc waja na mambo 11, Zitto aunda timu, yatawala dua ya Karume, daladala 25 mbaroni, DC asambaratisha mkusanyiko...*Endelea ukurasa 2, 3, 5 & 27*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (kulia); Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kulia); Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohammed Aboud Mohammen na Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Karume, wakiomba dua kwenye kaburi la Rais wa kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, wakati wa kumbukizi ya kifo chake, mjini Zanzibar jana. **PICHA: OWM**

## Lissu amshangaa Spika Ndugai kuhusu madai yake

UKURASA 4

## IPTL YAKWAMA KUTHIBITISHA MABILIONI

UKURASA 4

### BAA LA CORONA



MFUMO wenye uwezo wa kutambua mtu mwenye homa kali, ikiwamo ya corona ndani ya muda mfupi, umebuniwa na Kampuni inayoshughulika na masuala ya teknolojia iliyoanzishwa na Watanzania ya 'Emotec'.

Homa kali ni miongoni mwa dalili za mtu aliyeathirika na ugonjwa wa Covid -19, unaosababishwa na virusi vya corona.

* Epuka mikusanyiko ya watu
* Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
* Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
* Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo.




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO **SVEN AISHUKIA TFF KUREJEA LIGI KUU** UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mawaziri Sadc wakubaliana mambo 11 kuhusu corona

**Na Gwamaka Alipipi**

BARAZA la Mawaziri la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), limeridhia usafirishaji wa bidhaa muhimu kupita katika mipaka ya nchi zilizo katika jumuiya hiyo bila kuathiri afya za madereva na watu waliopo mipakani kipindi hiki cha ugonjwa wa virusi vya corona.

Mawaziri hao ni wa mambo ya nje, fedha, viwanda na biashara, utalii, mambo ya ndani pamoja na uchukuzi kutoka nchi 16 wanachama wa jumuiya hiyo.

Mawaziri hao walikutana jana kwa dharura jijini Dar es Salaam, na kuainisha bidhaa hizo kuwa ni chakula, vifaa tiba, dawa, mafuta, makaa ya mawe, pembejeo za kilimo, vifungashio pamoja na bidhaa zote zinazohusika katika utengenezaji, uchakataji na uhifadhi wa chakula.

Vilevile, wameazimia kuzuia usafirishaji usio wa lazima wa abiria kupitia mipakani na vile vile kuratibu sera, kanuni na hatua za haraka za kitaifa za kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa mwongozo na mapendekezo ya mkutano huo.

Alisema mkutano huo uliitishwa kwa dharura kutokana na kasi ya maambukizi na vifo vinavyoendelea kutokea na kwamba umeshaanza kuleta athari hasi, hali iliyowalazimu kukutana kwa dharura ili kujadili na kubuni mikakati ya pamoja itakayowawezesha kukabiliana na janga hilo.

"Tumekubaliana kuwa katika kipindi hiki lazima tuhakikishe zile bidhaa muhimu zinawafikia wananchi, kama mnavyofahamu zipo nchi ambazo hazina bandari ambazo ni Zambia, Malawi, Zimbamwe, Botswana na Lesotho na nchi zenye bandari ni Tanzania, Msumbiji Afrika Kusini, Angola na Namibia," alisema Prof. Kabudi na kuongeza:

"Kwa hiyo ilikuwa ni muhimu kwa nchi hizi zenye bandari kuona ni kwa jinsi gani zitaendelea kuruhusu bidhaa muhimu ziende kwenye nchi hizo ambazo hazina bandari bila kujiweka katika hatari ya kupata maambukizi haya, katika kutekeleza hilo, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo namna ambavyo madereva watapimwa na watakaobainika vipo vituo maalumu," alisema Prof. Kabudi.

Alisema mwongozo huo waliokubaliana utafanyiwa marejeo kulingana na hali itakavyokuwa ikiendelea, na kuongeza kuwa lengo si kufanya biashara bali kuangalia ni kwa jinsi gani wananchi wataendelea kupata huduma na bidhaa muhimu katika kipindi hiki.

Prof. Kabudi alisema idadi ya matukio ya maambukizi ya ugonjwa huo barani Afrika kwa nchi 51 ni 9,198, huku idadi ya vifo vikiwa chini ya 500, idadi ya natukio katika ukanda wa SADC kwa nchi 14 isipokuwa Comoro na Lesotho ni 2,127 na vifo ni 38.

Aidha, Prof Kabudi alisema Machi 9, mwaka huu ulifanyika mkutano wa dharura wa Mawaziri wa Afya wa SADC kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona ambao ulipendekeza kuundwa kwa Kamati maalum kwa ajili ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa itifaki ya afya ya SADC kufuatia mlipuko wa ugonjwa huo.

## Zitto aunda timu kufuatilia corona

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeunda timu ya ufuatiliaji wa ugonjwa wa corona, ili kufuatilia shughuli za Serikali pande zote za Muungano katika kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, ilisema timu hiyo itaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Juma Duni Haji, ambaye pia aliwahi kuwa Waziri wa Afya wa Zanzibar.

Wengine ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Dorothy Semu, ambaye pia ameelezwa aliwahi kufanya kazi katika Wizara ya Afya nchini.

"Kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya COVID-19 na madhara yake makubwa kwa taifa na kutokana na umuhimu wa uratibu wa suala hili, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na Mwenyekiti wa Taifa wa chama, Maalim Seif Sharif Hamad, wameunda timu ya ufuatiliaji wa Corona," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Wengine waliowekwa katika timu hiyo ni Janeth Fusi, Salim Bimani, Pavu Abdallah, Janeth Rithe Mbarala Maharagande, Issa Kheri na Seif Abalhassan.

Akieleza malengo hasa ya timu hiyo, alisema ni kufuatilia kwa karibu shughuli za Serikali katika suala la corona na kutoa ushauri katika chama hicho kuhusu namna bora ya kuhamasisha umma kuhusu kuratibu ugonjwa huo na mikakati ya chama kukabiliana nao.



Wananchi wakiangalia nyumba iliyobomoka kutokana mmomonyoko wa udongo kando ya Mto Ubungo, katika eneo la daraja la treni la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ataka JPM apite bila kupingwa, fedha zitumike kujikinga corona

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Kuteuliwa, Abdallah Bulembo, ameviomba vyama vya upinzani kumuacha Rais John Magufuli kupita bila kupingwa ili fedha zilizopangwa kutumika kwenye Uchaguzi Mkuu 2020 nafasi ya urais zitumike kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Pia, ameliaga Bunge kwa kusema amestaafu na hatagombea nafasi yoyote.

Akichangia juzi bungeni Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2020/21, Bulembo alisema, mkakati wa kukabiliana na ugonjwa huo ni vyama hivyo kumuacha apite ili kusiwe na uchaguzi wa Rais.

"Kwa vyovyote vile nina uhakika upinzani hawana mgombea urais sasa, kwanini tutumie gharama kubwa kufanya uchaguzi wakati mshindi tunaye na aliyoyafanya yanaonekana, kipindi kile kulikuwa na upinzani kwasababu ya Edward Lowassa kwenda upinzani, lakini wakati huu sioni,"alisema.

Aliwaomba kuchukuliwa fedha hizo kupelekwa kupambana na corona na uchaguzi ufanyike kwa wabunge na madiwani.

"Mkipata wabunge wengi na madiwani si mnaongeza pato, pato la ubunge halitokani na rais, kwanini tupoteze fedha kwa kushindana na jiwe, tuokoe fedha kukabiliana na corona,"alisema.

Alieleza kuwa uchaguzi ni gharama kubwa na serikali inaumia na uchaguzi wa rais gharama yake inatisha.

"Tunaweza kuleta hoja tukaungana nao humu ndani tukamuacha tukafanya kwa wabunge na madiwani, mimi najua wapinzani watanichukia, lakini ndio ukweli wenyewe huo maana atashinda kwa asilimia 85 au 90 kwanini tupoteze muda huo," alisema.

Kuhusu kutogombea, Mbunge huyo alisema anastaafu kwa kuwa amekuwa kwenye siasa kwa miaka 30.

"Mimi ni mmoja wapo naaga kwamba sitarudi bungeni sitegemei kugombea chochote ni mstaafu kwasababu nimeshiriki siasa kwa miaka 30 sijawahi kufanya ofisi yoyote ya serikali, mwaka 1995 niligombea ubunge na mtu anaitwa Joseph Lwegasira,"alisema.

Alisema amejifunza bungeni watu wanafanyaje na kipindi cha kung'atuka kimefika huku akisema mtu yeyote atakayejitokeza kumpinga jimboni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, atapiga kambi kwa Majaliwa kuhakikisha anashinda.

"Mheshimiwa Spika (Ndugai), tulikuwa tunashirikiana sana, nimejifunza mengi, umejawa na busara na huruma, uzoefu wako nina amini Kongwa watakupitisha bila kupingwa wasipokupitisha kampeni ni siku 60 nitakaa 30 kwa Majaliwa na 30 Kongwa kuhakikisha unashinda,"alisema.

Alisema akiwa mbunge aendelee kuwa spika kwa kipindi cha miaka mitano kwa kuwa mafanikio yaliyoonekana kwa serikali ya awamu ya tano yamechangiwa na Bunge la 11.

Alisema Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa na Rais Magufuli amefanya kazi yake.

## HABARI KITAIFA

# Tamwa yataka ulinzi wa watoto

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), kimeitahadharisha jamii kuwa makini kuhusu ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto waliopo likizo kwa sababu ya virusi vya corona.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Tamwa, Rose Rueben, kipindi hiki wazazi wanatakiwa kuchukua hatua madhubuti za kulinda watoto wao dhidi ya ukatili na corona.

Alisema endapo wazazi au walezi wakishinda kuwasimamia watoto wao, wanaweza kutengeneza kizazi kingine kilichoathirika na ukatili wa aina mbalimbali.

"Ni muhimu kwa wazazi na walezi kuwalinda watoto na virusi vya corona, lakini wakati huo huo tuangalie madhara yanayoweza kuyapata watoto wa kike na wakiume wanapokuwa nyumbani au mtaani," alisema.

Pia alisema takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), zinaonyesha dunia nzima asilimia 70 ya watoa huduma za jamii na za afya ni wanawake.

"Majukumu haya huwaweka mstari wa mbele katika utoaji wa huduma," alisema na kuhoji, "Je, katika janga hili la Covid 19 (corona), wanawake wanalindwa ipasavyo wasidhurike?"

Rueben aliiomba wadau wa sekta ya afya, elimu na watoto kutoa mafunzo ya namna ya kuwalinda watoto na kuripoti kuhusu ukatili kwa watoto wakati huu.

"Upatikanaji wa taarifa na misaada mingine kwa watoto iongezeke, kuwapo na ubunifu wa mfumo wa kuwapa elimu wawapo nyumbani na wazazi waimarishe ulinzi na kuzuia matembezi yasiyo ya lazima kwa watoto," alisema.

w



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi (kulia), akizungumza na wananchi nje ya majengo ya Ofisi za Jiji la Dodoma jana, walipofika kwa ajili ya kuchukua fomu za kuomba vibanda vya biashara katika eneo la soko jipya la Ndugai na kituo kikuu cha mabasi vyote vikiwa eneo la Nzuguni jijini humo. Mkuu huyo, alisitisha zoezi hilo kutokana na tahadhari ya kuzuia maambukizi ya virusi vya Corona. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC asambaratisha mkusanyiko ofisi ya jiji

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amesambaratisha mkusanyiko wa wananchi waliojitokeza kuchukua fomu za kuomba maneo ya biashara katika ofisi za jiji la Dodoma, kutokana na tishio la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Tukio hilo lilitokea jana wakati Mkuu huyo alipokuta mrundikano huo nje ya ofisi hizo kuchukua fomu za vibanda vya biashara kwenye soko jipya la Ndugai na kituo kikuu kipya cha mabasi eneo la Nzuguni.

Akiwa katika eneo hilo, aliamrisha kusitishwa kwa uchukuaji fomu haraka kutokana na kutokuwapo kwa tahadhari za kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa corona.

"Ndugu zangu wananchi mliojitokeza hapa naomba kuwajulisha kuwa kutokana na mrundikano wa watu mliopo hapa, na mnajua kuwa serikali imezuia mikusanyiko kwa lengo la kujihami na ugonjwa huu unaosumbua dunia nzima, hivyo nasitisha zoezi hilo mpaka utaratibu mzuri utakapowekwa sawa," alisema.

Alisema anafahamu kuwa wananchi wana uhitaji wa maeneo ya biashara, kutokana na hali ya maambukizi ya ugonjwa huo, wataalamu wa afya wanashauri watu wasisogeleane zaidi ya mita mbili.

"Hapa siwezi kuruhusu hali hii kuendelea, najua mnahitaji vibanda vya biashara lakini afya zenu ni muhimu zaidi, nawapa muda wa dakika 10 sitaki kuona watu hapa," alisema.

Alisema kuwa watakaa na uongozi wa jiji ili kuchukua tahadhari za kuzuia maambukizi kwa kuandaa utaratibu wa kila mwananchi anayeingia katika eneo hilo kuchukua tahadhari.

Kadhalika jiji lilitakiwa kuheshimu siku hiyo kutokana kuadhimisha siku ya kumbukumbu ya siku ya kifo cha hayati Abeid Amani Karume ambayo ilitengwa kwa ajili ya kukumbuka mambo mazuri yaliyofanywa na kiongozi huyo aliyekuwa miongoni mwa waasisi wa taifa la Tanzania.

Alisema siku hizo zinatakiwa kuheshimiwa na ndio maana serikali ilitangaza kuwa ziwe siku za mapumziko ili wananchi wajikumbushe historia nzuri ya waasisi hao.

Mkurungenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema uongozi uliandaa utaratibu mzuri wa kujihami na ugonjwa huo kwa kuweka maji ya kunawa mikono kabla ya kuingia katika eneo hilo.

"Lakini kutokana na mwitikio mkubwa wa wananchi, walifika watu wengi na sisi tulikuwa na utaratibu wa watu kuingia ndani, lakini nje ya uzio walikuwapo watu wengi wakisubiri kuingia kulipia fomu," alisema.

Kunambi alisema uongozi wa jiji unaendelea kuandaa utaratibu wa kuomba vifaa vya kupima joto kabla ya mtu kuingia ndani ya eneo la ofisi hizo.

Alisema fomu zinazotolewa na Jiji hilo ni kwa ajili ya kuomba kupangishwa maeneo ya biashara katika eneo hilo la uwekezaji.

Alisema katika eneo la kituo kikuu kipya cha mabasi kuna vizimba 34, ofisi za kukatia tiketi 45, maduka 58, migahawa mikubwa miwili.

Pia kwenye eneo la soko jipya la Ndugai kuna vizimba 379, mabucha 11 ya nyama, samaki na kuku, machijio ya kuku, sehemu moja ya kufungashia, maeneo mawili ya taasisi za kifedha na maduka 175.

# Corona yatawala dua ya kumbukumbu ya Karume

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

VIONGOZI wa dini jana walitumia dua ya maadhimisho ya kumbukumbu ya muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, kumuomba Mungu kuiepusha dunia na janga la ugonjwa wa corona.

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, jana alijumuika na viongozi wa Serikali na wa madhehebu mbalimbali ya dini katika dua hiyo ya kumbukumbu ya miaka 48 tangu muasisi hiyo alipofariki dunia..

Dua hiyo ilifanyika kwenye kaburi la kiongozi huyo lililopo eneo la Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, mjini Unguja, ambapo viongozi wa madhehebu ya dini walipata fursa ya kumuombea dua.

Akifungua dua ya kiislamu, Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, alimtakia malazi mema Sheikh Karume, na kusema kuwa wakati wa uhai wake akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alizingatia umuhimu wa usawa kwa wananchi wake pamoja na kuhakikisha wanaishi katika makazi bora.

Alimuomba Mwenyezi Mungu kuinusuru Zanzibar na dunia kwa ujumla ili kuondokana na maradhi ya corona, yaliosambaa ulimwenguni.

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Zanzibar, Askofu Michael Hafidh, alimtakia msamaha, rehema na amani kiongozi huyo katika mapumziko yake sambamba na kumuomba Mwenyezi Mungu kubainisha njia ya kuondokana na ugonjwa wa corona.

Aidha, Kiongozi wa jamii ya Kihindu Yoges Pirocit, alitumia fursa hiyo kumuombea dua na kumtakia rehma kiongozi huyo.

Dua ya kumbukumbu ya Sheikh Karume, ambayo kwa kawaida hufanyika Aprili 7 ya kila mwaka, ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, wakiwamo Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, viongozi wakuu wa kitaifa wastaafu akiwemo Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume na baadhi ya mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Wengine ni Kiongozi wa Mabalozi wadogo waliopo Zanzibar, George Augostino, mwakilishi wa Familia ya marehemu, Balozi Ali Karume, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Abdulhamid Yahya Mzee, Jaji Mkuu wa Zanzibar Omar Othman Makungu na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdalla Juma Sadalla 'Mabodi'.

Wengine ni Kamanda Brigedia JWTZ Zanzibar, Brigedia Jenerali Fadhil Omar Nondo, Kamshna wa Polisi Zanzibar, Mohamed Hassan, Mwenyekiti Idara Maalum SMZ, Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Hassan Khatibu, pamoja na Wawakilishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na viongozi mbalimbali wa vyombo vya Ulinzi na Usalama vya SMZ na SMT.

Dua ya kumbukumbu ya Marehemu mzee Abeid Amani Karume, mwaka huu imehusisha washiriki wachache, tofauti na ilivyozoeleka ambapo wananchi na waumini hupata fursa ya kushiriki na kusoma hitma.


## TATHMINI YA AWALI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA KIJAMII

### TAARIFA KUHUSU MRADI TARAJIWA WA MCHANGA WENYE MADINI UNAOJULIKANA KAMA TAJIRI, ULIOPO WILAYA YA PANGANI, MKOA WA TANGA

Ili kutimiza matakwa ya sheria ya mazingira Sura ya 191 (Namba 20) ya 2004 pamoja na kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira za mwaka 2005 na mabadiliko yake ya mwaka 2018, taarifa hii inatolewa kuutaarifu umma kwamba kampuni ya MTL Consulting Limited kwa kushirikiana na kampuni ya Environmental Resources Management (ERM), wamepewa kazi ya kufanya tathmini ya awali ya athari za kimazingira na kijamii kwa niaba ya kampuni ya Jacana Resources (Tanzania) Limited kwa ajili ya mradi wa mchanga wenye madini wa Tajiri.

Mradi huu tarajiwa upo wilaya ya Pangani mkoani Tanga takribani kilometa 40 kutoka jiji la Tanga. Eneo la mradi lipo ndani ya leseni mbili za utafiti (PL): PL 7321/2011 iliyopo wilaya ya Pangani. Leseni hii ya utafiti inamilikiwa na kampuni za Jacana Resources ambayo imesajiliwa Tanzania na ni kampuni tanzu ya kampuni ya Strandline Resources Limited, kampuni iliyosajiliwa katika soko la hisa la Australian (Australia Stock Exchange listed mining company (ASX: STA) ambayo imejikita katika utafiti na uendelezaji wa miradi ya madini Tanzania na Australia. Makadirio ya kiasi cha rasilimali za madini yaliyopo katika mradi wa Tajiri ni kiasi cha 239Mt kwa asilimia 3.3 ya jumla ya kiasi cha madini mazito (Total Heavy Minerals (THM) concentration).

Miradi ya uchimbaji wa madini ya aina hii huangukia katika kundi A la miradi kama ilivyoelezwa katika jedwali la kwanza la kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Taarifa hii imetolewa ili kutafuta maoni ya pande zote zinazohusika na zitakazoathirika na uwepo wa Mradi huu. Mtu yeyote mwenye nia, maoni ama dukuduku au ufahamu mahususi kuhusiana na athari za mazingira na kijamii zinazoweza kutokea kutokana na uwepo wa Mradi uliopendekezwa anaweza kuwasiliana au kuwasilisha maoni yake kwa maandishi kwa anuani zifuatazo.

**Jacana Resources (Tanzania) Limited**
P.O Box 105009
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 222 600 430
Email: enquires@Strandline.com.au

**The Director General, National Environmental Management Council (NEMC),**
P.O. Box 63154, Regent Estate,
Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 22 2774889
Email: nemc@nemctz.org

**MTL Consulting Company Limited**
Masaki, Plot No. 689 Sandvick Street
P.O. Box 77894
Dar Es Salaam.
Tel: +255 22 2666879
Email: info@mtlconsulting-tz.com

115687502

# Lissu amshangaa Spika kuhusu madai yake

**Na Enock Charles**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amedai kuwa bado hajalipwa 'gratuity' (bahkshishi) yake ambayo ni asilimia 40 ya mshahara wake, tofauti na kile kinachoelezwa bungeni.

Lissu amesema hayo ikiwa ni siku chache baada ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, kulieleza kuwa Lissu ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Singida Mashariki, hadai chochote na kwamba ameshalipwa madai yake yote.

Vile vile, alidokeza kuwa mwanasiasa huyo anadaiwa Sh. milioni 70 ya mikopo aliyokopa benki.

Akizungumza na Nipashe akiwa nchini Ubeligiji, alihoji: "Niliuliza swali dogo tu, je, nimelipwa kiinua mgongo changu ambacho ni sawa na asilimia 40 ya mishahara yangu?"

"Hayo ya mikopo yangu ya benki yana uhusiano gani na madai yangu ya 'gratuity', hakuna uhusiano hapo," alisema.

Juzi Spika wa bunge, Ndugai, alieleza kuhusu fedha ambazo Bunge limemlipa Lissu ikiwamo posho mbalimbali na mishahara zaidi ya Sh. milioni 500 na kusema kuwa kwa sasa hana madai yoyote anayodai Bunge isipokuwa yeye (Lissu) ndiye anayedaiwa mikopo aliyodai kupitia bunge hilo inayofikia Sh. milioni 70 ambayo bado hajalipa.

"Lissu anapenda sana kuzungumza mambo yake mbele ya jamii, mimi nadhani si busara tena anachokizungumza hakina ukweli ni vyema angepiga hesabu vizuri," alisema Spika Ndugai.

Tangu kuvuliwa ubunge kwa kiongozi huyo wa Chadema, pamekuwa na mvutano kati yake na Bunge kuhusiana na madai mbalimbali ambayo aliyaibua Lissu ikiwamo mishahara, posho na fedha za matibabu wakati mwanasiasa huyo akidai kuwa ni haki yake kulipwa madai hayo Spika wa Bunge, amekuwa akisisitiza kuwa hakuna anachokidai katika bunge hilo.

Lissu alipigwa risasi 32 kati yake tano zilimpata mwilini Septemba 7, 2017, alipelekwa jijini Nairobi kwa ajili ya matibabu na baadaye nchini Ubeligiji ambako amekuwapo hadi sasa.




Dereva bajaji, Justine Chaula (kulia), akisaidiwa na msamaria mwema kunyanyua chombo hicho, ili aweze kubadilisha tairi lililopata hitilafu katika eneo la Posta, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Utata kijana akidaiwa kuuawa na Polisi Dar

**Na Enock Charles**

UTATA umeibuka kutokana na kijana Claud Manda (20), mkazi wa Kinondoni Moscow, kudaiwa kuuawa na Polisi Kinondoni jijini Dar es Salaam jana.

Imedaiwa kuwa aliuawa baada ya kukamatwa kwa mkosa ya uvutaji wa bangi na kushushiwa kipigo.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi katika mkoa wa kipolisi wa Kinondoni, limesema kuwa halina taarifa za mtuhumiwa yeyote kuuawa, ila wanatambua kuna vijana walikamatwa jana kwa matukio mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, babu wa marehemu Lucas Manda, alisema wamesikitishwa na kifo cha mjukuu wake kupigwa hadi kufa, huku wenzake saba wakidaiwa kushikiliwa na polisi.

"Wale vijana walikutwa ndani, wanavyodai ni kwamba walikuwa wanavuta bangi, hawana makundi mabovu ... ni bangi tu wanavuta, na katika kuvuta unajua ni vijana katika vijiwe vyao wale polisi wakaingia mle ndani wakaanza kuwapiga mikong'oto wakaburuzwa mpaka kituo cha polisi," alieleza Mzee Manda. Mama mzazi wa kijana huyo, alilitupia lawama Jeshi la Polisi kutokana na kifo cha mwanawe anayedaiwa kukamatwa eneo la Kinondoni Moscow akiwa na wenzake sita, na kwamba walipaswa kumchukulia hatua za kisheria na siyo kumpiga hadi kufa.

"Kama hawakumuua wao kwanini walichukua jukumu la kuja kumtibu kwani mtuhumiwa anatakiwa kupigwa mpaka afe au kupelekwa kwenye vyombo vya sheria hata kama kaua hata kama kafanya nini," alisema, huku akilia na kuongeza:

"Mwanangu alikuwa mdogo ana miaka 20, hata malengo yake hakutimiza."

Akizungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Edward Bukombe, alithibitisha kuwapo kwa watuhumiwa waliokamatwa na polisi mkoani humo kwa makosa mbalimbali.

Hata hivyo, alidai kutofahamu taarifa za mtuhumiwa yeyote kuuawa na polisi, na kwamba ukweli wa jambo hilo utafahamika baada ya polisi kufanya uchunguzi.

"Kuhusu taarifa za watu kukamatwa ni kweli, lakini kama kuna mtu ameuawa au la itafahamika baada ya uchunguzi kufanyika na taarifa kamili tutaitoa," alisema.

# IPTL yakwama kuthibitisha uhalali wa deni la mabilioni

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

KAMPUNI ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL) imeshindwa kuthibitisha uhalali wa deni lake la Sh. bilioni 102.12 katika Shirika la Umeme (Tanesco), imeelezwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi, kuhusu mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018/19, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema kampuni hiyo ni miongoni mwa 913 zilizoshindwa kuthibitisha madai yake yanayofikia Sh. bilioni 291.17.

CAG alisema amebaini madai hayo yaliyokosa uthibitisho yanatokana na uzalishaji wa nishati ya umeme unaonunuliwa na Tanesco kutoka kwa wazalishaji binafsi.

Alisema aliomba uthibitisho wa madeni kutoka kwa wadai na kwamba kampuni 23 pekee ndiyo zilizothibitisha madeni yake yenye thamani ya Sh. bilioni 647.33 huku kampuni 913 zenye madai ya Sh. bilioni 291.17 hazikuthibitisha madai yake.

"Kati yao, ipo kampuni ya IPTL ambayo ina jumla ya madai ya Sh. bilioni 102.12. Kampuni hii ilishindwa kufanya uthibitisho wa deni lake kutokana na changamoto za kiutendaji zinazoikabili," alisema.

CAG pia alisema amebaini Tanesco ilikuwa na wateja 72,463 ambao hawajafanyiwa upimaji kwa ajili ya kuunganishwa huduma na wateja 155,127 ambao walishalipia gharama lakini hawajaunganishiwa umeme.

Alisema ucheleweshaji huo umelipotezea shirika mapato yaliyokadiriwa kufikia Sh. bilioni 60.7 kupitia malipo ya kuunganishwa na kiasi cha Sh. bilioni 8.33 kupitia matumizi ya umeme.

Pia, alisema Tanesco ilipoteza wastani wa Sh. bilioni 67 kwa mwaka kutokana na upotevu wa nishati ya umeme.

**"Kati yao, ipo kampuni ya IPTL ambayo ina jumla ya madai ya Sh. bilioni 102.12. Kampuni hii ilishindwa kufanya uthibitisho wa deni lake kutokana na changamoto za kiutendaji zinazoikabili," alisema.**

## HABARI KITAIFA

# Jenerali Mabeyo akagua mpaka Tanzania, Msumbiji

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Venance Mabeyo, amefanya ziara maalumu ya kukagua usalama katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji kufuatia matukio ya vitendo vya uhalifu yaliyotokea nchini humo hivi karibuni.

Ziara hiyo inafuatia siku chache baada ya Jeshi la Polisi nchini kupeleka vikosi vyake maalumu kwa ajili ya kulinda usalama katika eneo hilo na mengine yaliyopakana na Tanzania.

Juzi IGP Simon Sirro pia alifika eneo hilo na kufafanyia ukaguzi akiwa na viongozi wengine wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Jenerali Mabeyo amefanya ziara hiyo jana na kuzungumza na waandishi wa habari mkoani hapa kueleza hali halisi ya lengo la ziara hiyo katika maeneo hayo.

Alisema wamekwenda mkoani Mtwara kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama katika mpaka kati ya Tanzania na Msumbiji, pia kujiridhisha na hali hiyo ya usalama kwa vile tayari wameshachukua hatua za kuimarisha usalama wa eneo hilo.

Jenerali Mabeyo alisema matukio ya uhalifu yanayotokea nchini Msumbiji yamewashtua na kuona haja ya kuimarisha ulinzi kwenye mipaka yake na Msumbiji.

Jenerali Mabeyo alisema jeshi hilo linasikitishwa na vitendo hivyo vya uhalifu vinavyotokea nchini Msumbiji na kwamba Jeshi la Tanzania limeshajipanga kudhibiti matukio hayo.

Alisema wakuu wa vyombo vya ulinzi wanao wajibu wa kufika kwenye mipaka hiyo kuona hali ya ulinzi inavyoendelea na nguvu ya kulinda mipaka hiyo.

"Tumesikitishwa sana na matukio yale yaliyotokea kwa majirani wetu wa Msumbiji hivyo sisi hatupendi kwetu yatokee matukio kama hayo, ndio maana tumekuja kuangalia na kujiridhisha hali ya usalama, sisi tumejipanga kukabiliana na vitendo hivyo vya uhalifu," alisema Jenerali Mabeyo.

Vile vile, Jenerali Mabeyo alisema kutoka na wananchi wa Tanzania na Msumbiji wamekuwa ni watu wanaoingiliana na wengine hata kuwa wameoana na wengine wanandugu zao huko Msumbiji hivyo mwingiliano huo usije ukasababisha uhasama na kuhatarisha usalama.

Alisema jambo bora ni kuhakikisha kunapokuwa hali ya kuhatarisha usalama ni bora wananchi wakatoa taarifa mapema kwa vyombo husika ili kwa pamoja kunusuru hali ya hatari ya kuhatarisha usalama wa nchi.

Jenerali Mabeyo alisema wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo pembezoni washirikiane na serikali kutoa taarifa dhidi ya wahusika wanaofanya matukio hayo ya kihalifu kwa kuwa jeshi lipo kwa ajili ya kuimarisha usalama na kuwasaka wahusika hao wanaohatarisha hali ya usalama.



Kamanda wa Polisi mkoa wa Morogoro, Walboard Mtafungwa, akipata maelezo kutoka kwa dereva wa daladala, Juma Hamis, kuhusu namna anavyowakinga abiria wake, dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona, alipofanya ukaguzi kwenye mabasi hayo, jana. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Daladala 35 zakamatwa kukaidi agizo vifaa vya kunawia

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro limeyakamata magari zaidi ya 35 kwa kutokuwa la vifaa vya kujikinga na maambukizi ya corona.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi wa mkoa, Wilibroad Mtafungwa, alisema operesheni hiyo ilifanyika jana baada ya baadhi ya madereva na makondakta wa magari hayo kukaidi agizo la kujikinga na virusi vya corona.

"Tumeyakamata magari zaidi ya 35 kwa kosa la kukaidi agizo la serikali la kuweka maeneo yote ya stendi vifaa vya kunawia mikono ili abiria wanaotumia vyombo hivyo wajikinge na maambukizi ya corona," alisema.

Kamanda Mtafungwa alisema daladala zilizokamatwa baadhi yake hufanya ruti kutoka mjini kwenda maeneo ya Kihonda, Azimio, Mkundi, Manyuki na Yesipa katika Manispaa hiyo na kwamba wahusika watachukulia hatua kali za kisheria.

Alisema uchunguzi uliofanywa na polisi umebaini kuwa stendi nzima ina ndoo mbili pekee za kunawia mikono jambo ambalo ni hatari na kusema jeshi hilo litaendelea kuwachukulia hatua wataokaidi agizi hilo.

Vile vile, aliwataka madereva na makondakta wa daladala hizo kuwa na dawa za kunyunyuzia kwenye magari yao kabla ya kuaza ruti zake na baada ya kazi.

Aliwataka abiria wote wanaotumia daladala hizo kujali afya zao dhidi ya ugonjwa wa corona kwa kuwa bila wao kuwa mstari wa mbele kukabiliana na ugonjwa huo juhudi zinazofanywa na serikali hazitakuwa na tija kwao.

Andrea Msofe, Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa daladala alisema, wanaunga mkono operesheni hiyo na kwamba changamoto iliyojitokeza inatokana na wao kutokuwa na elimu ya kutosha.

Msofe alisema baadhi ya abiria wanakuwa wagumu wanapotakiwa kunawa mikono na kutaka elimu zaidi ili kufanikisha.

Abiria kwa upande wao wamelipongeza jeshi hilo kwa kitendo hicho na kulitaka kuongeza msako kwa kuwa baadhi ya madereva huzidisha abiria nyakati za usiku wakiamini kuwa askari wa usalama barabarani wameshatoka vituoni.

# Viongozi kujaza fomu za maadili kidijitali

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imeanza rasmi ujazaji fomu za matamko ya rasilimali, madeni na mali za viongozi wa umma kwa njia ya mtandao 'Online Declsration System (ODS)' ili kupunguza upotevu wa fomu na muda.

Utaratibu huo umepangwa kuanza kutumika katika dirisha la Oktoba mwaka huu hadi Desemba 31, 2020.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyeki wa Sekretarieti ya Maadili, Jaji Harold Nsekela, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utaratibu huo wa ujazaji fomu za mali na madeni ya viongozi wa umma.

"Zoezi la mwishio wa mwaka litaanza Oktoba mwaka huu na litafungwa Desemba 31, kuna miezi mitatu ya kujaza fomu hizo bila kuchelewa na hii ni lazima siyo ombi," alisema.

Jaji mstaafu Nsekela, alisema mfumo huo utawasaidia viongozi wanaotakiwa kujaza mali zao wasikwame wala kutoa visingizio vya kuchelewa.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kwenda na wakati kama zilivyo taasisi nyingine ambazo zinakwenda kidijitali nao wameanza kutumia mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasailiano (Tehama).

"Naomba viongozi muanze sasa kujaza fomu msisubiri tarehe za mwisho ndio mnaanza kuhangaika," alishauri Jaji Nsekela.

Alisema hakuna sababu ya wao kuanza kuwafuatilia, kinachotakiwa ni kila mmoja kutii sheria ya kujaza mali hizo kwa sababu ni wajibu wao kisheria.

Alisema kuja fomu hizo ni takwa la sheria namba 13, ya mwaka 1995 ambayo inasema kiongozi atakayejaza fomu atakuwa ametengenezewa akaunti na sekretarieti ya maadili.

Naye John Kaole, Katibu Msimamizi wa Maadili, alisema ni vyema watu wakatumia mfumo huo kwa sababu unarahisisha namna ya ujazaji na kupunguza gharama kusafiri umbali mrefu.

Kaole, alisema viongozi husika baada ya kuona taarifa hiyo, wanapaswa kuanza kujaza fomu hizo mapema kabla ya muda.

"Tunawaomba viongozi kuanza zoezi mapema ili kupunguza msongamano," alisema Kaole.

Kwa upande wa Mkuu wa kitengo cha Tehama, Stanslaus Mwita, alisema mfumo wa kidijitali ni mzuri, ndio maana wameamua kuanza kuutumia ili kuwarahisishia viongozi ambao wanalalamika kutokana na umbali wa kuja kujaza fomu.

Alisema baada ya kuona hilo waliona wafanye hivyo ili nao wapate urahisi wa kujaza fomu hizo kwa haraka kabla ya tarehe ya mwisho ya ujazaji fomu hizo.


**ABBOTT FUND TANZANIA LIMITED**

**(Company No. 58641)**

**(Certificate of Compliance No. 1828)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT**

**(AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations require that all non-governmental organisations in Tanzania publish bi annually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE,** we wish to make the following public disclosure of the funds received in 2019 and their expenditure, which publication covers the reporting period from 1st January, 2020 to 30th June, 2020:

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Emergency Medicine; Central Pathology Laboratories; Leadership Capacity-Building | 721,000 |
| **Regional Laboratories and Laboratories IT Projects; Mentorship** | 492,000 |
| **Building Livelihoods:** Includes National Children's Centre Infrastructure Project (Dodoma) | 1,400,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff | 1,743,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2019** | **4,356,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA LIMITED**

115691302

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Ripoti ya CAG iwaadabishe wafujaji wa fedha za umma*

**JUZI** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), aliwasilisha bungeni ripoti ya mwaka 2018/19, iliyoonyesha bado kuna tatizo la utunzaji na ukusanyaji, pamoja na kutozingatiwa kwa sheria na taratibu za fedha za umma.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alisema kamati yake kwa kushirikiana na kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) itakutana na CAG na kuchambua majina ya vigogo ambao wameonekana kuendelea kufuja fedha za umma.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa watawasilisha majina hayo kwa Rais John Magufuli kwa ajili ya hatua zaidi.

Moja ya madudu yaliyoainishwa na CAG ni Jeshi la Polisi kulipa kiasi cha Sh. milioni 196 .13 kwa watumishi 11 ambao walishafariki dunia, kufukuzwa kazi au kustaafu, jambo ambalo ni kinyume cha matakwa ya Kanuni ya 113 (3) ya Kanuni za fedha za Umma ya mwaka 2001.

Aidha, CAG alibaini taasisi tano za Serikali Kuu kufanya manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 5.46 pasipokuwa na mikataba.

Pia, alibaini upungufu katika mkataba wa ukusanyaji mapato kwenye uwanja wa Taifa na Uhuru jijini Dar es Salaam kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Selcom Paytech PLC, akisema wizara haina mtaalamu wa Tehama anayesimamia stakabadhi zinazouzwa kupitia mfumo wa kielektroniki.

Mengine ni matumizi ya Sh. bilioni 5.06 yaliyofanyika bila kuwapo kwa nyaraka toshelezi kulikokwamisha mawanda ya ukaguzi katika taasisi 39.

Madudu hayo yalikwenda mbali zaidi hadi kwenye Balozi za Tanzania nchini Brazil, Algeria na Sweden ambazo zilitumia Sh. bilioni 1.02 kukodi nyumba za makazi, kiasi ambacho kingeepukika kwa kukarabati nyumba za makazi zilizochakaa.

Kazi kubwa ya CAG ni kuwa jicho la Serikali, kwa maana ya kukagua kila mahali ambako fedha ya umma inatumika au kukusanywa, na inapotoka ripoti kama hii inaonyesha uhalisia wa mambo kwenye maeneo hayo ambayo mengine husababishwa na kushindwa kutunza nyaraka muhimu kwa ajili ya ukaguzi.

Mara nyingi hoja nyingi za ukaguzi hujikita kwenye matumizi ya serikali, manunuzi, sheria na taratibu hasa katika ushindani wa zabuni kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali.

Licha ya kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kupambana na matumizi mabaya ya fedha za umma, bado inaonekana hakuna woga katika kwenda kinyume na utaratibu wa kutumia fedha hizo.

Jicho la CAG limedhihirisha kuwa bado kuna tatizo na viongozi wa umma wanapaswa kubadilika kwa kuhakikisha hoja hizo za kuonyesha fedha ya umma imetumiwa vibaya zinakwisha, kiasi cha kufikia mahali hakuna taasisi au Serikali Kuu zinakuwa na hoja zenye utata.

Kuendelea kuwapo kwa hoja hizo ambazo wakati mwingine zingeweza kumalizwa, maana yake bado yanahitajika mabadiliko katika utendaji kazi wa umma kwa mujibu wa sheria.

Ni lazima watumishi husika wajifunze na kuwa na nidhamu ya kusimamia fedha za umma, kuliko kuacha hali iendelee kuwa kama ilivyo, kwa kuwa misingi isipofuatwa, fedha za walipakodi zitaendelea kuteketea kwa kwenda kwenye mikono isiyo salama.

Mathalani, kwenye suala la zabuni ya huduma fulani ni lazima sheria ifuatwe, kuwe na ushindani thabiti katika suala hilo kwa kuwa bila kufanya hivyo, inaweza kugeuka ndiyo mahali pa kupewa na baadaye huduma dhaifu kutolewa kwa wananchi.

Tunashauri kwamba ripoti ya CAG iwe jicho la serikali kuona pale inapotakiwa kuanzia katika kuwaadabisha wale wote wanaojihusisha na wizi, ubadhirifu na uvujaji wa fedha za umma

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wapigakura waandaliwe kuwapima wagombea 2020

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya matukio makubwa na muhimu kwa taifa hili, ambayo yanatarajia kuwapo mwishoni mwa mwaka huu wa ni uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani.

Kabla ya uchaguzi huo, kuna hatua muhimu zinazoendelea kufanyika kwa ajili ya kuufanikisha, ikiwamo uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ambao unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Hadi sasa zaidi ya wapigakura milioni 30 wamehakiki taarifa zao kwenye awamu ya kwanza ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura uliokamilika hivi karibuni.

Idadi hiyo inatajwa na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, kwenye mkutano wake na viongozi wa vyama vya siasa, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Baada ya uboreshaji huo pamoja na mambo mengine kukamilika, zitafuata kampeni za uchaguzi zitakazofanywa na wanasiasa watakaokuwa wameteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Hapa ndipo ninapotaka kujikita zaidi kutokana na ukweli kwamba kuna changamoto katika uchaguzi zinazotokana na tatizo la ukosefu wa elimu na kusababisha wapigakura kushindwa kuchagua viongozi sahihi.

Linapokuja suala la kampeni, ni kwamba wagombea wanajinadi kwa wapigakura, wakielezea kile ambacho wamepanga kukifanya mara watakapopewa ridhaa na wananchi.

Kitendo cha kujinadi au kupiga kampeni ni sawa na kuonyesha mwelekeo na dira ama mbinu watakazotumia kutekeleza kile ambacho wameahidi kwenye kampeni za uchaguzi kupitia sera na ilani za vyama vyao.

Wakati vyama vikiwa bado havijateua wawakilishi kwa ajili ya uchaguzi huo, ni vyema Watanzania kupewa elimu itakayowawezesha kuwapima wanasiasa watakaoteuliwa na vyama vyao kuwania uongozi.

Lengo la kufanya hivyo ni kwa ajili ya kupata viongozi bora na siyo bora viongozi, hivyo umakini unahitajika katika jambo hili la mnada wa kuwapima wale watakaojitokeza kuwania uongozi.

Hili linaweza kufanikiwa iwapo Watanzania wataelimishwa kuhusu kampeni za uchaguzi ili mwisho wa siku wafanye uamuzi sahihi mara baada ya kampeni hizo zitakazofuatiwa na uchaguzi mkuu.

Elimu inatakiwa kutokana na ukweli kwamba wanasiasa ni wajanja, wana mbinu nyingi ambazo wanaweza kuzitumia wakashinda na kumbe hawana uwezo wa kuongoza, hivyo suala la elimu kwa wapigakura ni muhimu.

Kimsingi siasa ni kila kitu kwa maisha ya kila siku, kwa hiyo wananchi wasipoelimishwa wanaweza kuchagua viongozi wasiofaa, matokeo yake watajikuta wanakosa maendeleo kwa sababu ya uvivu wa kuchagua.

Wananchi wanatakiwa kutambua kuwa msingi wa utawala ni wao wenyewe, na hili watalitambua kwa kupewa elimu, hivyo ni muhimu wanasiasa kuwasaidia wananchi waelimike na wachukue nafasi yao.

Nafasi yao ni kushiriki katika siasa wakiwa na uelewa wa kutosha utakaowawezesha kuwania nafasi za uongozi na hata kuchagua viongozi sahihi watakaoshirikiana nao kuleta maendeleo.

Hilo likifanyika linaweza kupunguza mtindo wa baadhi ya wanasiasa ambao wamekuwa wakidaiwa kuwahadaa wapigakura ili wachaguliwe, lakini baada ya kuchaguliwa tu wanatowatosa wale waliowachagua.

Imekuwa ni kawaida kuona wanachama na wafuasi wa vyama wakimshangilia mgombea fulani kwenye kampeni, kisha kumpa kura halafu baada ya miezi kadhaa wanaanza kumlalamikia.

Kwamba fulani alituahidi hiki na kile lakini hajafanya hata kimoja, mara hataki kupokea simu, ofisini haonekani, amebadili 'laini' ya simu, tangu achaguliwe hajaonekana jimboni au katika kata.

Malalamiko ya aina hiyo huwa yanajitokeza kwenye maeneo ya majimbo na kata nchini, ndiyo maana nikasema suala la wananchi kupata elimu ni la muhimu kwani litawawezesha kuchagua viongozi sahihi.

Elimu inamsaidia mpigakura kutafakari kwanza kabla kufanya maamuzi badala ya kusukumwa na mihemko na ushabiki wa kisiasa, ambao mwisho wake mara nyingi huwa siyo mzuri.

Ni muhimu kuwapo kwa siasa zilizopevuka na hizo zitatokana na wananchi kupata elimu itakayowaweza kutambua haki yao ya kupiga kura na kupata viongozi sahihi watakaoshirikiana nao kujiletea maendeleo.

Wananchi wakielimika hawatapiga kura kwa mazoea na badala yake watachagua viongozi, ambao wao wenyewe (wananchi) wanaamini kwamba wana mchango kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Yawezekana wananchi wakalalamikiwa kuwa wana mchango mkubwa katika kupata viongozi wabovu, lakini je, wameelimishwa vya kutosha kuhusu wanavyotakiwa kushiriki kwenye uchaguzi?

# Tunahitaji kumtangaza Karume zaidi

**MHARIRI**

*PONGEZI kwa Watanzania kwa kumuenzi Karume na jana ndiyo yalikuwa maadhimisho ya Karume Day.*

*Nishauri kuwa tunahitaji kuwa na miradi mikubwa inayotumia jina lake ili kuongeza heshima yake na kuzidi kumkumbuka.*

*Ninasema haya nikiangalia kazi zinazofanyika kwa mfano daraja la Ubungo, kuna kazi nyingine kama ujenzi wa barabara nyingi zaidi na vituo vya mabasi ya mwendokasi na ujenzi wa miumbombinu mbalimbali unaoendelea mkoani Dodoma ambayo sasa ni makao makuu ya nchi.*

*Ni vyema tukayapa jina la Karume na kuongeza utambulisho wa miundombinu na majengo hayo kwa kuyaita Abeid Amani Karume ili tuzidi kulitangaza zaidi jina lake.*

*Pamoja na Karume mwezi huu pia Waziri Mkuu kipenzi cha Watanzania Edward Moringe Sokoine alipoteza maisha kwenye ajali iliyotokea mkoani Morogoro.*

*Tunaendelea kuwakumbuka na kuwaenzi viongozi hawa kwa kufanyakazi kubwa ya kulitumikia taifa.*

***Ni Sudi Mkwama***
***Pugu Kajiungeni***
***Mwisho***



## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

## ABEID AMANI KARUME 1905-1972

# Zanzibar ianzishe miradi mipya kumuenzi Karume

**Na Gaudensia Mngumi**



APRILI 7, ni siku ya kukumbuka maisha na kifo cha muasisi wa taifa la Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume, ambaye licha ya kuondoka duniani ameacha mafanikio kisiasa, kiuchumi na kijamii nje na ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Kisiwani Zanzibar kuna tumaini jipya licha ya mwaka Aprili 1972 kuwa mwisho wa maisha yake, kadhalika eneo la Kisiwandui alipouawa kwa kupigwa risasi Karume, haliwezi kubaki kuwa eneo la huzuni tena, kwani Wazanzibari wanaendelea kufurahia mafanikio na ushindi wa kisiasa uliopatikana baada ya Karume kuongoza mapinduzi ya mwaka 1964 yaliyomng'oa mkoloni .

Ni dhahiri marejeo na tafakari za maisha ya Karume yanafanyika kila wakati akiwa ndiye aliyebuni na kutekeleza mikakati ya kuijenga Zanzibar na kuipa taswira inayoonekana leo. Ndiyo maana wakazi wa Zanzibar, Pemba na Tanzania Bara wanaendelea kukiri kuwa ni Karume ndiye aliyeiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia, kwani ni miongoni mwa viongozi wa jamhuri hii waliofanikisha Tanzania kujulikana kote duniani.

Wanalosema ni kweli kwani ndiye aliyeanzisha mikakati ya kujenga uchumi na kuboresha maisha ya Wazanzibari pamoja na kubuni na kuuweka mwelekeo wa Zanzibar inayoonekana leo.

Tafakari iliyoko mbele yao zama hizi pengine ni kuona kuwa ni wakati wa kuundwa mkakati wa kitaifa wa kupata mfuko maalumu wa kukamilisha na kuijenga miradi iliyoanzishwa na muasisi huyu ili kuhakikisha kuwa lengo alilolikweka linatimia kwa manufaa ya wananchi wake.

Kuzifanikisha kazi za Karume ni muhimu ili hata miaka 500 ijayo vizazi vyake vione na kufahamu kazi za muasisi wa taifa hilo. Mambo hayo yatahusisha kuanzia ujenzi wa makazi bora ya wazee, utoaji elimu bora, huduma za afya, kilimo na maisha ya utoshelevu kwa Wazanzibari wote.

Lakini pia, pamoja na kuenzi aliyoyaanzisha, suala la ukosefu wa ajira kwa vijana wa Zanzibar linapaswa kupewa mtizamo mpya.

Nafasi yao katika kuondoa umaskini ambayo Karume angeifikiria pengine ni kuona kuwa ni wakati wa kuhimiza uwekezaji kwenye uvuvi wa bahari kuu ili kuinua na kuuimarisha uchumi wa Zanzibar ambao pamoja na kuing'arishwa na utalii haujapata fursa za kutosha za kutumia rasilimali za maji ya bahari kuu na kuondooa umaskini na tatizo ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana.

Naamini vijana wa Zanzibar wangependekeza kuhamasisha ununuzi wa meli za kisasa za kuvua bahari kuu na kufanyika uwekezaji vijijini wa kusindika na kuuza samaki ili wapate ajira na kubadilisha maisha yao.

Lakini si hayo tu huenda wananchi na vijana pia wangependa kujengwa taasisi za kielimu kama Chuo Kikuu cha Utafiti wa Samaki na Mwani kwa ajili ya kumuenzi mwasisi aliyehifadhi maliasili hizo hadi Watanzania watakapokuwa na uwezo wa kuzivuna.

Wazanzibari wangependa pia kuanzishwe kiwanda cha kuchakata na kuuza bidhaa mbalimbali zinazotokana na mazao ya bahari na kuifanya kuwa kituo kikubwa cha biashara ya samaki Afrika Mashariki.

Kwa hiyo ni wakati wa kufikiria kuwa na kituo kinachoitwa kwa jina la Karume ili kuendeleza na kuuenzi mchango wake wa kuikomboa Zanzibar pamoja na Tanzania na Afrika pia.

Karume alikuwa ni kimbilio la kusaidia wenye shida yakiwamo mahitaji muhimu, kama fedha , ushauri na faraja kwa wajane, maskini na wazee hivyo ni lazima kuanzisha Mfuko wa Karume ili kuendeleza kazi za Karume ili liwe kimbilio kwa wananchi wa kipato kidogo na wanaohitaji mkono wa kuwalinda.

Mfuko huo wa Karume ufanye kazi pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya JAmii (Tasaf), na kuongeza chanzo kingine cha kupunguza umaskini miongoni mwa kaya maskini hasa kwa kaya zenye maisha duni.

Ni vyema pia kuutumia mfuko huo kuwasaidia kujenga makazi na kuanzisha miradi ya kiuchumi wanavijiji wa Pemba na wengine wanaokosa ardhi kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha mawimbi ya bahari kumeza baadhi ya maeneo ya vijiji kutokana na mawimbi makubwa yanayotishia uhai wa mazao na watu.

Tatizo la mafuriko na kina cha bahari kujaa limekuwa tatizo na changamoto kubwa na kusababisha watu kuhangaika kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Ni dhahiri kuwa kuna mengi ya kufanya ili kumuenzi Karume, lakini ni vyema taifa lisisahau kuboresha na kuimarisha Makumbusho ya Karume ili yawe kitovu cha kupata taarifa za kiuchumi, kitamaduni na elimu ya siasa na kuhamasisha uzalendo miongoni mwa vijana.

Pia yawe ni kitivo na kitovu cha kujipatia kumbukumbu na mafanikio ya kazi za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni na yale yote yanayostahili kuenziwa na kudumishwa na Watanzania na Wazanzibari.

Aidha, ni wakati kuudumisha Muungano kwa kumuenzi Karume zaidi kwa kukubali kuwa kiongozi huyo alitanguliza utaifa na uzalendo.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Mbunge Mtaturu awataka wapinzani kuiamini NEC

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu, amewataka wabunge wa upinzani kuiamini Tume ya Uchaguzi (NEC) kwa kuwa ndio iliyowafanya kuwapo na bungeni zaidi ya 100.

Akichangia mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2020/21 ambayo ilipitishwa na Bunge juzi, Mtaturu alisema Tume iliyopo ni huru hakuna haja ya wao kutoamini.

"Hakuna malaika ambaye atakuja kusimamia uchaguzi, ndio maana sheria na taratibu mmeelezwa kule ndani ya chumba cha uchaguzi kutakuwa na wakala, kutakuwa na wasimamizi wasaidizi, kutakuwa na vyombo vya ulinzi na usalama, ninaamini vitakwenda kutenda haki kwa sababu haki siku zote haipotei,"alisema.

Aliwaomba kuwa na utulivu na kutunza amani iliyopo.

Wakati huo huo, mbunge huyo alisema wabunge wa CCM wamekuwa wakitembea kifua mbele katika majimbo yao kutokana na Rais John Magufuli, kugusa maisha ya Watanzania katika sekta za maji, umeme na miundombinu.

"Ukienda kila mbunge mmoja mmoja ukimuuliza namna ambavyo serikali imegusa maisha ya wananchi katika jimbo lake atakueleza mambo sio chini ya matatu, nichukue nafasi hii ya kwanza kumpongeza Rais kwa namna alivyokuwa kinara kwenye mabadiliko katika nchi yetu," alisema.

Mtaturu alitoa mfano katika jimbo lake la Singida Mashariki kulikuwa na tatizo la maji na waliomba visima 15 na mpaka sasa wameishapata visima 11.

"Nichukue fursa hii kuwahakikishia wananchi wa Singida Mashariki, serikali yao na mimi mwakilishi wao nipo kwa ajili ya kuona maslahi yao yanapatikana hasa tatizo la maji ambalo kwa kweli limekuwa ni tatizo kubwa," alisema.




Moses Hella, Mkurugenzi wa kampuni ya Emotec Limited, akielezea mfumo mpya wa kamera unaoweza kumtambua mtu mwenye homa kali kwa muda mfupi, jana jijini Dar es Salaam. Mfumo huo umelenga uisaidia serikali kwenye janga la Covid19. **MPIGA PICHA WETU**

# Mmiliki mtandao Tv ahukumiwa

**Na Mwandishi Wetu**

MMILIKI wa Mtandao wa Tv, Yusuf Feruzi, amehumumiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitatu, baada ya kukutwa na hatia ya kosa la kujiunganishia Chanel 24 king'amuzi Cha DSTV bila kibali cha Kampuni ya Multi Choice Africa Ltd.

Kadhalika, mshtakiwa huyo alijiunganishia chanel hizo zikiwamo zinazorusha matangazo ya ligi ya Uingereza (EPL) bila kibali cha Kampuni ya Multi Choice Africa Ltd.

Hukumu hiyo ilisomwa na Hakimu Mkazi, Boniface Lema, aliyesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mwanza.

Alisema bila kuacha shaka upande wa Jamhuri umethibitisha kosa kwanza la kukiuka haki miliki katika ya makosa mawili yaliyokuwa yanamkabili.

"Bila kuacha shaka mahakama hii imekutia hatiani kwa kosa la kwanza, inakutia hatiani, utalipa faini ya Sh. 500,000 ukishindwa utakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitatu," alisema Hakimu Lema.

Hata hivyo, mahakama hiyo imemwachia huru kwa kosa la pili la kuvunja haki miliki kinyume cha sheria baada ya ushahidi wa mashahidi saba wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha kosa hilo.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Sabina Choghorhwe, akisaidiana na Lilian Meli, ulidai kuwa Novemba 19, 2016 eneo la Ghana Karume ,Wilaya ya Ilemela jijini Mwanza, mshtakiwa huyo ambaye pia ni mfanyabiashara kwa njia ya udanganyifu ya kuonyesha mechi za Ligi ya Uingereza, alitumia jumla ya channel 24 kupitia Ghana Tv Network bila kibali cha Multi Choice Tanzania Ltd, wamiliki wa haki miliki hiyo kwa hapa nchini kwa niaba ya Multchoice Africa Ltd.

# Mfumo kutambua mwenye homa kali kwa muda mfupi

**Na Maulid Mbaga**

MFUMO wenye uwezo wa kutambua mtu mwenye homa kali, ikiwamo ya corona ndani ya muda mfupi, umebuniwa.

Homa kali ni miongoni mwa dalili za mtu aliyeathirika na ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Mfumo huo umebuniwa na kampuni inayoshughulika na masuala ya teknolojia iliyoanzishwa na Watanzania ya 'Emotec'.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa teknolojia hiyo, jana jijini Dar es Salaam, Moses Hella, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, alisema mfumo huo unafanya kazi pindi unapowekwa katika kamera.

Hella alisema kamera yenye mfumo huo, ina uwezo wa kutambua watu wengi wenye homa kali, ndani ya muda mfupi, ambapo hutambua joto la mtu mmoja, ndani ya sekunde chache.

"Sasa hivi mtu anawekea kipimo karibu sana kitendo cha hatari. Kutokana na hilo, tumewaletea kamera hizi ambazo zinaweza kutambua joto la mtu, kutoka umbali wa kutosha. Kamera ionyesha mfano yule mwenye nguo fulani ana joto lisilo la kawaida," alisema na kuongeza:

"Inaweza kumtambua kila mmoja kwa sekunde, na kutambua watu wengi kwa wakati mmoja."

Hella alisema wameamua kuvumbua teknolojia hiyo, ili kuunga juhudi dhidi ya mapambano ya kudhibiti maambukizi na kuenea kwa virusi hivyo.

"Hizi kamera zinaweza kuwa mbali mita 1.5, wakati vile vifaa vya kupima mtumishi huwa karibu zaidi, lazima umsogelee zaidi mhusika. Ni hatari zaidi," alisema Hella.

Hella alisema kamera hizo zinauzwa kulingana na ubora wake, ambapo kima cha chini, kamera moja inauzwa kuanzia Sh. milioni moja.

"Zipo kamera za kushika mkononi zenye uwezo wa kutambua umbali mrefu na za kufunga. mara nyingi kamera hizi zinatumika maeneo yenye mkusanyiko," alisema Hella.

# CAG abaini shida elimu ya ufundi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amesema amebaini kuwapo kwa dosari katika utoaji wa elimu ya ufundi stadi nchini.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka 2018/19 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa juzi, CAG Charles Kichere, alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilishindwa kufikia lengo la kudahili wanafunzi 1,012,967 wa elimu ya ufundi stadi hadi mwaka 2017/18.

Alisema hadi kufikia mwaka huo, ilikuwa imefanikiwa kudahili wanafunzi 119,184 tu, hivyo kuwa na upungufu wa wananfunzi 893,783.

Alisema ukaguzi wake ulibaini vyuo vilivyotembelewa vilikuwa na asilimia 57 tu ya zana na vifaa vya kufundishia vilivyohitajika. Pamoja na hayo, zana na vifaa vya kufundishia vilivyopo kwenye vyuo hivyo, vilikuwa vimepitwa na wakati na vilikuwa chakavu.

Vilevile, CAG KIchere alisema amebaini ucheleweshaji wa usambazaji wa chanjo na vifaa tiba vya chanjo ya surua, kupooza, kuhara, dondakoo, kifaduro, pepopunda, homa ya ini na kichomi ambao ulifikia hadi siku 11.

Alisema hali hiyo ilisachangia ukosefu wa chanjo kwenye baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema ukaguzi wake pia ulibaini ucheleweshaji katika kubaini na kuwasilisha taarifa za magonjwa ya wanyama na mfumo hafifu wa uthibitisho wa maabara inayosababishwa na maabara kufikiwa na wafugaji wa mjini tu, hasa walio karibu na ofisi za kanda.

"Ukaguzi ulibaini kiwango cha uchanjaji mifugo kilikuwa ni chini ya asilimia 10 na kwa mwaka 2016/17, uchanjaji wa mifugo ulikuwa chini ya asilimia moja," alisema.

"Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Mifuho haikufanya ufuatiliaji wowote kwa mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 kwa sababu hakukuwa na fedha iliyotengwa kwa shughuli hiyo kwa miaka iliyotajwa," aliongeza.




Wasamaria wema, wakiwa wameweka kitambaa chekundu kwenye shimo la muda mrefu lililopo katikati ya barabara katika makutano ya Mtaa wa Zanaki na Mali, jijini Dar es Salaam jana, ili kutoa tahadhari wa vyombo vya moto vinavyotumia barabara hiyo.
**PICHA: JOHN BADI**

## Pikipiki 24 zakabidhiwa kwa maofisa tarafa

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

RAIS John Magufuli, ametimiza ahadi yake aliyoitoa Juni mwaka jana ya kuwapa pikipiki maofisa tarafa nchini.

Pikipiki 24 aina ya Sanlg zimekabidhiwa kwa maofisa tarafa wa Mkoa wa Mwanza kwa lengo la kuwarahisishia utendaji kazi.

Akikabidhi pikipiki hizo kwa niaba ya Rais Magufuli, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwataka kuzitumia kwa shughuli za serikali zilizokusudiwa na kuzingatia maadili ya kazi katika maeneo yao ili kuleta maendeleo kwa wananchi .

" Rais amewaamini maofisa tarafa, akaamua kuwapa nyenzo hizo ambazo ni mali ya Serikali kwa ajili ya kuondoa kilio cha usafiri, hivyo mzitunze kama mnavyotunza ofisi na nyaraka nyingine, sijawahi kusikia sifa mbaya kwa maofisa hawa wa Mkoa wangu," alisema Mongella na kuongeza:

"Sitegemei baada ya kupatiwa chombo hicho cha usafiri ndio hadithi zianze, ninachotarajia pikipiki hizi zitumike kwa matumizi yaliyolengwa ya kusimamia ulinzi na usalama wa wananchi kwa kutunza watu na mali zao, kuhamasisha maendeleo na kusimamia maendeleo ndio kazi yenu kubwa."

Alisema, zitawafanya wafike kila eneo kwa urahisi anategemea akifika kwenye tarafa akute amsha amsha ya maendeleo, kwa sababu watakuwa hawajachoka wakitoka eneo moja kwenda vijiji vitatu vinne wanakagua kisha wanarudi baada ya hapo wanaenda tena vijiji vingine.

Alisema wanapaswa kuwa na mpangilio mzuri wa kazi, na kwamba mwaka huu kuna kazi nyingi za maendeleo, hivyo wahakikishe wanazifanya pamoja na uchaguzi mkuu unaokuja watimize wajibu wao.

Aliongeza kuwa maofisa hao ni kiungo kikubwa katika maendeleo kwani wapo katika kazi zote.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Emmanuel Tutuba, akitoa mchanganuo wa namna pikipiki hizo zitakavyogawanywa kwa maofisa tarafa wa wilaya za mkoa huo, alisema Mkoa huo umepokea jumla ya pikipiki 24 ambazo wamegawiwa maofisa tarafa wote ambapo Wilaya ya Kwimba tarafa 5, Sengerema 5, Magu 4, Misungwi 4, Nyamagana 1, Ilemela 1 na Ukerewe 4.

Naye Ofisa Tarafa Ukara Wilayani Ukerewe James Chuwa, alimshukuru Rais kwa kuwapatia pikipiki hizo, ambazo zitawasaidia katika usafiri kwani awali wamepitia kipindi kigumu katika kuwafikia wananchi.

## Wanafunzi Ihsan wapewa tabuleti kujifunzia nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI kidato cha kwanza na cha pili wa Shule ya Sekondari Ihsan iliyoko Kigamboni, Dar es Salaam, jana walipewa simu kubwa ziitwazo tablets ili wajifunze tokea nyumbani kwa njia ya mtandao wakati wa kipindi hiki cha ugonjwa wa corona.

Tabuleti hizo zimetolewa na taasisi ya Moshi iitwayo Opportunity Education Foundation ili kufanikisha mpango wa wanafunzi kujifunza wakitokea mbali katika likizo ya mwezi mmoja ambayo imeamriwa na serikali ili kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Akizungumza wakati wa ugawaji tabuleti hizo, Mkuu wa Shule hiyo, Hashim Saiboko, alisema tabuleti hizo zina teknolojia ya kuwawezesha walimu kuwafundisha na wanafunzi kwa njia ya mtandao na kwa ratiba kama ilivyo ratiba ya darasani, na kueleza kwamba teknolojia hiyo haiwaruhusu wanafunzi kutumia vifaa hivyo kwa mambo mengine nje ya masomo.

"Teknolojia hii inawaruhusu wanafunzi wakiwa huko huko nyumbani kufundishwa na kuuliza maswali kwa mwalimu wa kipindi husika, na mwalimu kujibu maswali hayo kwa njia hiyo hiyo ya mtandao," alifafanua Saiboko.

Kadhalika, walimu watatoa maswali na kusahihisha majibu ya wanafunzi kwa njia ya mtandao kwa kutumia vifaa hivyo.

"Mfumo huu utawasaidia kuwaandaa wanafunzi kuwa na sifa katika mfumo wa sasa wa soko la ajira. Matumizi sahihi ya teknolojia hii itamfanya mwanafunzi awe mahiri zaidi," aliongeza Saiboko.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Hashim Msuya, aliipongeza taasisi kwa kutoa msaada huo na kusema tabuleti hizo zitawasaidia sana wanafunzi kuongeza ufanisi kwenye masomo yao.

"Mimi ninaamini uwajibikaji kwa wanafunzi wangu utaongezeka kwa kuwa kila mwanafunzi atashiriki kwa kujibu na kufanya kazi zote anazopewa na walimu na kazi hizo zitasahihishwa pia," alieleza na kuongeza kwamba shule itapata uzoefu wa kufundisha kwa njia ya mtandao.

Sabrina Mboya, ambaye alipokea tabuleti kwa niaba ya mwanae, aliupongeza uongozi wa shule kwa jitihada ya kuwaendeleza wanafunzi kwa kutumia teknolojia za kisasa zinayopatikana. "Inafurahisha kumuona mtoto akijifunza kutokea nyumbani bila kuwa darasani," alieleza.

Adam Athuman Saidi, mwanafunzi wa kidato cha pili, aliahidi kutumia kifaa hicho kwa mafanikio makubwa.

HABARI BUNGENI

## Tanesco sasa huduma kwa mtandao kisa tishio corona

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) mkoa wa Kagera, linaunga mkono juhudi za Serikali zinazohimiza wananchi kuendelea kupambana kujikinga na ugonjwa wa virusi vya Corona (COVID-19), kwa kutoa huduma ya kiofisi kwa wateja kwa njia ya mtandao.

Lengo la hatua hiyo ni kuepusha msongamano unaoweza kusababisha maambukizi ya ugonjwa huo.

Hayo yalisemwa na Ofisa Uhusiano wa Tanesco mkoani hapo, Samuel Mandari, wakati akitoa maelezo kwa wateja waliofika ofisi kwake kwa ajiri ya kutatuliwa changamoto.

Mandari alisema hatua hiyo itasaidia kuondoa msongamo wa wananchi ambao wanafika kupata huduma mbalimbali zinazotakiwa kufanyiwa utatuzi na shirika hilo.

Aidha, alisema kwa kutambua kuwa nchi ipo katika mapambano ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu kwa wananchi, lazima kuwe na tahadhari zinazotangazwa na wataalamu zifuatwe na wananchi kwa kutoruhusu mikusanyiko.

"Sisi kama Tanesco Kagera, tumeanza utoaji wa huduma kwa njia ya mtandano licha ya kwamba njia hii ilishaanza tangu Machi mwaka huu na ndiyo mtazamo wa shirika, ambao unalenga kumpatia huduma kila mwananchi" alisema Mandari.

"Njia hii pia itaondoa garama ya kutumia muda kuwafuata ofisi na gharama na nauli ambavyo akijiunga kwenye mtandao inakuwa rahisi sisi kumfikia mahali alipo na kutatua shida zao kwa haraka, kwani taarifa inatufikia mapesa na kwa haraka," alisema Mandari.

Alisema huduma zinazofika ofisni hapo ni utatuzi wa changamoto, uhitaji wa huduma ya umeme mijini na vijijini, maombi ya upatikanaji wa umeme, ambayo yanafanyiwa kazi ndani ya shirika.

Alisema mkoa huo una wateja zaidi ya 100,000, hivyo kuna ulazima wa kutoa Huduma kwa njia ya simu, barua pepe na mitandao ya kijamii kwa kila mwananchi alie na uwezo kutumia njia hizo.

Aliongeza kuwa, katika maeneo ya ofisi wasaidizi wa shirika hilo wameweka vifaa vya kuoshea mikono kwa kila mtu anayeingia na kutoka kipindi chote.

**"Njia hii pia itaondoa garama ya kutumia muda kuwafuata ofisi na gharama na nauli ambavyo akijiunga kwenye mtandao inakuwa rahisi sisi kumfikia mahali alipo na kutatua shida zao kwa haraka, kwani taarifa inatufikia mapesa na kwa haraka," alisema Mandari.**

# Serikali kuzipa benki nchini unafuu mikopo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema serikali itatoa unafuu kwa mabenki ili kufanya 'Loans Resheduling' ili kukabiliana na athari za kiuchumi zitokanazo na ugonjwa wa corona.

Aidha amesema kimeundwa kikosi kazi maalum cha wataalamu kwa ajili ya kuangalia athari za kiuchumi zitokanazo na ugonjwa huo.

Akichangia hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2020/21, Waziri Mpango alisema kikosi hicho kinafanya kazi ya uchambuzi wa kina wa athari zinazoweza kujitokeza na kuwa kazi hiyo inatakiwa kufanyika kwa umakini.

"Na ndio uweze kuwa msingi wa kuandaa programu ya kiuchumi ya kukabiliana na janga hili, bila hivyo tutaendelea kuwa 'alarmist' lakini bila 'facts' kutoka kwenye sekta mbalimbali ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaandaa mikakati ambayo ni ya uhakika,"alisema.

Alisema timu hiyo inajuyomuisha watu kutoka Zanzibar, wako katika kamati ya kitaalamu, lakini pia kwenye kamati ya kitaifa ambayo inaongozwa na Waziri Mkuu, pia katika Wizara ya Fedha imeelekeza wizara zingine za kisekta ikiwamo Benki Kuu kukutana na wadau mbalimbali kwa majadiliano mbalimbali ili wapokee mapendekezo yao.

"Tumeanza kupata mapendekezo, ni kutoka kwa Chama cha utalii, umoja wa mabenki Tanzania, wawindaji, shirikisho la vyama vya utalii, Taasisi ya sekta binafsi na wadau wengine," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (kulia), akikabidhi pikipiki 24 kwa maofisa tarafa wa mkoa huo, jijini Mwanza juzi. Habari uk. 9. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Watakaokaidi kunawa mikono kukamatwa

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

SERIKALI mkoani Shinyanga, imesema kuwa yeyote atakayekamatwa kwa kutotekeleza maelekezo ya kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka, atachukuliwa hatua kali pamoja na kupelekwa Polisi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, aliyasema hayo jana wakati akikabidhi vifaa vya kujikinga na corona kwa Mganga Mkuu wa mkoa wa Shinyanga. Dk. Yudas Ndungile.

Alisema Serikali imeshatoa elimu ya kutosha kwa wananchi, kuchukua tahadhari ya kujikinga na corona, pamoja na kukagua vifaa vya kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka, na kubainisha kinachofuata ni msako kwa wale ambao hawatakuwa wakinawa mikono, na kuwachukulia hatua pamoja na kuwapeleka Polisi.

"Tumeshatoa elimu ya kutosha, hakuna mahali ambapo hatujapita, sasa ni wakati wa kuchukua hatua kwa wale ambao kwa makusudi kabisa wanakataa kunawa mikono, tutawapiga faini na wale ambao watakaidi kabisa tutawapeleka kituo cha polisi ili hatua nyingine zichukuliwe," alisema Telack.

"Na nyinyi watoa huduma za afya naomba muwe mstari wa mbele kuhakikisha mnapoingia hospitalini, mnawe mikono yenu na kuonyesha mfano, ili wananchi waige kutoka kwenu," aliongeza.

Aidha, alisema vifaa hivyo vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwa wahudumu wa afya mkoani Shinyanga, vimetolewa na wadau mbalimbali wa afya zikiwamo, Surgical gloves, Non Sterile gloves, barakoa 'Mask', vidonge vya Chrorine na pamba vikiwa na jumla ya thamani ya Sh. milioni 10.7.

Mganga Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alipongeza utolewaji wa vifaa hivyo, ambavyo vitawakinga watakapokuwa wakimhudumia mgonjwa wa corona, na kubainisha kuwa mpaka sasa mkoani humo hakuna mshukiwa wa virusi hivyo.

# Wanandoa watakiwa kuwa waangalifu magonjwa hatari

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

WANANDOA wametakiwa kuchukua tahadhari na kuepuka mapenzi ya kinywa , ambayo yanadaiwa kuwa chanzo cha kupata maambukizi ya magonjwa mengi, ukiwamo corona na Ukimwi.

Tahadhali hiyo ilitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Kinywa na Meno wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Edward Magoma, wakati akizungumza na Nipashe.

Dk. Magoma alisema mdomoni kuna bakteria wengi, hivyo wanaopenda kutumia mdomo kwenye starehe zao, hujiweka kwenye hatari ya kupata magonjwa ya fizi au ugongwa wa Ukimwi.

"Sisi hatuzuii ila kitu kikubwa ni kufahamiana afya kwanza za watu wa namna hiyo, ili kuepuka kupata magonjwa ," alisema Dk. Magoma.

Aidha, alisema hatari zaidi inakuja wanandoa hao akiwa na tatizo la kutokwa damu kwenye fizi, maambukizi kwa mwenzi wake ni rahisi.

Mkazi wa Babati, Asha Husein, akizungumzia suala hilo, alisema watu wanatakiwa kujiridhisha na afya ya mwenzi wake kabla ya kufanya mapenzi hayo.

Mkazi wa Negamsi, Neema Bura, alisema hajui kuwa kufanya hivyo anaweza kupata ugonjwa na aliwashauri wataalamu kutoa elimu hiyo kwa umma ili afahamu na kuepuka katika kitendo hicho.

## Kifaa maalum cha unawaji wa mikono chabuniwa

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), kupitia mradi wa 'WASH SDG', wamebuni kifaa maalum cha kunawa mikono kwa kutumia miguu kuruhusu maji na sabuni badala ya kutumia mikono.

Akizungumza jana na Nipashe jijini Arusha, Ofisa Ufuatiliaji wa Magonjwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha, Allan Rushokana, alisema wamebuni kifaa hicho ili kudhibiti usambazaji wa wadudu waenezao magonjwa kama corona na magonjwa mengine.

"Hapa unatumia miguu 'Foot Press" kuruhusu maji na sabuni kutoka, wakati wa kunawa mikono bila kugusa mahali popote kwenye kifaa hiki," alisisitiza.

Allan alisema ubunifu huo ni sehemu ya kampeni maalum inayotekelezwa jijini Arusha, inayojulikana kama mazingira safi maisha bora inayolenga kuboresha hali ya afya na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Aidha, alisema ili kuleta chachu ya matumizi ya kifaa hicho, wanalo jukumu la kuhamasisha mafundi mchundo kutengeneza kifaa hicho kwa wingi, ili kifikie jamii katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Jiji la Arusha, huku kipaumbele zaidi ikiwa ni sehemu zenye mikusanyiko kama stendi za mabasi, sokoni, ofisi za umma, kanisani ,vituo vinavyotoa huduma za afya na taasisi mbalimbali.

"Kifaa hiki kizuri sana kukitumia kwa sababu wakati wa kunawa mikono mtu hashiki kwa mikono yake kufungulia maji bali anatumia miguu yake kuruhusu maji na sabuni na mikono hubaki salama," alisema.

Nae Meneja wa mradi wa Wash SDG Proramme Tanzania, Olivier Germain, alisema baadhi ya faida za kutumia kifaa hicho ni pamoja na urahisi wa kukitumia na kina matumizi madogo ya maji, ukilinganisha na vifaa vingine wanavyotumika kunawa mikono.

"Lakini kizuri zaidi katika kuhifadhi mazingira, kina uwezekano wa kuelekeza maji yaliotumika kunawa mikono kwenda kwenye mfumo wa majitaka na kinazuia usambazaji magonjwa kutokana na mtumiaji kutoshika kwa mikono kuruhusu maji na sabuni," alisema.

**"Kifaa hiki kizuri sana kukitumia kwa sababu wakati wa kunawa mikono mtu hashiki kwa mikono yake kufungulia maji bali anatumia miguu yake kuruhusu maji na sabuni na mikono hubaki salama," alisema.**




Ofisa ufuatiliaji wa magonjwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Arusha, Allan Rushokana, akionyesha jinsi ya kunawa mikono kwa kutumia mguu kuruhusu maji na sabuni kutoka kwenye kifaa maalum jijini humo jana, kilichobuniwa na Halmashauri hiyo, kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), kupitia mradi wa 'WASH SDG', ili kuepusha watumiaji kupata magonjwa mengine ukiwamo wa Corona, kwa kushika kitufe cha kuruhusu maji. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Azaki sasa kuisaidia serikali vita ya corona

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MASHIRIKA yasiyo ya kiserikali jijini Arusha, wamekutana na kuweka mikakati ya kusaidiana na serikali, katika vita ya kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19.

Wakizungumza katika ukumbi wa Zimamoto jijiji Arusha, wakati wa kikao cha kuweka mikakati ya kushirikiana na serikali na wadau wa afya, katika harakati za kupambana na ugonjwa huo, walisema wanaunga mkono jitihada za serikali na tayari wameanza kutoa elimu kwa wananchi wanaohudumia jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.

Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) mkoani Arusha, Nina Nchimbi, alisema amefarijika kuona wadau wa maendeleo wakishirikiana na wadau wa afya, katika kukabiliana na ugonjwa wa COVID 19.

"Kweli katika kupambana na maambukizi ya ugonjwa huu inahitajika nguvu ya pamoja, kukabiliana na ugonjwa huu na Sido iko mstari wa mbele katika kukabiliana na ugonjwa huu ili kila mmoja aendelee na shughuli zake za uzalishaji mali,"alisema.

Nina alisema kuwa, afya njema ni mali na lazima kila mtu ahakikishe ulinzi wa afya yake na mwenzake, ili hatimaye kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo.

Mratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), Ahadi Msangi, alisema mashirika yasiyo ya kiserikali ni wadau muhimu katika maendeleo ya wananchi na serikali inatambua mchango wake na ndiyo maana wameona umuhimu wa kuwakutanisha, ili kupokea michango yao.

"Sisi tunahitajika kushirikiana pamoja na serikali na kutoa michango yetu ya hali na mali, ili kuwezesha kukabiliana ugonjwa wa COVID 19 nchini kuwe rahisi na mwisho tuishinde vita hii inayoangamiza dunia," alisema.

Ofisa Afya Jiji la Arusha, Omary Omary, alisema, kampeni za kukabiliana na ugonjwa huo ,inahitaji nguvu ya pamoja ya wadau na amefurahi kuona jinsi wadau kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali walivyojitokeza katika kikao hicho na kutoa ahadi ya kusaidia serikali, katika kutoa elimu kwenye maeneo yao ya jinsi ya kukabiliana na ugonjwa huo

Naye Katibu wa Muungano wa Mashirika yasiyo ya kiserikali, Mkoa wa Arusha ACUNGOS, Laurent Sabuni, alisema amefarijika kuona serikali inatambua mchango wao na wapo tayari kutoa elimu ya ugonjwa huo, katika maeneo wanaofanyia kazi na wataendelea kuunga mkono jitihada za serikali na wadau wa afya kuukabili ugonjwa huo .

Alisema mashirika yasiyo ya kiserikali ni washirika wa maendeleo katika nyanja zote na kudai kuwa, afya bora ndiyo msingi wa maendeleo na kuhimiza wadau wa afya, kushirikiana na serikali kukabiliana na ugonjwa wa COVID -19 huku wakihimiza watu kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya kuhusu ugonjwa huo.

# Vijana wajikita uelewa ulingano wa ulimwengu

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

IDADI ya vijana wa kitanzania waliojikita kuelewa zaidi juu ya ulingano na utengamano wa ulimwengu kuhusu elimu ya maendeleo, inazidi kuongezeka siku hadi siku, Shirika la Tanzania Youth Coaliation, limeeleza.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jana kuhusu elimu hiyo, Mratibu wa Miradi wa Shirika la Tanzania Youth Coaliation, Erick Nyoni, alisema vijana hao wanajiandaa kutumia fursa za kiuchumi ili kuboresha maisha yao na uchumi wa Tanzania.

"Kupitia mradi wa ASA, vijana hawa wanaendelea kujifunza elimu ya maendeleo na kuelewa zaidi juu ya ulingano na utangamano wa ulimwengu, huku wakijiuliza maswali ya kina ya namna wanavyotaka kuimarisha taifa lao kuwa endelevu na lenye usawa," alisema Nyoni.

Alisema mradi huo unalenga kuwajengea uwezo vijana ambao ni wanawake na wanaume kuyafahamu masuala ya utangamano na ulingano wa fursa za kiuchumi.

Miongoni mwa mambo wanayojifunza ni pamoja na utambuzi wa fursa za kiuchumi na namna wanavyoweza kusimama katika ushindani wa elimu.

Kwa mujibu wa Nyoni, kuna fursa nyingi za kiuchumi zilizoko katika nchi za Afrika Mashariki, ndio maana wanawaandaa vijana wa Kitanzania kuzichangamkia ipasavyo ili kuboresha maisha yao.

Alisema serikali za nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatumia fedha nyingi kuibua fursa mbalimbali za kiuchumi na kwamba vijana hawana budi kutumia fursa hizo kujinufaisha kupitia fursa hizo.

Aidha, alitoa wito kwa vijana watakaojaliwa kujiingiza katika biashara na ujasiriamali kuhakikisha wanazalisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu ili kulinda masoko waliyoyapata na kuongeza masoko mengine.

**"Kupitia mradi wa ASA, vijana hawa wanaendelea kujifunza elimu ya maendeleo na kuelewa zaidi juu ya ulingano na utangamano wa ulimwengu, huku wakijiuliza maswali ya kina ya namna wanavyotaka kuimarisha taifa lao kuwa endelevu na lenye usawa," alisema Nyoni.**

# Ukatili wa kijinsia washika kasi Same

**Na Godfrey Mushi, SAME**

MAOFISA wa serikali katika Wilaya ya Same, wamesema kata nne zilizopo nje ya mji wa Same, ni tishio kwa matukio ya ukatili wa kijinsia licha ya elimu kutolewa na wabia wa serikali.

Kata zinazotishiwa na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ni Ruvu, Kisima, Stesheni na Same.

Akizungumzia vitendo hivyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Charles Anatoly, amekiri kuwa maeneo hayo ni tishio na kwamba serikali inafanya kila iwezavyo kutoa elimu na kushughulikia baadhi ya matatizo yanayochipua au kuonekana kukomaa katika jamii.

"Viko visa vingi ambavyo vinaashiria kwamba maeneo hayo ni tishio kwa ukatili hasa kutokana na kuchipua kwa visa vipya vya kuoza wanafunzi, vipigo kwa wanawake, watoto kukatisha masomo ili kwenda kuchunga mifugo, ndoa za utotoni, vitendo vya udhalilishaji wa kingono na mfumo dume katika baadhi ya koo za jamii ya wafugaji," alisema.

Aidha, Ofisa Maendeleo, Benedict Misani, alinukuliwa na Nipashe hivi karibuni, akieleza kuwa ili kupunguza matatizo hayo serikali inakusudia kuimarisha uchumi wa familia na kaya zake.

Alieleza mkakati huo wa serikali, alipokuwa akitoa taarifa kuhusu hali halisi ya ukatili kwa wanawake na watoto, mbele ya wajumbe wa kamati ya Mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa).

Misani zaidi alifafanua akisema: "Muongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, unataka na unaelekeza tupanue mpango wa uimarishaji mifumo ya ulinzi na usalama wa mtoto katika kila halmashauri, tuwe na uhamasishaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama kwa watoto.

"Lipo pia suala la utoaji huduma za msaada wa kisaikolojia kwa familia na watoto waathiriwa wa vitendo vya unyanyasaji na ukatili na hasa tumeelekezwa kufanya ufuatiliaji na tathimini ya shughuli za ulinzi na usalama kwa watoto na masuala ya mila na desturi."

Alisema ukatili wa ngono unaongezeka kulingana na umri wa mwanamke, kwa mfano asilimia 11 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 19, walifanyiwa ukatili huo ukilinganisha na asilimia 18 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 40 hadi 49 kwa mujibu wa Ripoti ya Upimaji wa Demografia na Afya Tanzania (TDHS 2015/16).

"Kwa hili la unyanyasaji wa kingono, watoto 3 kati ya 10 ambao ni wasichana na mtoto 1 kati ya 7 wa kiume wamefanyiwa ukatili kabla hawajafikisha umri wa miaka 18,

Wakati unyanyasaji wa kimwili ni asilimia 72 kwa watoto wa kike na asilimia 71 ya watoto wa kiume wamefanyiwa ukatili kabla hawajafikisha umri wa miaka 18,"alisema.

Alisema kulingana na taarifa ya utafiti, asilimia 60 ya ukatili dhidi ya watoto hutokea nyumbani na asilimia 50 hutokea shuleni.



Wananchi wa Bassotu, wakishuhudia maji ya mvua yaliyozingira makazi ya watu kutokana na mvua kubwa iliyonyesha mkoani Manyara jana. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Agizo la DC ujenzi wa zahanati lawapa wakati mgumu watendaji

**Na Godfrey Mushi, HAI**

AGIZO la Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, la kuwataka watendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya kwa Tito ndani ya siku 14, linawatoa jasho viongozi wanaohusika na mradi huo wa ujenzi.

Jana, Nipashe limeshuhudia viongozi wa Kata ya Weruweru inapojengwa zahanati hiyo, wakipishana kwa zamu kusimamia shughuli za ujenzi ili kukwepa mkono wa Mkuu huyo wa Wilaya kuwawajibisha kwa kushindwa kutekeleza agizo lake.

Alipoulizwa kuhusu maendeleo ya ujenzi huo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha kwa Tito, Olivia Mwasamba (VEO) alisema: "Ndugu yangu hatulali, hapa kila kiongozi anakuja kuchungulia mambo yanaendaje, tunachakarika kumaliza ujenzi wa zahanati ya kwa Tito ambayo Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya) alitoa siku 14 iwe imekamilika lasivyo tutawajibika."


Aprili mosi mwaka huu, Ole Sabaya alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya hiyo kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Kwa Tito ndani ya siku 14 ili kusogeza huduma za afya kwa wananchi wa Kijiji hicho.

Ole Sabaya alitoa agizo lake, wakati alipokwenda kukagua maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya afya katika Kata ya Weruweru.

Kutokana na kusuasua kwa ujenzi wa zahanati hiyo, aliwashutumu wataalamu kwa kuchelewa kufanya uamuzi sahihi katika kukamilisha ujenzi huo, kwa vile fedha za kazi hiyo zilishaletwa na serikali tangu mwezi Agosti mwaka jana.

Zahanati hiyo ya kwa Tito iliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi tangu mwaka 2009, inatarajiwa kuhudumia zaidi ya kaya 250 na wananchi wa vijiji jirani zaidi ya 1,000

Diwani wa Kata ya Weruweru ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Ujenzi ya Halmashauri hiyo, Swalehe Juma, allipoulizwa kuhusu maendeleo ya ujenzi huo alisema kazi hiyo kwa sasa inakwenda vizuri na wanatarajia agizo hilo litakamilika katika muda uliotolewa.



**Karume kutambua uwezo, dhamira safi ya Nyerere kulinusuru historia**

Ukurasa 14

## UN yalia ubaguzi watoa huduma utakavyomaliza weusi na corona

Ukurasa 17





Ukurasa 19

**Sasa ni rasmi Prof. Tibaijuka kuliachia jimbo Muleba Kusini**


# siasa

JUMATANO APRILI 8, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 15

**'Karume Day' cheche ya kuuenzi zaidi Muungano**

MIAKA 48 BILA KARUME

# Bado anasifika kuimarisha karafuu Z'bar

**Na Haji Nassor,** PEMBA

KATIKA karne ya 19, Zanzibar ilikuwa chini ya utawala wa Sultan wa Oman na mwaka1830 ilikuwa inaongoza kwa kilimo cha karafuu duniani.

Uongozi wa Sultani wa Zanzibar ulianzishwa mwaka 1856, wakati Sultani Sayyid Said, alipoamua kuhamisha makao makuu yake kutoka Maskat-Omani na kuyahamishia kisiwani Unguja.

Kwa wakati huo, mtawala huyo, aliona nafasi kubwa ya biashara ya karafuu kwa ajili ya soko la Uhindi na kwingineko. Ingawa

INAENDELEA UK.16



Wanavijiji wakichambua karafuu kuzipanga katika madaraja mbalimbali , bei ya karafuu daraja la kwanza ni Shilingi 14,000 kwa kilo. **PICHA: MTANDAO.**

**Licha ya kuondoka fikra zake zinawaongoza Wazanzibari**


Ukurasa 18

URITHI WA KARUME

# Kutambua uwezo, dhamira safi ya Nyerere kulinusuru historia



Abeid Amani Karume



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

**Na Ani Jozeni**

NCHI za Afrika kwa haraka zina makundi mawili katika historia za siasa, yale ambayo yamekuwa na umoja na utulivu, hivyo kuweza kuwaenzi waanzilishi waliyoyafikisha mataifa hayo katika uhuru, na wale ambao hawana mazingira kama hayo.

Katika nchi ambazo zimepitia mikondo tofauti na dhoruba zilizopepeta taifa na kutesa au kufisha maelfu ya raia , siyo rahisi walioasisi hali hiyo kukumbukwa kwa heshima na taadhima.

Wanakuwa tu sehemu ya historia, na msomi akitaka kuzungumza habari zao anangalia kwanza yuko na nani na wanatazamia nini?

Zanzibar ingedumu katika usultani halafu 'wazawa' wakaanza kuingia serikalini au kupanda kufika vyeo vya juu hatua kwa hatua ingekuwa na mandhari tulivu na uwezo wa kumbukumbu kama ilivyo Tanzania Bara, lakini sumu ilishapandwa kabla ya hapo.

Ni wazi utafiti wa kutosha upo unaoeleza bayana kwanini uhasama ulikuwa mkubwa kati ya ukoo uliotawala Zanzibar na waliokuwa karibu nao ambao kimsingi walitwa Waarabu licha ya historia kuonyesha kuwa zaidi walikuwa Wamanyema waliooana na Waarabu. Hapakuwa na koo halisi za Kiarabu za Unguja.

> "Mpasuko wa Zanzibar kisiasa unafanana na Uganda, Rwanda na Burundi, na ni muungano uliozuia Zanzibar isifuate njia hiyo.

Mara nyingine suala ni kuangalia aina gani ya mahusiano ya jumla lilikuwepo pamoja na kuwa chanzo halisi cha uhasama ni harakati za kitabaka, kihistoria zinazoelezea hali hiyo kwa ujumla wake.

Hivyo, hata katika uchaguzi wa mwaka 1961 (ambako machafuko yalifuata) tofauti za msingi zilichanganya watawala na wazawa upande mmoja, na wazawa kundi lingine halafu siasa za kimapinduzi upande wa pili. Andiko moja la historia linasema kuwa baada ya uchaguzi Januari 1961 yalitokea machafuko wiki nzima ambako Waarabu takriban 68 waliuawa.

Suala la msingi hapa ni kuwa utawala wa kisultani uliohamia kutoka Oman kufanya Zanzibar iwe ndiyo makao makuu yake ulijenga uchumi wa kitumwa kisiwani Unguja ambako wenyeji waliondolewa katika ardhi na walowezi wakaanza kulima karafuu.

Waafrika walitumika kwanza kama watumwa na baadaye kama manamba, hawakupanda katika ngazi halisi kijamii, baadaye wakawa pamoja na wafanyakazi wa kawaida wengine wa bandarini, na hata 'polisi aliyefukuzwa kazi' kama 'Field Marshal' John Okello.

Kisiwani Pemba wakulima wa jadi waliingizwa katika kilimo cha karafuu bila kupoteza ardhi yao, wakawa na ngazi tofauti kijamii na wale wa Unguja.

Ni kutokana na mpasuko huo wa jadi kuwa wazawa walio wengi kisiwani Unguja walikuwa hawana uwezo wa kufikiria jema kwa walowezi, wakati wale wa Pemba walipata nafasi ya kushirikiana nao kwani watu wa karibu wa Sultani wasingeweza kusimamisha utawala wao kutumia ufuasi kisiwani Unguja.

Ingebidi Uingereza iendelee kudhibiti eneo hilo ili amani iwepo, au kuwe na hali kama ya Comoro ambako Ufaransa haikuondoka, lakini Uingereza ilikuwa na dhamira ya kuachia makoloni au 'maeneo yanayolindwa na Malkia' (protectorates).

Walipoachwa peke yao, wakashindwa kuimudu dola, kwani polisi wasingezuia wimbi la hasira.

Kukwama kwa Zanzibar tulivu yenye historia ya Kiarabu na utamaduni wa pwani ambayo ndiyo inajitokeza katika majarida ya kitalii kulitokana na kutowapa ardhi wenyeji wa Unguja.

Halafu ghasia zilizofuata uchaguzi wa Januari 1961 na miaka miwili baadaye maelfu ya waliokuwa karibu na Sultani pamoja na wafanyabiashara wengine ambao mali zao ziliporwa na wengi tu kuuawa katika mapinduzi kulikuweka jeraha la kijamii ambalo lingezuia amani na utulivu, hata kuweza kutunza historia ya mabadiliko na kuyaenzi kila mwaka.

Mpasuko wa Zanzibar kisiasa unafanana na Uganda, Rwanda na Burundi, na ni muungano uliozuia Zanzibar isifuate njia hiyo.

Kifo cha Rais Abeid Karume kwa risasi Aprili 7 1972, miaka minane baada ya mapinduzi, ni kielelezo halisi cha hali iliyoingojea Zanzibar endapo ingesimama yenyewe kama dola. Tofauti na baadhi ya watu walivyozoea, kuwa bila muungano Waarabu wangerudi, uhalisia ni kwamba kila utawala lazima uwe na sehemu ya nchi (wazawa, walio wengi) ambapo wangejikita, na kwa Zanzibar ingebidi Mwarabu akitaka atawale tena basi Pemba ijitenge, kwani asingekuwa na ushawishi wowote Unguja hata wa kuunda serikali ya kijeshi apate mamluki.

Hali hiyo ya machafuko haikufikiwa kwani juhudi zilianza kuleta Muungano, kutokana na maelewano ya miaka kadhaa kati ya viongozi wa kundi lililounga mkono mapinduzi, na Rais Julius Nyerere.

Urafiki huo ulikuwa ndiyo jambo Mwalimu alilolifanya katika maisha yake ya kisiasa pale mwanzoni ambalo alilithamini kuliko yote, au labda alipata furaha ya ndani ya hisia zake kuwa amefaulu jambo kubwa.

Unaweza kusema alifaulu jambo kubwa zaidi kuliko alivyofikiria, kwani umuhimu wa kuunganisha Shirazi Association (wafuasi wake walitoka Pemba zaidi, ila ni miongoni mwa wananchi wa kawaida au hata wafanyabiashara wadogo, si waliojiona wako karibu na Waarabu) na African Association (kundi la wazawa Unguja) lilikuwa ni kuunganisha nguvu kupata uhuru, au kuunda serikali baada ya hapo.

Licha ya kuwa ubabaishaji wa Sultani au watu wake wa karibu ulihakikisha kuwa viti vingi zaidi vinaenda kwa mafariki zao, walishinda.

Walichokikosa kutokana na ubabaishaji kilipatikana katika mapinduzi, lakini hali hiyo iliacha dondandugu katika siasa za Zanzibar ambalo lingehakikisha kuwa hata siku moja amani isingepatikana, labda baada ya miaka 50 kama ambayo aliwahi kughani Shaaban Robert.

Ina maana kuwa Zanzibar huru ingepigwa na wimbi moja halafu jingine la kisiasa, visiwa hivyo vingetengana kama ilivyo kwa Comoro (Pemba iko mbali mno na Unguja isingeweza kuidhibiti) na historia ya jinsi mapinduzi yalivyofanyika ingesahaulika.

Kutokana na Muungano, ambao ulianzia kwa Karume na Sheikh Thabit Kombo kumkubalia Nyerere na kuunganisha vyama vyao kuunda chama cha Afro-Shirazi Februari 5, 1957 ndiyo siri ya mafanikio, umoja, kumbukumbu.

Bila hatua hiyo Nyerere angeangalia tu kwa mbali Zanzibar ikiungua, na hata kama mapinduzi yangedumu, mpasuko na Pemba halafu visasi Unguja, mapinduzi ya kijeshi, vingesahaulisha kumbukumbu hiyo na kusingekuwa leo na Siku ya Karume.

# 'Karume Day ' cheche ya kuuenzi zaidi Muungano

Na Mwandishi Wetu

MIAKA 48 imetimia tangu kuuawa kwa risasi kwa Muasisi wa Taifa la Zanzibar Aprili 7, 1972, mwanamapinduzi Abeid Amani Karume.

Karume licha ya kuwa ameondoka miongoni mwa Wazanzibari na Watanzania lakini anaendelea kukumbukwa kwa mambo mengi ikiwamo kuwapenda wananchi.

Kwa ujumla rais huyu wa kwanza wa Zanzibar na mwasisi wa Tanzania Mwalimu Julius Nyerere wote waliwapenda Watanzania.

Tunapokumbuka siku ya kifo cha Karume aliyezaliwa Mei 1905, Wazanzibari na Watanzania Bara wana jukumu la kuuenzi na kuudumisha Muungano ambao waasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliuanzisha, kuulea na kuusimamia.



Walimu na waanzilishi wa Muungano Nyerere na Karume wataendelea kukumbukwa kwa kuimarisha udugu wa Tanzania na Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

### FAIDA ZA MUUNGANO

Muungano huo ulioanzishwa na Nyerere pamoja na Karume miaka nane kabla ya kuuawa kwa shujaa wa Mapinduzi ya Zanzibar, ni ishara ya umoja, upendo, mshikamano, ushirikiano na amani baina ya mataifa hayo mawili.

Mara kadhaa kumekuwa na hoja za kutaka kuuangalia tena Muungano . Mathalani, mambo yaliyojiri wakati wa Bunge la Katibu ambalo kulikuwa na hisia za kuwa na Muungano wa Serikali tatu ambazo ni ya Zanzibar, Tanzania Bara na ya Muungano.

Japo wengi wanaweza kufahamu umuhimu wa Muungano, ni vyema kuendeleza mema ya Karume na Nyerere kwa kuzingatia faida za umoja na mshikamano baina ya mataifa haya.

Baadhi ya faida ni pamoja na mosi Muungano huo ulioanzishwa na waasisi hao ndiyo uliowapa amani na utulivu Tanzania na Zanzibar tunu zinazoonekana hata sasa.

Muungano ndiyo uliokuza na kudumisha umoja ,upendo na mshikamano unaoonekana leo ikiwa ni pamoja na Watanzania Bara na Wazanzibari kuvua katika bahari na kufanya biashara mbalimbali bila kuwa na uhasama miongoni mwao.

Tanzania ina kila sababu ya kulinda Muungano huo ulioasisiwa na Karume na Nyerere kwa gharama yoyote na pia ikijiaminisha kuwa dunia ya leo mataifa yanaendelea kuungana si kutengana.

Ndiyo maana kuna Umoja wa Ulaya ambao licha ya kuwa na sarafu ya Yuro una viza moja , bunge na mipango na mikakati ya kiuchumi inayouwezesha kusimama kama mhimili mkubwa duniani kiuchumi, kisiasa na kwenye masuala ya ulinzi wa mazingira na rasilimali zake.

### RAIA WAHUSIKE

Ni vyema kukumbuka kuwa ni wajibu wa Watanzania na viongozi kuulinda Muungano na kwamba si kitu cha mtu binafsi, wala si wa viongozi ni wa Watanzania wote bila kujali ukabila, dini, rangi, ukanda au aina yeyote ya tabaka.

Hivyo kila raia ana jukumu la kuona ana wajibu wa kuutetea na kuuthamini kuwa ndicho kitu pekee kinachowaunganisha na kuwaweka pamoja Watanzania .

> Tanzania ina kila sababu ya kuulinda Muungano huo ulioasisiwa na Karume na Nyerere kwa gharama yoyote na pia ikijiaminisha kuwa dunia ya leo mataifa yanaendelea kuungana si



Karume akiwa na mwanasiasa maarufu viswani Zanzibar Abrahaman Babu (kulia) katika harakati za kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

Ni vyema raia kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Muungano huo unadumu. Kila wakati ni vyema kukemea wale wote wanaonyemelea kuhatarisha Muungano huo ili udumu hata kama ni viongozi wenye mamlaka za juu.

Halikadhalika, viongozi nao wawe mstari wa mbele kuulinda na kuutetea Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Watambue kuwa wana wajibu wa kuudumisha na kuulinda pamoja na kuutetea Muungano katika hali yoyote na kwa kuufanya hivyo wataudumisha.

Ikumbukwe Muungano ni tunu ya taifa iliyoachiwa Watanzania kutoka kwa waasisi wa taifa hili ambalo ni la Watanzania na Wazanzibari.

Katika kurekebisha kasoro zinazotolewa na wadau mbalimbali, serikali iruhusu wananchi kueleza kile wanachofikiri kinafaa kuuimarisha Muungano na kama inawezekana kuwe na majukwaa mbalimbali ya kutoa maoni na kupendekeza njia za kudumisha na kuboresha muungano huo.

Jukumu hilo likiratibiwa na ofisi ya Makamu ya Rais ambayo ndiyo yenye jukumu la kusimamia masuala ya Muungano.

MIAKA 48 BILA KARUME

# Bado anasifika kuimarisha karafuu Zanzibar

INATOKA UK.13

baadaye aliaanzisha mashamba ya karafuu kwa kutumia kazi za wananchi wa Zanzibar ambao kwa wakati waliitwa watumwa.

Baada ya kifo cha Sayyid Sultan, usultani wa Oman uligawiwa kati ya wanawe, Sayyid Majid bin Said Al-Busaid kuanzia mwaka 1834/1835-1870, akawa Sultani wa kwanza wa Zanzibar na kaka yake Sayyid Thuwaini bin Said al-Said akawa Sultani wa Oman akitawala nchi hiyo.

Hata hivyo, si kwamba Wazazibari walikaa kimya na kufurahia taifa lao likigawanywa, Jemedari wa Taifa Sheikh Abed Amani Karume, alikuwa na mbinu za chini kwa chini, ili kuhakikisha nchi inakuwa huru na wazalendo wanafaidika na uchumi wao kupitia zao la karafuu.

Mwaka 2020 tukiwa katika kumbukumbu ya siku ya kifo cha Karume kila mmoja hata aliyezaliwa mwaka juzi, ataona jinsi Sheikh Abeid Amani Karume, alivyopigania kwa dhati haki ya Mzanzibar kujitawala.

Mwaka 1972, kwa Wazanzibari na wapenda maendeleo walipigwa na butwaa, kwenye nyoyo zao, kutokana na wakatili kuondoa uhai wa Rais wetu wa kwanza na kipenzi cha Wazanzibari.

Baada ya wazalendo wa Zanzibar kuteseka sana wakiwa ndani ya nchi yao, Januari 12, 1964 yakatokea Mapinduzi ya Zanzibar, yaliomuondoa madarakani Sultani wa Zanzibar na serikali yake.

Kwa hapa, rais huyo wa kwanza na wenzake, walifanya mapinduzi halali, ambayo yalikuwa na malengo kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuuweka uongozi mikononi mwa Waafrika wenyewe, ambao ndiyo wenye haki ya kufaidi uchumi wao.

**NGUZO YA UCHUMI Z'BAR**

Uchumi wa wananchi wa Zanzibar hasa ulianza kupewa nafasi na Rais Karume, kuanzia mwaka 1964, baada ya kumfyeka Sultani na kisha kuamua kugawa eka tatu za ardhi tena bila ya ubagauzi kwa wananchi.

Makame Hamad Makame (85), mkazi wa Makoongwe wilaya ya Mkoani Pemba, anasema kama kuna mtu, asiyemkumbuka na kumuenzi Karume kwa kile alichokifanya, hasa kufanya mageuzi ya karafuu, apimwe akili.

"Kiongozi wetu huyu mpendwa, alikuwa mstari wa mbele ili kuhakikisha karafuu inakuwa almasi kama si dhahabu kwa wananchi wote,"anasema, anapozungumza na gazeti hili, kuelezea anavyomkumbuka Karume.

Abubakar Mohamed Ali, ambaye ndie Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuia za Wazalishaji wa Karafuu Zanzibar, (ZAPCO) anasema, kama kuna jambo ambalo wao wanalikumbuka kwa Karume, ni kuamua kuuwekea mazingira imara mti wa karafuu.

"Kama viongozi wote waliopita baada ya mwaka 1964, wangefuata nyendo za rais wa kwanza wa Zanzibar sheikh Abeid Amani Karume, karafuu zingekuwa nyingi kuliko watu wenyewe."

"Kwanza yeye mwenyewe alikuwa mkali kwa kudhibiti magendo. Namkumbuka mtu mmoja wa Tibirizi Chakechake, alifungwa miaka 10 na kupanda mikarafuu 100," anasema akikumbuka Karume alivyokuwa mkali kwa karafuu.

Jemedari huyo alikuwa akibuni kila njia ya kuhakikisha uchumi kupitia zao la karafuu unakwenda moja kwa moja kwa wananchi na anakumbukwa kwa kuanzisha katazo la kwanza mwaka 1970.

Anasema katazo hilo (decree, 1970), liligusa mambo kadhaa ndani yake ikiwa ni pamoja na marufuku ya kuukata mti wa karafuu, kuharibu karafuu na hata suala la kuzisafirisha kimagendo.

Lakini, kutokana na kuweka mazingira imara ya karafuu, hata baada ya kifo chake, sheria nyingine ziliendelea kutungwa hasa ndani ya mwaka 1985 kiwamo sheria ya karafuu namba 11.

Ingawa hata rais wa sasa wa Zanzibar, Dk Ali Mohamed Shein, naye mwaka 2014, alisaini sheria hiyo na mwaka 2016 ilifanyiwa mapitio na kuongezwa baadhi ya vifungu kikiwamo cha kutaja nini kinachoitwa magendo.

Mapinduzi yaliyoitwa ya kiuchumi kwa Wazanzibari, yaliyofanywa na Jemedari wa Zanzibar, sheikh Abeid Amani Karume, kwa wakati huo yaliungwa mkono na nchi za Kikominist za China, Ujerumani Mashariki na Umoja wa Kisovyeti.

Historia inaonyesha kuwa, karafuu iliingia visiwani hapa ikitokea mji wa Molucca ulioko Indonesia kwenye karne ya 20. Kuna wanaosema ilifika kisiwani hapa kwa njia saba, ingawa wengine hueleza ililetwa na Sultan, kama zawadi na baada ya kuona Zanzibar inastawi, ilipelekwa Kizimbani Chuo cha Kilimo Kaskazini Unguja, ili kuoteshwa.

Hata kabla ya mwaka 1964, wakulima wa karafuu, kutokana na kuona umuhimu wa zao hilo ,walianzisha muungano wa wakulima wa karafuu uliojulikana kama CGA kwenye mwaka 1956.

- Videos
- Jarida la Khilafah
- Majarida Mengine
- Vitabu
- Vitabu Rasmi
- Vitabu vya Ziada
- Ujumbe wa Wiki

Ni takriban miaka 48, japo Wazanzibari wamempoteza kiongozi wao, wanaendelea kumkumbuka shujaa wao mahiri na kiongozi wa mapinduzi hayati Karume, kwa kuhakikisha wanasimamia karafuu na kudumu katika kilimo chake hadi leo likiwa na thamani yake kama vile lilivyoachwa na Karume.

**MLINZI KARAFUU**

Huyu ni kiongozi aliyetumia muda wa uhai wake, kufanya kazi na kuwatumikia Wazanzibari, kabla ya kuuawa kwake kikatili Aprili 7, 1972, na wapinga maendeleo waliokuwa na ndoto ya kurudi tena kwa utawala wa kisultani uliopinduliwa kupitia Mapinduzi ya Zanzibar, Januari 12, 1964.

Kama inavyofahamika mti upo juu ya ardhi, yaani karafuu inastawi, ndivyo hivyo Karume, ilipofika Machi 11, 1964 kazi ya kugawa ardhi kwa ajili ya kilimo, ambayo awali ilikuwa ikishikiliwa na Waarabu, ilianza rasmi huko kijiji cha Dole Wilaya ya Kati mkoani Unguja.

Mapema Machi 11, mwaka 1964, kazi ya kuigawa ardhi kwa wazalendo kwa kuwapa kila mmoja eka tatu za ardhi ilifanyika, hadi leo wapo waliyoyaendeleza mashamba hayo ya karafuu hadi sasa hawajatetereka na wanaendelea kuzalisha karafuu.

Asha Mbaraka Khamis (70), wa eneo la Mkoani, anasema ukali wa kuliimarisha zao la karafuu, aliokuwa nao hayati Karume hajapata kumuona kiongozi mwingine hadi leo, akiwa nao katika kulisimamia.

Anasema kwa wakati huo, ilikuwa kazi ya kuangalia magendo ya karafu na ukataji wa mti huo, ilipewa kikosi cha mgambo na kwamba hakuna aliyethubutu kufanya kosa kwenye zao hilo.

"Mimi nakumbuka tumeshaitwa mara tatu kushuhudia mtu akipigwa viboko . Akilala chini kwa kosa la kutoshiriki kwenye upandaji wa mikarafuu," anasema mkulima huyo.

Mwanamjaka Himid Seif (65), mkazi wa Mtambile, anasema huwezi kutaja historia ya karafuu kwa Zanzibar na hasa baada ya mwaka 1964, bila ya kumtaja Karume.

"....Aaa kwa wakati huo ilikuwa kwanza hakuna kujengea mti ya mkarafuu ni miti ya msituni au baharini tu, na ukikamatwa hakuna rushwa ni viboko na unapanda mengine," anasimulia Mwanamjaka.

Anapoulizwa iwapo anakumbuka kisa chochote cha karafuu wakati wa uhai wa Karume, anasema aliitwa na balozi au 'brachi', na kuelezwa kwamba kuna tawi la zao hilo limekatika na akaliondoe haraka barabarani.

"Hata kama tawi la mti wa karafuu lililokatika, ilikuwa huruhusiwi kulitumia mpaka likauke, sio leo tena watu wanaifanya kama leso," anasema Mwanamjaka.

**MAKUSANYO YA MAPATO**

Mwanamjaka anasema sasa ni miaka 48, tokea kiongozi huyo auawe hapo mwaka 1972, zao hili limekuwa likipitia katika changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja kupungua kwa idadi ya miti ya mikarafuu na pia kupandwa mipya lakini mapato yanaongezeka.

Kukua kwa makusanyo ya mapato na kufikia Sh. bilioni 548. 571 kwa mwaka 2017, ikilinganishwa na Sh.bilioni 487.474 mwaka 2016 hapa Zanzibar, pia limechangiwa na kasi aliyorithi Dk. Shein ya kuliimarisha zao la karafuu.

Aidha, jumla ya tani milioni 33. 549 za karafuu kavu zenye thamani ya Sh. bilioni 448. 684 zimenunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka kwa wakulima kwa kipindi cha mwaka 2010 hadi 2019.

Huku kwa miaka tisa mfululizo serikali hii ilioasisiwa na Rais wa kwanza Abeid Amani Karume, na leo tukiwa tunafuta machozi ya miaka 48 tokea alipokatishwa uhai wake inamlipa mkulima wa zao hilo kiwango cha asilimia 80 ya bei ya karafuu kwenye soko la dunia.

Kwa hiyo kwa bei ya ndani kwa sasa kilo ni Sh. 14,000 kwa kilo moja ya karafuu kavu za daraja la kwanza , sambamba na uwepo wa bima maalum kwa wakulima wanapopata ajali za kuanguka au kupoteza maisha wakati wanapoliokoa zao hilo la taifa.

Azma na shabaha ya rais wa kwanza wa Zanzibar ambaeye leo hayupo duniani kwenye mgongo wa ardhi, lakini kwa vile wosia wake, ushauri na juhudi zake zinaendelea kufanyiwa kazi, ndiyo maana hata miche ya karafuu inatolewa bure.

Tayari miche ya mikarafuu 2, 617, 994 imeshaoteshwa kuanzia mwaka 2011 hadi mwaka 2017 na baadhi yao umeshaanza kuzaa, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Kilimo.

Kwa hiyo ni sahihi kusema kuwa, hayati Karume aliweka misingi na njia endelevu za kuliimarisha zao la kafaruu na mti wake na hapo sasa kumfanya rais wa awamu ya saba kufanya vyema katika kuliendeleza zao hilo.

Kwa ile ile misingi ya hayati Karume ya kuliimarisha zao la karafuu, kuanzia mwaka 1964 baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, na leo mwaka 2018, bajeti kuu ya serikali nayo imepata maendeleo.

Kwa mujibu wa hotuba ya Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, aliyoitoa kwenye maadhimisho ya miaka 54 ya Mapinduzi, alikiri kuwa, kwa mwaka 2017/2018 utegemezi wa bajeti kuu umepungua.

Kwa mwaka 2017/2018 umefikia asilimia 7.3 ikilinganishwa asilimia 30.2 ilikuwa kipindi cha mwaka 2010/2011, ambapo karafuu ndiyo kichochecho kikubwa cha kupunguza utegemezi wa bajeti.

Leo siku ya maadhimisho ya miaka 48, misingi ya kuliimarisha zao la karafuu iliyofanywa na hayati Karume, sasa hata uvunaji wa zao hilo, umekuwa ukiongezeka mara dufu.

Anasema hadi kufikia Januari 5 mwaka 2017, tani 8,182.04 za karafuu kavu, zenye thamani ya Sh. bilioni 114.17 baada ya serikali kununua kwa wakulima, nayo imeshauza tani 5,881 zenye thamani ya Sh. bilioni 103.49.

Mitandao inaeleza kuwa, tathmini iliyofanywa ya Sensa ya Miti (Woody Biomass Survey 2013), imeonyesha kuwa, Zanzibar ina idadi ya karafuu 4,131,783, Unguja karafuu 277,196 na Pemba 3,854,587.

Ingawa tathmini ya mwaka 1997 ilionyesha idadi ya karafuu 790,400 kwa Unguja ni karafuu 5,042,700 kwa upande wa Pemba, ikifanya idadi ya karafuu yote kuwa ni 5,833,100.



Kila mwaka viongozi na Watanzania hukusanyika kumwombea dua na kufanya kisomo kwa ajili ya jemadari wa Mapinduzi ya Zanzibar, hayati Karume. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> ....Aaa kwa wakati huo ilikuwa kwanza hakuna kujengea mti ya mkarafuu ni miti ya msituni au baharini tu, na ukikamatwa hakuna rushwa ni viboko na unapanda mengine.



Rais Shein akiungana na wakulima kuchuma karafuu.

> Hata kama tawi la mti wa karafuu lililokatika, ilikuwa huruhusiwi kulitumia mpaka likauke, sio leo tena watu wanaifanya kama leso.

## UN yalia ubaguzi watoa huduma utakavyomaliza weusi na corona



Mkimbizi wa ndani anayerejea nyumbani kwa hiari huko Bentiu Sudan Kusini, akipimwa corona: **PICHA: UN NEWS**

KIKOSI kazi cha waatalamu wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu watu wenye asili ya Afrika, kimetaka kuwapo na uwiano na usawa wa makundi mbalimbali ya binadamu wakati wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa virusi vya COVID-19, la sivyo utoaji wa huduma kwa misingi ya rangi unaweza kusababisha vifo zaidi.

Wito huo, umo kwenye taarifa ya wataalamu hao wanaotetea haki za watu walio na asili ya Afrika, katika taarifa iliyotolewa jana jijini Geneva, Uswisi ikisema kuwa ubaguzi wa kimfumo katika utoaji huduma unaleta matokeo ya kibaguzi na vifo zaidi na idadi ya wagonjwa miongoni mwa watu wenye asili ya Afrika.

Mwenyekiti wa kikosi kazi hicho, Ahmed Reid anasema, "licha ya hatua mujarabu zilizochukuliwa, serikali bado hazijatambua athari mahsusi za kiafya zinazokabili watu wenye asili ya Afrika au jinsi ubaguzi wa rangi na upendeleo kwa misingi ya rangi vinaweza kuchochea sera hiyo."

Wataalamu hao wa haki za binadamu wanasisitiza kuwa tatizo jingine ni ukosefu wa uwakilishi katika ngazi ya juu wakisema kuwa, "hili linazuia kusambaza utaalamu na ulinzi kwa mahitaji ya watu wenye asili ya Afrika wakati wa utekelezaji wa hatua na utoaji dawa dhidi ya COVID-19."

Wataalamu hao wanasisitiza kuwa serikali zinapaswa kuchunguza jinsi gani upendeleo wa aina hiyo bila mwongozo wowote unavyoweza kufanya janga la COVID- 19 kuwa kubwa zaidi kwa baadhi ya watu wa rangi fulani wakiongeza kuwa, "tayari ambako kwenye data zilizonyumbuliwa, tofauti za huduma kwa misingi ya rangi ya watu ni dhahiri."

Mathalani, wanasema kuwa, "hatua zinazoonekana usoni kuwa haziegemei upande wowote, zinaweza kuruhusu au kuchochea ubaguzi wa rangi. Kwa mantiki kwamba hadi sasa hakuna hatua za kulinda au kujikita katika utoaji huduma za afya kwa kuzingatia hatari wanazokabiliwa nazo watu wa makundi fulani ikiwamo Waafrika na wenye ulemavu."

Wataalamu hao wanasisitiza kuwa mazingira ambayo watu wa asili ya Afrika wanafanya kazi au kwenye jela wanakofungwa, kunahatarisha zaidi maisha yao katika kuambukizwa virusi vya Corona.

Ni kwa mantiki hiyo, wataalamu hao wanasisitiza kuwa, suala la wafanyakazi wa afya na wahudumu wanaotoa huduma katika ngazi za chini kwenye jamii waliozidiwa uwezo wanapaswa kupata mwongozo zaidi ikiwamo kuwasilisha data zilizonyambuliwa ili kuhakikisha kuwa kuna huduma zenye uwiano.

Katika taarifa hiyo Reid anaongeza kuwa "serikali zinazotumia janga la COVID-19 kusitisha au kupunguza haki za kibinadamu zinazotolewa kwa misingi ya upendeleo chanya zinakwamisha watu wenye asili ya Afrika na hatua hizo zitadumu zaidi hata baada ya janga la Corona."

Hata hivyo, kikundi kazi hicho kimekaribisha hatua za COVID-19 lakini kimezisihi serikali kutambua udharura wa haki za binadamu na kuhakikisha huduma za elimu, afya, intaneti zinapatikana kwa watu wote na kwa nyakati zote. **UN NEWS**

URITHI WA KARUME

# Licha ya kuondoka fikra zake zinawaongoza Wazanzibari



Moja ya mikakati ya Karume ilikuwa kujenga nyumba na kuboresha makazi ya wananchi kote Zanzibar na Pemba. **PICHA: MTANDAO**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IMETIMIA miaka 48 sasa tangu muasisi wa taifa la Zanzibar Abeid Amani Karume, kuuawa kikatili na wapinga maendeleo mnamo Aprili 7, 1972.

Wanaopinga maendeleo walimshambulia Karume na kumua akiwa kwenye makao makuu ya chama kilicholeta uhuru cha ASP ofisi ya Kisiwandui.

Tamko la Baraza la Mapinduzi mwaka 1972 liliweka bayana kwamba "hayati Abeid Amani Karume, ameuawa na kuzikwa lakini kilichokufa ni kiwiliwili chake tu . Mawazo busara na mambo yote mema hasa ya kumuenzi Mzanzibari na kumletea maisha bora yataendelea kulindwa na kuenziwa kwa faida ya wananchi wote wa vizazi vilivyokuwepo na vijavyo.

Zanzibar itaendesha kisomo cha kumkumbuka Mzee Karume na kwamba hakitakuwa na watu wengi kama ilivyozoeleka katika miaka iliyopita kutokana na ugonjwa corona.

Licha ya Karume kuondoka taifa limeendelea kushuhudia awamu mbali mbali za marais wakiongoza Zanzibar wakiendelea kufuata nyayo na kuyalinda yale mambo yote ya msingi yaliyoanzishwa na kiongozi huyo.

Zanzibar inatajwa kuwa miongoni mwa nchi za mwanzo katika Bara la Afrika kutekeleza kwa vitendo maazimio na matamko ya jumuiya za kimataifa yanayohusu haki za binadamu na utawala bora mara baada ya Mapinduzi ya Januari 12 mwaka 1964

Hata, katika tamko lake la mwanzo mara baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 1964, lililotangazwa na Jemedari Karume aliuhakikishia umma kuwa Zanzibar itaongozwa kwa misingi ya kulinda utu wa binadamu na kuwajali wazee pamoja na watoto yatima.

> ...Hayati Karume mara baada ya mapinduzi alianzisha mradi wa ujenzi nyumba za makaazi katika maeneo mbali mbali kwa ajili ya kuishi wananchi wake.

Hatua, hiyo ilikwenda sambamba na kuundwa kwa wizara inayoshughulikia haki za wananchi pamoja na kujenga nyumba za kuhifadhi wazee na wasiojiweza ziliopo Sebuleni mjini Unguja.

Ndivyo anavyosema Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, akitaja Mapinduzi ya Januari 12 mwaka 1964, yaliyoongozwa na hayati Abeid Amani Karume, kuwa ndiyo yanayoweka sawa utekelezaji wa haki za binadamu ambapo makundi yote ya vijana,wazee na watoto yalitambuliwa rasmi na kupewa huduma na serikali.

Anasema wizara hiyo na taasisi wadau zinaendelea kutekeleza mambo yote ya msingi yaliyoasisiwa na Karume kwa vitendo.

Anaeleza kuwa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (Zaeca) kwa kiasi kikubwa imeweka misingi ya kupambana na ufisadi kwa viongozi waliokabidhiwa majukumu ikiwamo serikali na taasisi za umma.

Anaeleza kuwa rushwa ni adui wa haki na sehemu ambayo rushwa imetawala, watu wa kawaida na kusababisha wanyonge kunyimwa nafasi ya kupata mambo ya msingi wanayostahiki zikiwamo huduma za lazima.

**KUBANA MAFISADI**

"Tumepiga hatua kubwa katika kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi katika sehemu za utoaji wa huduma... tunawataka watu kutoa taarifa za rushwa ili tuwachukulie hatua za kisheria','anasema Suleiman.

Anakumbusha kuwa hayati Karume alichukizwa na vitendo vya matajiri kuwakopesha fedha wananchi wanyonge na kuwatoza riba kubwa na hivyo kuwaweka katika maisha magumu.

"Mara baada ya Mapinduzi ya Januari 12, Karume alipiga marufuku matajiri kuwatoza fedha wananchi wanyonge katika mfumo wa riba pamoja na rehani,"anasema Suleiman.

Waziri huyu anakumbusha kuwa mara moja baada ya mapinduzi Karume alianzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kumteua Mohamed Aboud, kuiongoza na baadaye, kiongozi huyo alikuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Tanzania Bara, akiwa ndiye mzalendo wa kwanza kufanya kazi hiyo baada ya kuondoka kwa mzungu.

Aidha, Suleiman anasema kwa upande wa watumishi wa umma,Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haipo nyuma kutekeleza yale yote yaliyoasisiwa na rais wa kwanza katika kujali watumishi wake.

Suleiman anasema Karume alikuwa akisema siku zote kwamba tumefanya mapinduzi kwa ajili ya wananchi walio wengi kushika hatamu ya kuongoza taifa lao.

Anasema wizara yake imekuwa ikizingatia maslahi ya watumishi wake yakiwamo kuongeza mishahara mara kwa mara kadri hali ya mapato inavyoimarika na kuweka mazingira mazuri na kuwawekea fedha zao katika mazingira bora wakati watakapostaafu.

"Karume siku zote alikuwa akizungumza suala la hatma ya wafanyakazi na kuhakikisha wanakuwa na akiba yao wakati watakapostaafu... Ndiyo maana tumeanzisha mfuko wa hifadhi ya jamii ZSSF,"anakumbusha.

**UUMINI WA KARUME**

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akilifungua kongamano la utawala bora,anajinadi kuwa ni muumini mkubwa wa dhana ya utawala bora pamoja na misingi yake muhimu ikiwemo iliyoasisiwa na viongozi wakuu wa nchi hasa Rais wa Kwanza wa Zanzibar hayati Karume.

Dokta Shein anasema katika kipindi chake cha uongozi wa miaka tisa amefanya kazi kubwa kuhakikisha mambo ya msingi yaliyoasisiwa na hayati Karume ambayo ndiyo yaliyopelekea kufanyika kwa mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 yanadumishwa na kuenziwa.

Anataja elimu bure, matibabu bure pamoja na kuwapatia hifadhi bora wazee na makazi bora wananchi wa kawaida kuwa ni miongoni mwa mambo muhimu aliyoyasimamia mwasisi huyo.

Rais anasema katika sekta ya elimu hivi sasa michango yote iliyokuwa ikitolewa na wazazi kwa ajili ya kuchangia huduma hiyo imefutwa na ni marufuku mzazi kudaiwa fedha kwa ajili ya gharama za elimu.

"Hayati Karume anatangaza elimu bure Septemba mwaka 1964 na mimi nimeamua kulinda na kuheshimu uamuzi huo na sasa nimefuta michango yote na hakuna mzazi atakayedaiwa kutoa fedha kwa ajili ya gharama za elimu,"anasema Dk. Shein.

Aidha, anasema serikali imetenga fedha Shilingi bilioni 90 kwa ajili ya kujenga nyumba bora za kisasa makazi ya wananchi Kwahani ikiwa ni moja ya azma ya hayati Karume kuona Wazanzibari wanaishi kwenye nyumba bora.

"Tumeanzisha mradi wa ujenzi wa makazi nyumba za ghorofa huko Kwahani mjini Unguja...Hayati Karume mara baada ya mapinduzi alianzisha mradi wa ujenzi nyumba za makaazi katika maeneo mbali mbali kwa ajili ya kuishi wananchi wake," anakumbusha.

**SMZ INAVYOMUENZI**

Mifano mingine ya kuendelea kumuenzi hayati Karume yanayotekelezwa na Rais Shein katika kipindi cha uongozi wake ni kuanzisha pensheni ya jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya wazee Zanzibar (JUWAZA) Masururu Saad Ferouz, anasema kinachofanywa na Dk.Shein katika kipindi cha uongozi wake ni kutekeleza yale yote yaliyofanywa na hayati Karume mfano kuwahifadhi na kuwapatia matunzo bora wazee.

Ferouz anaipongeza serikali kwa kuanzisha pensheni jamii kwa wazee waliofikisha umri wa miaka 70 ambayo inatolewa bila ya ubaguzi huku zaidi ya wazee 28,022 wakifaidika na malipo hayo bila ya kujali kama mtu alikuwa mtumishi wa serikalini au lah.

"Sisi wazee tunampongeza kwa dhati Rais Shein kwa kuanzisha pensheni jamii na kuwapatia wazee Shilingi 20,000 kila mwezi bila ya ubaguzi. Hatua hiyo ni sawa na kufuata nyayo za Rais wa kwanza wa Zanzibar hayati Abeid Amani Karume za kuyalinda Mapinduzi na kuwaenzi wazee,"anaongeza Forouz.

# Sasa ni rasmi Prof. Tibaijuka kuliachia jimbo Muleba Kusini

**Na Sabato Kasika**

NI dhahiri kwamba, Mbunge wa sasa wa Muleba Kusini mkoani Kagera, kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Profesa Anna Tibaijuka, amedhamiria kutogombea na kuachana ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Ilikuwa ni Novemba mwaka 2017 alipotangaza kwa mara ya kwanza uamuzi wake huo lakini baadhi ya watu wakaanza kusema kwamba hiyo ndiyo kawaida ya wanasiasa, wakiamini kwamba angebadili msimamo huo.

Kuendelea kusisitiza tena kuwa hatashiriki kinyang'anyiro hicho safari ikiwa imesalia miezi michache kabla ya kuanza mchakato wa uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu, kunadhihirisha kuwa ameazimia kung'atuka.

Aliweka bayana uamuzi huo mkoani Kagera, wakati akizungumzia miaka miwili ya serikali ya Rais John Magufuli, na ameendelea nayo mara kadhaa licha ya kubezwa na baadhi ya wadau wa siasa.

Katika kuonyesha msisitizo kuhusu uamuzi wake huo, wiki iliyopita, mbunge huyo aliwaaga rasmi wabunge wenzake bungeni na kusema hatagombea tena ubunge, hali ambayo inaonyesha kuwa hakuubadili msimamo wake huo.

Wakati akitangaza uamuzi huo kwa mara ya kwanza mwaka 2017, wapo baadhi ya watu walioandika kwenye mitandao ya kijamii wakibeza, kwa madai kwamba wanasiasa hawaaminiki.

Katika mawazo yao waliamini kwamba angesema hivyo lakini baadaye akabadili msimamo, lakini Prof. Tibaijuka haikuwa hivyo na badala yake ameendelea kusimamia uamuzi wake hadi kufikia kuaga rasmi.

Hatua yake ya kuliaga bunge, imeonyesha ni jinsi gani mbunge huyo hakuwa 'anabipu' na wala hakuwa na utani na siyo mwanasiasa asiyekuwa na msimamo bali anajua kusimamia kile alichoamua kukifanya.

Ikumbukwe ni Novemba mwishoni mwaka 2017 alipotangaza kutogombea ubunge, na ilidhani kwamba huenda ungefika wakati aamue kujitosa tena, lakini hilo halikutokea kwake.

Ijumaa ya wiki iliyopita, mbunge huyo alikaririwa na vyombo vya habari akiaga rasmi bungeni akisema, hatagombea ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

Katika kuaga kwake, mbunge huyo aligusia pia sakata la Escrow na kukabidhi serikalini hoja yake binafsi aliyodai kuwa aliipigania kuingia bungeni kwa miaka 10 bila mafanikio.

"Kwa kupitia ofisi yako nakushukuru kuwa umemwandikia mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Jenista Mhagama, kumkabidhi hoja yangu binafsi, ambayo nimehangaika nayo tangu Bunge la 10," Prof. Tibaijuka anakaririwa akisema.



Mbunge wa Muleba Kusini mkoani Kagera, Prof. Anna Tibaijuka, ambaye amesema hatagombea tena ubunge mwaka huu. **PICHA MTANDAO**

> Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema tung'atuke... na mimi nang'atuka ili maarifa yangu yaweze kutumika kushauri. Jamani tufanye hivi ili tuende mbele.

Anaongeza kwamba, rekodi ya kumbukumbu rasmi za taarifa za bunge ionyeshe kuwa amemkabidhi Jenista hoja yake binafsi na kusema kwamba ilikuwa inazungumza baada ya kukumbwa na tatizo la Escrow na kujikuta anahukumiwa bila kuruhusiwa kusimama kujitetea.

"Nikaona kuwa tuna upungufu mkubwa wa mfumo wetu, nikaja na muswada binafsi bunge la Makinda (Spika wa Bunge la 10 Anne Makinda) muda haukupatikana, lakini nashukuru bunge lako muda haukupatikana lakini angalau umepiga hatua na kukabidhi serikalini," anasema.

Katika sakata la Escrow Profesa Tibaijuka aliyekuwa Waziri wa Ardhi alituhumiwa kupokea Sh.bilioni 1.6 kutoka kwa mmiliki wa kampuni ya VIP Engineering ambaye pia alikuwa mwanahisa wa mradi wa kufua umeme wa mafuta uliokuwa unazalishwa na kampuni ya IPTL.

Waziri huyo wa zamani alidaiwa kuzipokea kutoka kwa mtuhumiwa wa uhujumu uchumi, James Rugemalira, bilioni 1.6, akisema alipewa kwa ajili ya kujengea bweni la Shule ya Barbro Johanson

"Nawashukuru sana wananchi wa Muleba Kusini kwa kunipa nafasi ya kuwa kwenye jimbo hili kwa miaka 10, nimejifunza mengi, ambayo yatanifanya niende kuandika vitabu,"anasema

### KWA NINI HAGOMBEI?

Tangu mwaka 2017, mbunge huyo amekuwa akitaja sababu za kuachana ubunge kuwa ni kupumzika na kuwapisha vijana wenye mawazo mapya ili nao wapate nafasi ya kuongoza taifa.

Mbunge huyo anasema, miongoni mwa vitu alivyojifunza kutoka kwa Mwalimu Julius Nyerere ni kung'atuka, hivyo uamuzi huo usichukuliwe kama anaogopa kushindwa, kwa vile hamuhofii mtu yeyote.

"Ninatambua kwamba, katika uongozi kuna kung'atuka, hivyo sisi ni watu wazima, kizazi chetu tumeshamaliza kazi. Tumeshastaafu na mimi nikimaliza ubunge muhula huu nastaafu," anasema.

Anaeleza kuwa , anapenda awape nafasi vijana, lakini pia anafafanua kuwa kuzeeka hakumaanishi kwamba maarifa yake yameondoka, bali suala la msingi ni kuwapa nafasi vijana washike nchi.

"Bunge ni la uwakilishi lenye hoja zinazolinda masilahi mapana ya umma, na mimi ninawakilisha wananchi na ninaamini kwamba Muleba inaweza kupata mwakilishi mzuri badala yangu," anasema.

Lakini pia anasisitiza kuwa hatua yake ya kustaafu ni uamuzi wa kawaida wa kupeana vijiti na kwamba kwa miaka 10 ya ubunge amejifunza na ameelewa matatizo ya wananchi wa jimbo lake na kuyashughulikia.

"Wakati ule nilipotoka Umoja wa Mataifa, nilikuja na nia moja ya kujifunza kwamba taifa letu lina tatizo gani, nimefanya sehemu yangu na sasa ni vyema nikang'atuka kupisha wengine," anasema.

Anasema, siyo vibaya wabunge wakongwe kama yeye wa kizazi cha Mwalimu Nyerere wakapumzika na kuwapisha vijana wenye mawazo mapya na kubaki kama washauri ili wasaidie taifa kusonga mbele.

"Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema tung'atuke...na mimi nang'atuka ili maarifa yangu yaweze kutumika kushauri. Jamani tufanye hivi ili tuende mbele," anasema.

Profesa Tibaijuka anaamini kwamba siasa haina umri, lakini pia kwenye nafasi ya ubunge, bado kuna haja ya kuwapo damu changa hasa kwa kuzingatia dhana ya kung'atuka iliyoasisiwa na Baba wa Taifa.



Baadhi ya watu weusi nchini Marekani katika mikutano. **PICHA: MTANDAO.**

# COVID-19 ni kitisho zaidi kwa weusi nchini Marekani

WAKATI Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amelazwa katika chumba cha kuhudumia wagonjwa wanaohitaji huduma na uangalizi maalumu (ICU), jijini London, watu weusi wako kwenye hatihati za kupoteza maisha zaidi.

Hatua hiyo ya kulazwa ICU, inakuja baada ya hali ya Johnson kiafya kuwa mbaya kwa siku 10 zaidi akiugua COVID 19, hata hivyo, zile tambo kuwa Waafrika hawafi kwa corona zinaanza kukosa mashiko baada ya maelfu kupoteza maisha nchini Marekani.

Waafrika au watu weusi wengi wanadaiwa kufariki kutokana na COVID 19 nchini Marekani jambo linalopingana na madai kuwa eti kirusi cha corona hakiwadhuru watu weusi.

Taarifa za Waziri Mkuu kulazwa ICU ni kwa mujibu wa msemaji katika makazi ya Waziri Mkuu, akisema Johnson amemwambia Waziri wa Mambo ya Nje Dominic Raab, kuchukua usukani "pale ambapo kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo", msemaji anaongeza.

Waziri Mkuu Johnson mwenye miaka 55, alilazwa katika hospitali ya St Thomas mjini London, wakati hali yake ya kiafya ilipokuwa haina ahueni huku homa na kukohoa kukiongezeka zaidi siku ya Jumapili.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya ushauri kutoka kwa timu yake ya matibabu na anaendelea kupata huduma stahiki.

Taarifa zaidi zinaarifu kuwa : "Tangu Jumapili jioni, Waziri huyo Mkuu amekuwa chini ya madaktari wa hospitali ya St Thomas mjini London, baada ya kuonyesha dalili mbaya za virusi vya Corona.

> Takribani asilimia 40 ya vifo vitokanavyo na virusi vya corona katika jimbo la Louisiana katika jiji la New Orleans ambako watu weusi ni wengi zaidi.

### WEUSI KUFARIKI ZAIDI

Wakati huohuo, takwimu kutoka maofisa wa afya mjini Chicago zinaonyesha athari kubwa ya virusi vya corona kwa Wamarekani weusi, inatisha.

Raia weusi wa mji wa Chicago ni nusu ya vifo vyote vya ugonjwa wa COVID 19 katika mji huo na zaidi ya asilimia 70 ya vifo vyote , licha ya kwamba idadi yao ni asilimia 30 ya watu wote katika jiji hilo.

Miji mingine yenye idadi kubwa ya watu weusi ikiwamo Detroit, Milwaukee , New Orleans na New York pia imetajwa kuwa maeneo yaliyo hatarini.

Marekani imerekodi wagonjwa 370,000 wa virusi hivyo na takriban vifo 11,000. Wakati hayo yakitokea nchini humo, duniani kote kumekuwa na vifo 75,000 na maambukizi yamefikia milioni 1.3 kwa jumla.

Swali linaloibuka linasema je, takwimu hizo za Chicago zinaonyesha nini? Hadi kufikia Aprili 5, wagonjwa 1,824 wa maradhi ya corona kati ya 4,680 vilivyothibitishwa vilihusisha wakazi weusi, walisema maofisa wa mji huo Jumatatu wiki hii.

Hiyo ni tofauti na wagonjwa 847 weupe, 478 vya jamii ya Wahispanic na 126 vya Waasia wa Chicago. Chicago iliripoti vifo 78 Jumapili iliyopita huku asilimia 72 ya vifo hivyo vikihusisha watu weusi.

Utofauti huo unaonekana katika jimbo zima, ambapo watu weusi ni asilimia 41 ya vifo vilivyotokana na Covid-19, licha ya kuwa ni asilimia 14 ya watu wote wa jimbo la Illinois.

Kamishna wa Afya ya Umma wa Jiji la Chicago Dk. Allison Arwady, anawaambia wanahabari kuwa watu weusi wa jiji hilo tayari wana wastani wa maisha mafupi kwa miaka 8.8 kulinganisha na Wazungu.

Meya Lori Lightfoot, akizungumzia suala hilo alisema kuwa virusi vya corona "vitateketeza Chicago ya watu weusi".

Anaeleza kuwa, wakaguzi wa jiji hilo watatumwa madukani kuhakikisha kila mtu anatekeleza maelekezo ya kujitenga kwa umbali unaoshauriwa kitaalamu na wengine.

Meya Lightfoot pia ameelezea juu ya uwezekano wa kuwekwa marufuku ya kutoka nje kwa baadhi ya saa katika maeneo ambayo watu hukusanyika kwenye maduka ya pombe, linaripoti gazeti la Chicago Sun-Times.

### HALI NCHI NZIMA

Japo virusi vya corona vimepewa jina la "msawazo mkuu ", takwimu zinaonyesha kuwa madhara ya maambukizi yanaweza kutofautiana kwa sehemu.

Katika jimbo la Michigan, Wamarekani Weusi ni asilimia 14 ya watu wote, lakini wao ni asilimia 33 ya wagonjwa wa corona na asilimia 41 ya vifo kutokana na ugonjwa huo, zinaonyesha takwimu kutoka idara ya afya ya jimbo hilo kufikia jana Jumatatu.

Wazungu katika jimbo hilo ni asilimia 23 ya wagonjwa na vifo vyao ni asilimia 28, kwa mujibu wa takwimu hizo.

Jiji la Detroit, katika jimbo la Michigan, lina wakazi weusi takribani asilimia 80, na jiji hilo pekee pamoja na viunga vya karibu yake vina asilimia 80 ya wagonjwa wote wa corona katika jimbo hilo.

Utofauti kama huo pia unaonekana jiji la Milwaukee, jimboni Wisconsin, moja ya maeneo yaliyoathirika zaidi na ubaguzi wa rangi nchini Marekani.

Watu weusi kufikia Ijumaa wiki iliyopita wanafikia nusu ya wagonjwa 1,000 na asilimia 81 ya vifo, japo watu weusi ni asilimia 26 tu ya wakazi wa jiji hilo.

Takribani asilimia 40 ya vifo vitokanavyo na virusi vya corona katika jimbo la Louisiana katika jiji la New Orleans ambako watu weusi ni wengi zaidi.

Maofisa wa afya hapo awali walieleza kuwa wakazi wengi wa New Orleans wanakabiliwa na matatizo ya unene wa kupitiliza, kisukari na presha ya kupanda kwa kiwango cha juu zaidi nchini Marekani hali inayowafanya kuwa rahisi kudhurika zaidi na COVID-19.

### WEUSI WAGONJWA

Meya Lightfoot anasema kisukari, magonjwa ya moyo na maradhi ya mfumo wa hewa yapo "kwa kiwango kikubwa" kwenye jamii za weusi.

Wakati Dk. Arwady anawaambia waandishi kuwa hata kama kila mtu katika jiji hilo angekuwa na uwezekano wa kumuona daktari, "bado tungeendelea kuona utofauti mkubwa kutokana na upatikanaji haba wa chakula bora na mitaa ya kutembea ".

Dokta Cameron Webb, ambaye ni tabibu mweusi anayewania ubunge katika jimbo la Virginia, ameiambia BBC kuwa tofauti za rangi na kiuchumi zinaonyeshwa wazi na janga hili.

"Janga la corona linaonyesha nyufa za jamii yetu," anaeleza.

Alderman Jason Ervin, ambaye ni mwenyekiti wa umoja wa wawakilishi weusi katika baraza la jiji la Chicago analiambia gazeti la Chicago Tribune kuwa "Wingi wa watu wasiofuata maagizo ya kujitenga nyumbani katika baadhi ya sehemu za jiji hilo" inawezekana pia ikawa inachangia takwimu hizo. **BBC**



# Mbaroni tuhuma za udanganyifu

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WATU wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kujipatia mali mbalimbali zikiwamo televisheni zenye thamani ya Sh. milioni 19.68 kwa njia ya udanganyifu wakitumia hundi hewa kununua vitu madukani.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Enock Kyaruzi (41), Satala Makoba (50) na Michael Chuwa (65) wakazi wa jijini Dar es Salaam pamoja na Dickson Warioba (34), mkazi wa Mlowo mkoani Songwe.

Alisema watuhumiwa walikamatwa Aprili 4, mwaka huu katika maeneo tofauti ya Jiji la Dar es salaam wakiwa na mali hizo kufuatia msako mkali uliofanyika baada ya kupata taarifa zao.

Alisema watuhumiwa walijipatia mali hizo katika duka la mfanyabiashara wa vifaa vya muziki aitwaye, Michael Mdoe, lililopo katika soko la Sido jijini Mbeya.

Kamanda Matei alizitaja mali ambazo watuhumiwa hao walijipatia ni televisheni 24 za kampuni tofauti tofauti na zenye ukubwa wa aina mbalimbali.

"Tuliwakuta na gari aina ya Toyota Brevis yenye namba za usajili T.681 DGV ambayo ndiyo waliitumia kusafirisha mali hizo kutoka hapa Mbeya mpaka Dar es Salaam," alisema Kamanda Matei.

Alisema upelelezi unaendelea ikiwamo kuwajua watu wengine ambao wanashirikiana na watuhumiwa hao kwenye shughuli hizo pamoja na maeneo mengine ambayo wamejipatia mali kwa njia hiyo.

Alisema baada ya upelelezi huo kukamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

Tukio hilo limekuwa la pili kutokea katika Mkoa wa Mbeya, siku chache baada ya mtuhumiwa mwingine, Adelhard Method (37), kukamatwa Machi 24, kwa tuhuma za kujipatia mali kwa njia kama hiyo.

# Nyumba 20 zanusurika kuteketea

Na Nebart Msokwa, MBEYA

ZAIDI ya nyumba 20 za wananchi na maduka katika Mtaa wa Forest Makanisani jijini Mbeya, zimenusurika kuteketea kwa moto baada ya kutokea hitilafu ya umeme kwenye moja ya nguzo za umeme na kusababisha moto mkubwa.

Ajali hiyo ilitokea juzi alasiri wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilipokuwa ikiendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona kwenye baa zilizopo jirani na eneo hilo.

Moto huo ulizua taharuki kwa wananchi pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo, ambao walichukua hatua mapema za kuukabili moto huo ili usilete madhara makubwa.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Joseph Mbuza, alisema wakati moto huo unatokea, yeye pamoja na wafanyabiashara wenzake walikuwa ndani ya maduka wakiendelea na biashara na kwamba ghafla walisikia kelele nje zikiashiria kuwa kuna hatari.

Alisema baada ya kutoka nje walikuta moto mkubwa unawaka kwenye nguzo ambayo ipo jirani na maduka hayo na ndipo wakaanza harakati za kuokoa mali zao kwa kushirikiana na baadhi ya wasamalia.

"Bahati nzuri Mkuu wa Mkoa pamoja na baadhi ya wajumbe wa Kamati walishafika katika eneo hili, kwa hiyo wakatusaidia, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na maofisa wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) walifika haraka," alisema Mbuza.

Alisema wanaamini uwapo wa Mkuu wa Mkoa katika eneo hilo ndio sababu ya maofisa hao kufika haraka, na kuwa inawezekana walipigiwa simu moja kwa moja na Mkuu wa Mkoa.

Naye Jema Kanzugalla, alisema nguzo nyingi za umeme katika eneo hilo zimechakaa na hivyo akauomba uongozi wa Tanesco kuzibadilisha ili kuwaepusha na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na hitilafu za mara kwa mara.

Alisema nguzo iliyowaka moto wakati wa tatizo hilo ni miongoni mwa nguzo ambazo ni za muda mrefu na kwamba moto ulianzia kwenye mita.

Aliwashukuru maofisa wa Jeshi la Zima Zima Moto na Uokoaji na maofisa wa Tanesco kwa kufika haraka katika eneo la tukio na kuuzima moto huo kwa maelezo kuwa mali zao zingeteketea na kuwaingiza hasara.

"Tuna taarifa kuwa Mkuu wa Mkoa alikuwa na ziara ya kwenda Kyela, lakini ratiba ikabadilika akaja huku kwa ajili ya kutoa elimu na moto umetokea akiwa hapa hapa, sasa endapo angeenda Kyela hatujui nini kingetokea, hivyo tunamshukuru sana kwa kutusaidia," alisema Jema.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwataka wananchi hasa wanaotumia nishati ya umeme kufuata maelekezo ya wataalam ili kuepusha madhara ambayo yanaweza kujitokeza kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya nishati hiyo.

Aliwataka kuunganisha nishati hiyo kwenye nyumba zao kwa kuwatumia wataalamu kutoka Tanesco badala ya kuwatumia mafundi wa mitaani maarufu kwa jina la vishoka.

Ntinika alisema wataalamu wa Tanesco wana mbinu za kuunganisha nishati hiyo na kuepusha madhara ya kutokea hitilafu za mara kwa mara tofauti na mafundi wa mitaani ambao wengi wanafanya kazi hiyo kwa sababu ya njaa na kwamba hawaruhusiwi kufanya kazi hiyo.

"Navishauri vyombo vyetu pia likiwamo Jeshi la Zima Moto na uokoaji kuwa tayari kukabiliana na majanga haya muda wowote, wananchi wana imani kubwa na vyombo hivi, lakini vinapochelewa kuwasaidia imani yao inashuka.

Aliwataka maofisa wa Tanesco kushughulikia matatizo yaliyoainishwa na wananchi wa eneo hilo ikiwemo kubadilisha nguzo ambazo wanadai kuwa zimechakaa ili madhara ya hitilafu ya umeme yapunguwe.



Baadhi ya wajasiriamali wa Mji wa Kasumulu, wilayani Kyela, mkoani Mbeya, waliokuwa wanafanya shughuli zao upande wa Malawi wakivuka Daraja la Mto Songwe, kurejea nyumbani baada ya kufukuzwa na wenzao wa Malawi kutokana na tishio la ugonjwa wa Corona. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Timu ya elimu corona yaanza kazi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

TIMU ya kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona iliyoundwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, imeanza kazi mkoani Mbeya ikiongozwa na mtaalamu wa mashairi, Mrisho Mpoto.

Timu hiyo ilipokelewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye alifanya nayo mazungumzo ofisini kwake akiitaka kuwa huru kutoa elimu hiyo kwa maelezo kuwa Mkoa huo uko salama katika kila eneo.

Chalamila aliwataka wananchi wa maeneo mbalimbali ya Mkoa huo kuipatia ushirikiano timu hiyo ili elimu inayotolewa iwe na manufaa kwao na kwa taifa kwa kusaidia kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni janga la dunia kwa sasa.

Aliwataka wakazi wa mkoa huo, mbali na kuipatia ushirikiano timu hiyo, pia wanatakiwa kuyatekeleza mambo yote watakayokuwa wanaelekezwa ili kuhakikisha wanakuwa salama juu ya ugonjwa huo wa Corona.

"Serikali inatumia gharama kubwa kuukabili ugonjwa huu, sasa ni jukumu letu wananchi kusikiliza maelekezo wanayotoa, kuyatenda wanayoelekeza, watu hawa watatembea katika maeneo mbalimbali na hivyo ni muhimu sana kuwapa ushirikiano," alisema Chalamila.

Mkuu wa Kitengo cha Maji na Usafi wa Mazingira kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anyitike Mwakitalima, alisema pamoja na kutoa elimu pia timu hiyo inasambaza vifaa kwa ajili ya wananchi kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo.

Alisema wanashirikiana na timu ya wataalamu wanaoendesha Kampeni ya 'Nyumba ni choo' inayohamasisha ujenzi wa vyoo bora kwa wananchi kutoa elimu hiyo ya kujikinga na corona ili kuifanya kwa ufanisi zaidi.

"Tunakabidhi lita 150 za vitakasa mikono (Sanitizer) kwa ajili ya wananchi kuzitumia kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huu, na kampeni hii tutaifanya nchi nzima," alisema Mwakitalima.

Alisema kwa sasa madhara ya ugonjwa huo nchini sio makubwa kama ilivyo katika mataifa mengine duniani na kwamba ili kuhakikisha madhara hayo hayaongezeki ni lazima kila Mtanzania achukuwe hatua za kujikinga na kuwakinga wengine.

Naye Msanii Mrisho Mpoto alisema nguvu ya Watanzania katika kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwa sasa ni kunawa mikono kwa kutumia maji tiririka na sabuni.

Alisema Watanzania waache kabisa kufanya masihara na ugonjwa huo kwa maelezo kuwa baadhi wanafanya maigizo na wengine wanatoa taarifa ambazo sio sahihi kuhusu ugonjwa huo.

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrch Matei, aliishukuru Wizara ya Afya kwa kuwaletea vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo.





## Reli kupunguza msongamano Jiji Dodoma

Na Paul Mabeja, DODOMA

KATIKA kukabiliana na foleni ya magari, Jiji la Dodoma limeanza kufanya usanifu wa ujenzi wa reli ya kilomita 100, kwaajili ya usafiri wa treni maeneo ya katika ya mji.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa jiji hilo, Godwin Kunambi, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Kunambi, alisema hivi sasa wanaelekea kuanza kufanya usanifu kwaajili ya ujenzi wa reli itayosaidia kukabiliana na kero ya foleni na msongamano wa magari katika ya jiji la Dodoma.

Alisema treni hiyo itakuwa kiunganishi katika maeneo ya mji wa kiserikali Mtumba, Uwanja wa Ndege Msalato pamoja na maeneo yote ya barabara za mzunguko (Ring road).

"Jiji la Dodoma hivi sasa linakuwa kwa kasi sana hivyo hatuna budi kujipanga na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa linakuwa la kisasa kwa kuondoa changamoto mbalimbali zilizopo," alisema Kunambi.

Alisema jiji hilo linatarajia kupiga marufuku malori ya mizigo kuanzia tani 10, kuingia katikati ya mji baada ujenzi wa barabra ya mzunguko itakapo kamilika.

Kunambi alimshukuru Rais John Magufuli, kwa kutoa Sh. bilioni 400, kwaajili ya ujenzi wa barabara ya mzunguko ya kilomita 112 katika jiji hilo.

"Barabara hii ya mzunguko itazunguka Jiji la Dodoma na magari makubwa ya mzigo kuanzia tani 10, hayataruhusiwa kuingia katika ya mji na yatatumia ring road hiyo itakayojengwa na serikali,"alisema.

Alisema, miradi yote ya kimkakati katika hilo itakapo kamilika itabadili kwa kiasi kikubwa muonekano na kuwa la kuvutia kuliko maeneo mengine nchini.

**"Jiji la Dodoma hivi sasa linakuwa kwa kasi sana hivyo hatuna budi kujipanga na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa linakuwa la kisasa kwa kuondoa changamoto mbalimbali zilizopo," alisema Kunambi.**

# Mvua Dodoma yaharibu miundombinu ya bil. 11/-

Na Augusta Njoji, MPWAPWA

WAKALA wa Barabara nchini (Tanroads), Mkoa wa Dodoma, umesema mvua inayoendelea kunyesha imesababisha uharibifu wa miundombinu ya Sh. bilioni 11.8 kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Mhandisi wa Tanroads Mkoa wa Dodoma, Cyprian Lubida, alisema jana katika ukaguzi wa miundombinu iliyoharibika wilayani Mpwapwa.

Alisema mkoa mzima umepata uharibifu ambao umeshatathiminiwa wa kiasi hicho cha fedha.

"Athari hizi zimeshafikishwa kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji kwa mujibu wa miongozo iliyopo ndani ya saa 24 tangu madhara kutokea, ni lazima kuripoti Tanroads makao makuu na wizarani," alisema.

Alisema, kwa upande wa madaraja yaliyoharibika kwa miaka iliyopita upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulishafanyika na gharama zimeshawasilishwa serikalini kwa ajili ya kuomba fedha.

"Tanroads mkoa wanaendelea kutafuta njia mbadala ili barabara hii ya Mpwapwa ipitike muda wote isiendelee kujifunga,"alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema mvua iliyonyesha hadi sasa wilayani humo ni mara mbili ya mvua ya mwaka mzima.

"Eneo la Chipogolo kule kuliathirika sana, nichukue nafasi hii kushukuru Rais, Mkuu wa Mkoa na Waziri Simbachawene akiwa Waziri wa Mazingira walitusaidia kwa haraka kupitia Tanroads, kukarabati daraja la Chipogolo, makazi karibu laki nne yaliathirika na maji na kaya zisizopungua 30 tunaendelea kuzihudumia,"alisema.

Alisema kwa upande wa barabara, nyingi zinapitika kwa tabu lakini tayari serikali kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) na Tanroads baadhi zimeanza kukarabatiwa.

"Kama hii barabara ya Gulwe kuelekea Kibakwe na Chipogolo tayari ukarabati unafanyika mzuri, jana nimepita huko kujiridhisha, lakini kipande cha kutoka Mpwapwa kwenda Ngh'ambi, nafikiri mmekiona hiki ni korofi ni rai yangu Tanroads wakishughulikie kwa haraka, hii ndio sura ya wilaya yetu na kwa kweli wasafiri na mizigo wanasumbuka sana, imani yangu yatarekebishwa kwa haraka,"alisema.

Hata hivyo, alisema madaraja mengi yameathirika la Chipogolo la kwanza la Wilenzele na Mtamba, pia makaravati huku daraja la Kingiti lilisombwa na mkandarasi yupo hatua za mwisho kukamilisha.

"Daraja la Gulwe lilipata athari kidogo, daraja la Godegode unafahamu tangu mwaka jana limeshasombwa, na tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika, daraja la Mwembeni limeng'oka kabisa na ni kongwe la mwaka 1968,"alieleza.

Alisema wilaya imepokea Sh. bilioni sita kwa ajili ya kukarabati ujenzi wa miradi mbalimbali ya barabara husussan kufungua maeneo mapya ya utawala.



Mzoa taka akizoa mabaki ya majani ya migomba yanayotumia kufungashia ndizi, katika soko la Bonanza, jijini Dodoma juzi, ambayo yamepigwa marufuku na Halmashauri ya Jiji hilo, kuwamo kwenye masoko yake yote. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Tanzania yavunja rekodi umeme vijijini

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema miradi ya upelekaji umeme vijijini (REA), imeipaisha Tanzania kidunia na kushika nafasi ya kwanza Afrika kwa kupeleka umeme kwenye maeneo hayo kwa asilimia 75.2.

Akijibu hoja mbalimbali za wabunge zilizoibuka wakati wa kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2020/21, Kalemani alisema miradi hiyo imeipa sifa kubwa Tanzania na kuishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo kupeleka umeme kwa Watanzania.

"Takribani Sh. trilioni 2.8 zimetumika kuwapelekea umeme wananchi kwenye maeneo haya, huwezi kuzungumzia viwanda kama umeme vijijini haupo, maeneo ya viwanda yapo vijijini ndio maana umeme umepelekwa huko,"alisema.

Alifafanua kuwa mwaka 2008 Tanzania ilipoanza kutekeleza miradi ya REA ilishika nafasi ya 50 Afrika na kuwa na asilimia 16.5.

"Mwaka 2015 tulifikisha asilimia 39.6 na kushika nafasi ya 25 Afrika, mwaka 2017 tulifikia asilimia 47 na kushika nafasi ya 18, mwaka 2018 tulifikia nafasi ya nne Afrika tukiwa na asilimia 58,"alisema.

Hata hivyo, alisema mwaka 2019 ilishika nafasi ya tatu huku Afrika Kusini wakiwa na asilimia 64 na Nigeria asilimia 72.

"Mwaka huu 2020 mwezi wa Februari tumeshika namba moja Afrika kwa asilimia 75.2, nipongeze sana serikali kwa kutoa fedha za kupeleka umeme kwa wananchi wake, niwapongeze pia wabunge kwa ushirikiano,"alisema.

Alisema wilaya 35, kata na vijiji vyote vimefikiwa na umeme na kwamba mradi ujao umeme utapelekwa kwenye vitongoji.

Kuhusu mradi wa gesi asilia, Kalemani alisema utekelezaji wake unaendelea na serikali imetenga fedha huku akikiri kuwa kwa miaka miwili iliyopita kasi ya utekelezaji si kizuri kwasababu mbalimbali.


"Spika mwaka juzi uliunda tume maalumu ya wabunge ya kupitia mikataba na ugawanaji mapato na ilipendekeza mikataba yote 11 ifanyiwe mapitio hii sasa ni kazi ya serikali ili tusiangukie shimoni... kazi imefanyika na taarifa imewasilishwa serikalini hivi karibuni," alisema.

Alisema hatua iliyofikiwa hivi sasa zimetengwa tani milioni 10 za gesi asilia kwa ajili ya kutekeleza mradi huku ikitenga fedha ya kuwalipa fidia wananchi 693 wenye hekari takribani 2,071.

"Fedha zipo nadhani taratibu zikikamilika watalipwa kabla ya kumalizika mwaka wa fedha mwaka huu 2019/20," alisema.

Akizungumza kuhusu mradi wa bomba la mafuta, Kalemani alisema imeshafanyika tathmini ya watu wanaopaswa kufidiwa na watu 9,000 kwa upande wa eneo linapopita bomba na 3,420 kwenye maeneo zitakapojengwa kempu.

Alisema Sh.bilioni 50 zimetengwa na serikali na zilishapitishwa na Bunge huku akisisitiza kuwa miradi hiyo itatekelezwa kama ilivyopangwa na vikao kati ya Tanzania na Uganda vinafanyika kwa njia ya mtandao kutokana na janga la corona.



# Wanaume wanaokataliwa na wapenzi watakiwa kuomba ushauri nasaha

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Hassan, amewataka wanandoa au watu waliomo katika uhusiano wa kimapenzi kuacha kuchukua sheria mikononi mmoja wapo anapomkataa mwezake.

Akizungumza na Nipashe, Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja, alisema baadhi ya wanaume walio katika uhusiano wamekuwa wakichukua sheria mikononi kwa kuwaua wanawake ambao ni wapenzi wao baada ya kuwakataa.

Alisema Machi 31, mwaka huu, huko eneo la Pongwe Mwera, mwanamke mmoja ameuawa kikatili na mpenzi wake baada ya kumkataa.

Alisema marehemu huyo Anna Joseph (25), alipigwa panga la shingo na mpenzi wake Samuel Athumani (26) na kufariki dunia hapo hapo.

"Tukio hilo limetokea majira ya saa tano za usiku wa Machi 31, mwaka huu, chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi," alisema Kamanda Suleiman.

Alisema baada ya mtuhumiwa huyo kutenda kosa hilo alikimbia na polisi ilifanikiwa kumpata Aprili mosi katika eneo la Mkorogo, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema mtuhumiwa huyo alipatikana akiwa na hali mbaya kiafya na alikimbizwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na mtuhumiwa huyo naye alifariki dunia akiwa hospitali.

Alisema kwa mujibu wa uchunguzi wa daktari, mtuhumiwa huyo kabla hajafariki dunia alikunywa sumu kwa lengo la kujiua.

"Mtuhumiwa baada ya kumuua mkewe alikunywa dawa ya kuulia magugu ambayo kwa binadamu ni sumu na kufariki dunia," alisema.

Alisema hilo ni tukio la pili kwa mwaka huu katika mkoa huo kutokea chanzo kikiwa wivu wa kimapenzi.

Vile vile, alisema Februari 26, mwaka huu, huko eneo la Kijiji cha Paje, Mkoa wa Kusini Unguja, mtuhumiwa mwengine Haji Jaha Issa (25) alimuua mpenzi wake Hajra Abdallah (23), kwa kumchoma kitu chenye ncha kali eneo la tumboni na kifuani na kufariki dunia.

Kadhalika Kamanda alisema mtuhumiwa huyo alitenda mauaji hayo baada ya kukataliwa na mpenzi wake huyo ambaye tayari alishamchumbia na kumtolea mahari.

"Mtuhumiwa huyo amekimbia na jeshi la polisi linaendelea kumtafuta ili kumtia hatiani na kumpeleka mahakamani kwa kosa la mauaji," alisema.

Kamanda Suleiman aliwataka wananchi walio katika uhusiano wa kimapenzi wanapokataliwa na wapenzi wao waende kwa watalamu wa ushauri nasaha ili kupata ushauri.

Alisema wengi wa wanaume wanapokataliwa huwa na msongo wa mawazo na baadhi yao huchukua sheria mikononi jambo ambalo ni kinyume na sheria.

# Sasa baa mita 1,000 kutoka makazi ya watu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema Sheria mpya ya kudhibiti vileo ya Mwaka 2020, inalenga kuweka utaratibu wa kuwadhibiti binadamu na waamini wanaokwenda kinyume na maagizo ya vitabu vyao vya dini na kusababisha kuwabughuzi wenzao wanapokuwa katika starehe zao.

Akitoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizowasilishwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati wa mjadala wa Mswada huo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na , Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheir, alisema kumekuwa na ongezeko la utitiri wa baa mitaani jambo ambalo linaleta hofu za uvunjifu wa amani na maadili katika jamii.

Alisema Sheria hiyo inaweka masharti na kulazimisha baa zote za mitaani ziwe umbali wa mita 1,000 kutoka maeneo ya makazi ya wananchi, maeneo ya ibada, shule au hospitali.

Vile vile, aliwaomba wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kutokuwa na hofu na sheria hiyo ambayo ikianza kutumika, baa zote za mitaani zitakua hazipo.

Alisema chini ya Sheria ya kudhibiti vileo ya 2020, wauzaji wote wa vileo, leseni zao zitakufa na watalazimika kuomba na kukata mpya kwa masharti mapya ya sheria hiyo.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kauli moja wameupitisha Mswada huo.

Wakati huo huo, serikali imewasilisha Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa wataalamu wa maabara za tiba wa mwaka 2020.

Akiwasilisha Mswada huo, Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohammed, alisema unapendekeza masharti ya kisheria yanayohusiana na usajili pamoja na usimamizi wa wataalamu wa maabara za tiba Zanzibar kwa kuzingatia maadili na miiko ya utendaji wa maabara hizo.


Alisema sheria hiyo pia inalenga kuweka mfumo wa usimamizi wa ubora na viwango vya kitaifa na kimataifa vya maabara za tiba na taaluma hiyo.

Wakichangia Mswada huo, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekubaliana na uamuzi wa serikali wa kuja na sheria hiyo, kwa vile huduma za maabara za tiba zimekuwa zikiongezeka kwa kasi kubwa nchini.

Walisema sheria hiyo ni muhimu kwa wakati wa sasa kwa kuwa itaweka chombo cha kisheria ambacho kitawasajili na kuwatambua wataalamu wa fani hiyo waliopo nchini.

Katika hatua nyingine Baraza la wawakilishi jana limeanza kupokea taarifa za wizara mbalimbali kuhusu na utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya ripoti za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2019/2020.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2016, Kila Wizara inapaswa kuwasilisha mbele ya Baraza Ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi mara moja kwa mwaka.




Moja kati ya mitaa ya Mji Mkongwe mjini Zanzibar, ambayo kabla ya janga la Corona, ilikuwa na pilikapilika za watu wengi, lakini sasa ni nadra kuwaona watu wakipita. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Ofisi ya Mufti yasema misikiti haijazuia sala jamaa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Mufti Zanzibar imesema haijafunga misikiti wala kuzuia sala za jamaa kutokana na hofu ya virusi vya corona bali inawataka waumini wa dini ya Kiislamu kusali kwa kukaa umbali wa mita moja na nusu baina ya mtu na mtu wakiwa msikitini.

Katibu wa Mfuti Zanzibar, Khalid Mfaume, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi za Mufti zilizopo Mazizini Zanzibar.

Alisema kukaa umbali wa mita moja na nusu msikitini wakati wa sala hakutobadilisha sala hiyo na wala dini haijakataza hilo endapo kutakua na majanga kama hayo ikiwamo ugonjwa wa corona.

Katibu huyo alisema, serikali ilishatoa maagizo kuhusu utaratibu wa sala za jamaa misikitini katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona, lakini baadhi ya maimamu hawafuati maagizo hayo.

"Serikali ilitoa agizo kuhakikisha visomo katika ibada za sala kufupishwa ili kuchukua tahadhari na ugonjwa wa corona na kuleta kunuti katika sala hizo, lakini kwa masikitiko makubwa baadhi ya maimamu hawafuati maagizo hayo," alisema.

Aliviomba vyombo vya habari kuweka vipindi vinavyotoa elimu ya ugonjwa wa corona na kuacha kupiga muziki katika kipindi hiki ambacho taifa limo katika janga la maradhi hayo.

"Huu si wakati wa kufanya masihara, huu ugonjwa unawaangamiza watu...Tushirikiane katika kutoa elimu na kumuomba Mungu atuondolee janga la ugonjwa huu," alisema.

Wakati Ofisi ya Mufti inatoa taarifa hiyo, tayari watu zaidi ya 400 wapo katika karantini Zanzibar na saba waliothibitika kuwa na virusi vya corona wapo katika kituo maalumu kilichotengwa na serikali kwa ajili ya kupata matibabu huko Kidimni, Wilaya ya Kati Unguja.

**"Serikali ilitoa agizo kuhakikisha visomo katika ibada za sala kufupishwa ili kuchukua tahadhari na ugonjwa wa corona na kuleta kunuti katika sala hizo, lakini kwa masikitiko makubwa baadhi ya maimamu hawafuati maagizo hayo," alisema.**

# USAID yasaidia gari kituo cha wasichana

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha nyumba salama cha Mugumu, Serengeti mkoani Mara, kimepata msaada wa gari aina ya Land Cruiser Hardtop, kutoka Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) Tanzania, ili kurahisisha shughuli zake.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania, linalomiliki nyumba hiyo, Rhobi Samwelly, alisema walipokea gari hilo hivi karibuni.

Rhobi alisema, aliyekabidhi gari hilo ni Mkurugenzi Mkazi wa USDAID, Tanzania, Andy Karas, ikiwa ni kutimiza ahadi yake aliyowahi kuitoa alipofanya ziara ya kutembele kituo hicho.

"Tunamshukuru sana Andy Karas kwa msaada huu wa gari ambao utawezesha kurahisisha kazi zetu za kila siku za kuwahudumia wasichana na watoto wanaokimbia ukeketaji," alisema Rhobi.

Alisema, shirika lake linatambua miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Marekani nchini, ikijumuisha sekta za kilimo, lishe, elimu, afya, wanawake na vijana na utawala bora, na kwamba wao kama watetezi wa haki za wanawake wasichana na watoto, USAID Tanzania imewasaidia gari.

"Msaada huu wa USAID Tanzania ni mkubwa sana kwetu na hatuna budi kutoa shukrani na tunawaomba wafadhili wengine kuendelea kuunga mkono juhudi hizi tunazozifanya za kupambana na vitendo vya ukeketaji," alisema.

Wakati huo huo, mkurugenzi huyo, alisema kituo cha nyumba salama kingine cha shirika hilo kilichopo Butiama, kimekabidhi mashine ya 'fotokopi' kwa ajili ya shule za msingi na sekondari za kata ya Buhemba.

Rhobi alisema alinunua mashine baada ya kupata fedha kutoka kwa wafadhili na kuikabidhi kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Buatiama.

"Wafadhili wetu walituwezesha nasi tukanunua mashine hiyo kwa ajili ya shule za msingi za kata Buhemba ikiwamo na sekondari ili itumike kutoa kopi za masomo na mitihani," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema, alikabidhi mashine hiyo kwa uongozi wa halmashauri ili uamue ni wapi itawekwa kwa ajili ya kuziwezesha shule zote za kata ya Buhemba kuitumia.

**"Msaada huu wa USAID Tanzania ni mkubwa sana kwetu na hatuna budi kutoa shukrani na tunawaomba wafadhili wengine kuendelea kuunga mkono juhudi hizi tunazozifanya za kupambana na vitendo vya ukeketaji," alisema.**

# Mifugo yaharibu Chalinze miundombinu ya shamba

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

WIMBI la mifugo inayoingia katika shamba la umwagiliaji Ruvu Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo, linadaiwa kusababisha uharibifu wa miundombinu ya shamba hilo.

Mwenyekiti Chama Cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (Chauru), Sadala Chacha, akizungumza na Nipashe shambani hapo, alisema, wafugaji wanaoishi maeneo ya karibu na shamba hilo wamekuwa chanzo cha miundombinu kuharibika mara kwa mara.

Chacha alisema Aprili 5, mwaka huu sehemu ya tuta linalozunguka shamba hilo ambalo lilijengwa mwaka 1965, lilibomoka na kusababisha maji kuingia katika vitalu vya wakulima zaidi ya 450.

" Tuta hili ambalo thamani ya ujenzi wake ni zaidi ya Sh. milion 45, limekuwa likibomoka bomoka baadhi ya maeneo na kusababisha maji kujaa shambani, ambayo yanatoka katika Mto Ruvu na Kiloweko, hali hii inatokana na mifugo kupita mara kwa mara katika shamba letu," alisema.

Alisema, sehemu ya tuta hilo iliyobomoka na kuathiri wakulima wa mifereji zaidi ya mitano, imesababisha hasara ya zaidi ya Sh. milion 25 kwa vitalu vya wakulima, lakini pia ukarabati wake ambao unaendelea na maeneo mengine ya mifereji unatarajia kugharimu milioni 15.

" Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainabu Kawawa, aliwahi kutoa agizo wafugaji wasiingize mifugo yao shambani lakini hakina mabadiliko na hali ikiendelea hivi mifugo isipodhibitiwa tutaendelea kupata hasara, fedha zinazotumika kufanya ukarabati ni za wakulima wanaohangaika kila siku" alisema Chacha

Alisema, kutokana na hali hiyo kuendelea, amemuwagiza meneja wa Chauru kuhakikisha anawaandikia barua wenyeviti wa vijiji vya Visezi, Kwazoka na Ruvu kuwaelekeza wananchi wao wenye mifugo kuidhibiti isiingie katika shamba hilo la umwagiliaji.

Shamba hilo lenye ukubwa wa hekta 720, lina wakulima 900 ambao wanajishughulisha na kilimo cha umwagiliaji kwa kulima mahindi, mpunga na mboga.

Ofisa Tarafa ya Chalinze, Thomas Molel, ambaye alitembelea shamba hilo na kuona ukarabati unavyoendelea, aliwataka wafugaji kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Molel aliwataka wafugaji hao kuacha tabia ya kulisha mifugo yao katika shamba hilo, na atakayekamatwa hatua za kisheria zitachukuliwa kukomesha tabia hiyo.



Mafundi wakichemsha lami kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa upanuzi wa Barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa: NEC inasimamia watendaji kunusuru uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imekuwa ikifuatilia utendaji kazi wa watendaji wake ili kuhakikisha kuwa hakuna uzembe wa aina yoyote unatokea na kusababisha kuharibika kwa uchaguzi.

Amesema Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, zikisomwa pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Ushahidi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, ikithibitika kuwa mtumishi husika ameharibu uchaguzi na kuisababishia Serikali hasara, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuachishwa kazi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi bungeni wakati akihitimisha hoja ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2020/2021.

Waziri Mkuu alisema utaratibu upo wazi wa kushughulikia watendaji wa uchaguzi wanaofanya uzembe wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kwani NEC hutekeleza majukumu yake kwa uhuru na bila kufuata maagizo ya mtu yeyote.

"Kwa mujibu wa Ibara ya 74(7) na (11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikifanya kazi zake kwa weledi na kwa kuzingatia maelekezo ya Katiba, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo."

Waziri Mkuu aliongeza kuwa NEC imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kuwashirikisha wadau wa uchaguzi, mfano, kabla ya kuanza uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ilikutana na wadau wa uchaguzi katika ngazi ya Taifa na ngazi ya mikoa.

Alisema wadau hao ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wawakilishi wa Asasi za Kiraia, viongozi wa makundi maalum ya watu wenye ulemavu, vijana, wanawake, wahariri na waandishi wa habari.

Alisema lengo la ushirikishaji huo ni kuwataarifu kuhusu matakwa ya kisheria ya kuboresha Daftari, kupata maoni yao na kuwajengea wadau uelewa wa pamoja kuhusu uboreshaji.

HABARI KIMATAIFA

# Corona yampeleka ICU Waziri Mkuu Uingereza

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amelazwa hospitalini katika chumba cha wagonjwa mahututi baada ya afya yake kuzorota kutokana na kuugua ugonjwa wa virusi vya corona.

Taarifa zilizotolewa jana na ofisi yake zilieleza kuwa Johnson alipelekwa katika chumba hicho kutokana na ushauri wa madaktari wake na kwamba alikuwa akipokea uangalizi wa karibu sana.

Johnson alimtaka Waziri wa Mambo ya Nje, Dominic Raab kushika nafasi yake wakati huu akipigania maisha yake.

Waziri Mkuu huyo mwenye umri wa miaka 55 alilazwa katika hospitali ya St. Thomas akiwa na dalili kali za virusi vya ugonjwa huo siku ya Jumapili jioni.

**Vyumba hivyo huwa na wagonjwa wachache na madaktari wengi ili kutoa uangalizi wa moja kwa moja unapohitajika.**

Malkia Elizaberth alikuwa akipewa taarifa kuhusu afya ya Johnson kulingana na kasri la Buckingham.

Kutokana na kuugua huko, viongozi mbalimbali duniani akiwamo Rais Donald Trump na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron wamemtumia salamu za heri.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa Johnson alipatiwa oksijen baadaye siku ya Jumatatu mchana kabla ya kupelekwa katika chumba cha wagonjwa mahututi. Pia, alisahamishwa kama hatua ya kuchukua tahadhari ili awekwe karibu na mashine ya kumsaidia kupumua.

Mwanzoni mwa wiki Johnson aliandika ujumbe kwenye akaunti yake ya mtandao wa kijamii wa Twitter ukiashiria kwamba anaendelea kupata afueni.

Johnson alikuwa amepekekwa hospitalini kufanyiwa vipimo baada ya kutangaza siku 11 zilizopita kwamba alikuwa ameambukizwa virusi vya corona.

Dalili alizokuwa nazo ni pamoja na viwango vya juu vya joto na kikohozi.

Vyumba vya wagonjwa mahututi ni wodi maalumu zilizojengwa kutoa tiba na uangalizi wa karibu kwa wagonjwa walio katika hali mahututi.

Vyumba hivyo huwa na wagonjwa wachache na madaktari wengi ili kutoa uangalizi wa moja kwa moja unapohitajika.

Vyumba hivyo hushirikisha vifaa vya uangalizi . Kuna vitanda 4,000 vya wagonjwa mahututi katika hospitali mpya ya Nightingale. **BBC**



Daktari nchini Urusi, akimpima mmoja wa raia ugonjwa wa virusi vya corona, aliyeonesha dalili ya kuwa na ugonjwa huo. **PICHA: REUTERS**

# Maharusi wakamatwa wakifunga ndoa wakati wa janga la corona

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

WANANDOA wamejikuta matatani huko Afrika Kusini punde tu baada ya kufunga pingu za maisha.

Maharusi hao walivamiwa na maofisa wa Jeshi la Polisi baada ya kudokezewa kwamba kuna harusi inayoendelea huko Kwa Zulu-Natal licha ya marufuku ya kukusanyika kwa sababu ya ugonjwa wa virusi vya corona.

Wageni 50 waalikwa na kasisi aliyewafunganisha pamoja na wanandoa wenyewe walikamatwa na maofisa wa polisi na kupelekwa katika kituo cha polisi nje ya mji wa Richards Bay na wote wanatarajiwa kufikishwa mahakamani.

Video iliyosambaa mtandaoni inamuonesha bwana harusi akimsaidia bibi harusi kwa kushika gauni lake jeupe wakati wanaingia kwenye gari la polisi.

Majina ya wanandoa hao hayakuwekwa hadharani na maofisa wa polisi wala vyombo vya habari.

Aidha, manispaa ya Umhlathuze imesema kuwa maharusi hao watafurahia fungate yao chini ya dhamana kwa masharti watakayopewa.

Afrika Kusini ambayo imethibitisha kuwa na visa 1,655 vya maambukizi ya virusi vya corona ikiwamo vifo 11, kwasasa iko katika wiki ya pili yenye masharti magumu kabisa ya kufungiwa 'lockdown' kama ilivyo kwa baadhi ya nchi duniani.

Pia imekuwa miongoni mwa nchi zenye kupima watu kutoka eneo moja hadi jingine na hivi karibuni itafikia uwezo wa kupima watu 30,000 kila siku.

Raia wa Afrika Kusini kwa sasa wanaruhusiwa kutembea tu iwapo kuna ulazima wa kufanya hivyo na kama haitoshi pia kuna marufuku ya kununua pombe na sigara.

Wachambuzi wamekuwa wakikosoa jinsi nchi hiyo inavyokabiliana na janga la corona na shughuli zote nchini humo zimesitishwa ikiwa kwa 'lockdown' kwa kipindi cha wiki tatu za kwanza. **BBC**

## Waliofariki kwa corona Marekani wafikia 10,000

**WASHINGTON,** Marekani

IDADI ya waliofariki kutokana na ugonjwa wa virusi vya corona nchini Marekani imefikia 10,000, jambo linalozima matumaini ya hali kuwa afadhali kidogo.

Marekani imeibuka kuwa mojawapo ya nchi zilizoathirika zaidi huku kukishuhudiwa idadi kubwa ya watu wanaokufa kutokana na virusi hivyo kila siku na mamilioni wakiathirika kiuchumi.

Uongozi nchini humo ulianza wiki kwa kuwaambiwa raia wajiandae kwa mojawapo ya hali mbaya zaidi nchini humo, huku ikiwa bado mlipuko huo haujafikia kilele chake.

Italia na Hispania ndiyo nchi zenye idadi kubwa ya waliokufa kuishinda Marekani. Lakini kitovu cha virusi hivyo nchini Marekani, mji wa New York umeanza kupata matumaini kidogo kulingana na gavana wake Andrew Cuomo.

Gavana huyo alisema siku mbili zilizopita zimeshuhudia idadi ya waliofariki kupungua.

Miji mingine kama Washington imeshuhudia idadi ya maambukizi kupungua pia

Wakati huohuo, China jana haikuweza kuripoti kifo chochote kutokana na virusi hivyo, hii ikiwa ni mara ya kwanza kabisa jambo hilo kufanyika tangu Januari 19.

Haya yanajiri mnamo wakati mji wa Wuhan unajiandaa kuondoa marufuku yaliyokuwa yamewekwa. **DW**

## Israel yamuachia mpalestina aliyekamatwa Jerusalem

**JERUSALAM,** Israel

ISRAEL imemuachia gavana wa Palestina mjini Jerusalem,Adnan Gaith, baada ya kumzuia kwa siku nzima kwa kile walichosema ni kufanya siasa katika eneo hilo kinyume cha sheria.

Hata hivyo, gavana Gaith, alipojiwa alisema kuwa uwapo wake huko ulikuwa unahusiana na mapambano dhidi ya virusi vya corona.

Muda mfupi baada ya kuachiwa Gaith kupitia ujumbe alioutoa kwa njia ya video alisema hataogopa kufanya lolote lile kuhakikisha amewalinda raia wake kutokana na virusi vya corona.

Kulingana na wakili wake Rami Othman, Gaith alizuiliwa kwa sababu ya juhudi zake za kusitisha kuenea kwa virusi hivyo ambavyo vimeshuhudia kuambukizwa kwa watu 250 katika maeneo yanayokaliwa na Wapalestina.

Hii ilikuwa mara ya saba kwa gavana huyo kuzuiwa na Israel inayosema kwamba alikuwa anafanya mambo ya Kipalestina mjini Jerusalem jambo ambalo ni kinyume cha sheria. **DW**

# Waziri Mkuu ataka wananchi kupuuza ratiba inayosambaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), itatangaza ratiba ya uchaguzi kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria na kuwataka wananchi kupuuza ratiba inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Majaliwa (pichani) alitoa kauli hiyo juzi bungeni alipokuwa akihitimisha hotuba ya bajeti ya ofisi yake kwa mwaka 2020/21, Sh. bilioni 312.8 kimepitishwa na Bunge.

Alisema kwasasa ratiba bado haijatangazwa.

"Tume ya Uchaguzi itatangaza ratiba ya uchaguzi kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria, kwasasa ratiba bado haijatangazwa, nalisema hili kwa sababu tumeona kwenye mitandao ya kijamii watu wakitangaza ratiba ya Tume.

"Hiyo iliyotolewa kwenye mitandao sio sahihi, wananchi wenye sifa ya kugombea nafasi mbalimbali waendelee kujitokeza,"alisema.

Alisema maandalizi ya uchaguzi huo ambao utakaofanyika Oktoba, mwaka huu yanaendelea vizuri.

"Hivi sasa Tume inajiandaa na uboreshaji wa Daftari la Kudumu, awamu ya pili inayotarajiwa kuanza wakati wowote ule mwezi huu (Aprili), baada ya Tume kufanya majadiliano na wadau maazimio mengi yamekubalika na sasa ni jukumu la Tume kutekeleza makubaliano,"alisema.



Alisema lengo la majadiliano hayo ni pamoja na kuiwezesha Tume kujipanga kupata vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya tahadhari ya homa kali ya mapafu (Covid-19).

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye ulemavu, Jenista Mhagama, akitoa ufafanuzi kuhusu hoja ya wabunge wa upinzani ya Tume huru, alisema iliyopo ni kwa mujibu wa Katiba ni huru.

"Ibara ya 11 inaonyesha Tume haitaingiliwa na mtu yeyote hata vyama vya siasa katika kufanya uamuzi wake, nina mfano wa Tume zinazoitwa huru lazima tujiulize misingi ya Tume hiyo ni nini?, Tume hizi zinapimwa kwa utendaji wake kwa kuzingatia sheria na kanuni na Tume yetu inazingatia sheria," alisema.

Mhagama alisema hakuna sehemu ambayo waangalizi wa kimataifa wamesema Tume iliyopo haifai kusimamia uchaguzi.




Dereva na kondakta wa daladala inayofanya safari zake kati ya Miyomboni na Mji Mwema mjini Iringa, wakiwa wamemkamata kijana (mwenye kofia), aliyedaiwa kuwa ni kibaka, baada ya kutaka kumpora abiria aliyekuwamo katika gari hilo, jana. Kijana huyo, alipelekwa katika kituo cha Polisi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# 28 wakamatwa kwa madai ya uhalifu

**Na Robinson Wangaso,** MUSOMA

WATU 28 wanashikiliwa na polisi mkoani hapa kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya uhalifu Ziwa Victoria wakiwa na vitu mbalimbali vinavyohisiwa kuwa ni mali za wizi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shillah, alitaja vitu vilivyokamatwa kuwa ni nyavu za kuvulia samaki 441, kati ya hizo 30 zimetambuliwa kuwa ni mali ya Nyanja Kunju (50) ambaye alivamiwa akiwa na wenzake wawili katika kisiwa cha Irugwa na kuporwa samaki kilo 15 na nyavu 70, huku 41 zikitambuliwa kuwa ziliibiwa katika kisiwa cha Ukara Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza.

Mali zingine zilizokamatwa ni injini 10 za boti ambazo Kamanda Shillah alisema, namba za usajili zilifutwa na polisi inawasiliana na kushirikiana na mamlaka nyingine za usajili wa vyombo hivyo ili kutambua wamiliki wake halali.

Vitu vingine vilivyokamatwa ni mitumbwi minane na mitatu imetambuliwa na wamiliki wake halali wamepatikana.

Pia jeshi hilo limekamata pombe ya moshi lita 440 na watu wanane wanashikiliwa kwa kupatikana na bangi kilo 80.

Watuhumiwa wote 28 wanashikiliwa na watafikishwa mahakamani upelelezi wa awali utakapo kamilika.

Kamanda wa polisi mkoa wa Mara amewaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi ili watuhumiwa wa uhalifu wakamatwe katika msako unaoendelea mkoani hapa.

Mwisho

# Chadema yamlilia mwandishi Elia Mbonea

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimemlilia aliyekuwa Katibu wa Chama cha Waandishi wa habari mkoa wa Arusha (APC), Elia Mbonea (44) (pichani), aliyefariki Jumatatu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alikokuwa amelazwa kwa ajili ya matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Chadema, Tumaini Makene, chama hicho kilifanyakazi na Mbonea katika maeneo mbalimbali ya kuhabarisha umma.



"Mbonea alikuwa ni miongoni mwa waandishi wa habari za siasa waliokuwa wanapewa majukumu na vyombo vyao vya habari kuambatana na misafara ya timu za Chadema kwa ajili ya kuandika habari na kuujulisha umma," alisema.

"Mbali na kushirikiana naye wakati wa operesheni za chama zilizohusisha shughuli za uchaguzi mkuu 2005, 2010 na 2015, Chadema kilifanya naye kazi katika shughuli mbalimbali za kihabari yaliyohusisha mikutano ya hadhara na mikutano na waandishi wa habari hususani iliyofanyika mkoani Arusha."

Alisema katika shughuli zote hizo ambazo Chadema kilikuwa kikifanya naye kazi, alikuwa akionyesha ushirikiano na uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kwa misingi ya weledi na maadili ya kazi na taaluma yake.

Mbonea alikuwa ni mwandishi wa habari wa kampuni ya New Habari (2006) inayochapisha magazeti Dimba, Bingwa, The African, Rai na Mtanzania.

Mwandishi huyo anatarajiwa kuzikwa kesho jijini Arusha.

**Katika shughuli zote hizo ambazo Chadema kilikuwa kikifanya naye kazi, alikuwa akionyesha ushirikiano na uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu yake kwa misingi ya weledi na maadili ya kazi na taaluma yake.**

# Baba matatani tuhuma kuchoma mwanawe unyayo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI LA Polisi mkoani Ruvuma, linamshikilia Mohamed Halifa (30), mkazi wa kijiji cha Mnazi Mmoja wilayani Tunduru, kwa tuhuma za kumchoma moto miguuni mwanawe.

Mtoto hiyo ana umri wa miaka saba ambaye ni mwanafunzi wa darasa la kwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema Machi 15, mwaka huu, kitengo cha dawati la jinsia kilipokea taarifa toka kwa raia wema kuwa katika kijiji hicho kuna mtoto amefanyiwa ukatili na baba yake mzazi.

Alisema mtoto huyo alichomwa sehemu za nyayo na baada ya tukio hilo baba yake alimficha ndani kwa zaidi ya wiki tatu ndipo majirani walianza kulalamika dhidi ya ukatili huo na kutoa taarifa.

Kwa mujibu wa Kamanda Maigwa, polisi baada ya kupata taarifa hiyo walifanikiwa kufika kwenye eneo la tukio na kumkuta mtoto huyo anatibiwa kwa mganga wa kienyeji, huku miguu ikianza kuoza kwenye nyayo.

"Polisi walimchukua mtoto huyo na kumpeleka hospitalini ambako anatibiwa na sasa anaendelea vizuri. Baba yake tunamshikilia na uchunguzi unaendelea ili kupata sababu za kumchoma mwanawe," alisema.

Wakati huo huo, mtu mmoja aliyejulikana kwa jina la Issaya Komba, mkazi wa eneo la Mkuzo Manispaa ya Songea, amekutwa amekufa ndani ya nyumba yake baada ya kujinyonga kwa kutumia mtandio. Kamanda Maigwa alisema kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 4, mwaka huu majira ya jioni na kwamba mkewe ambaye alikuta mume amejinyonga, na hakuacha ujumbe wowote.

Aidha, polisi wanaendelea na uchunguzi na mwili umekabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.

# Wawili wapona corona

**Na Romana Mallya**

HATUA zinazoendelea kuchukuliwa dhidi ya ugonjwa wa corona nchini, zinaendelea kuonyesha matumaini, baada ya wagonjwa wawili kupona.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema wamewaruhusu wagonjwa wawili ambao walikuwa wamepata maambukizi ya virusi vya corona baada ya kupona.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri Ummy alisema walioruhusiwa baada ya kupona mmoja anatoka Dar es Salaam na mwingine mkoani Arusha.

"Tumepata watu wawili ambao wamepona, mmoja wa Dar es Salaam na mwingine wa Arusha, ambao wote wameruhusiwa leo (jana)," alisema.

"Kwa sasa mkoa wa Arusha na Kagera hatuna mgonjwa wa corona, tumebaki na wagonjwa kutoka mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar," alisema.

Alisema takwimu zilizotolewa jana kutoka maabara ni kwamba, Tanzania haina maambukizi kwa watu ambao walichukuliwa sampuli juzi.

"Tunabaki na kesi 24, hivyo jumla ya wananchi walioambukizwa virusi vya corona wanabaki kuwa ni 24, ambapo kati yao wanaotoka Zanzibar ni wagonjwa saba na Tanzania Bara wapo 17," alisema.

Waziri Ummy aliwataka wananchi wawapokee watu hao waliopona corona na wasiwanyanyapae.

"Na hawa waliopona corona wamepewa elimu ya kujitunza na kujiangalia kwa sababu zipo takwimu kutoka China zinaonyesha katika kila watu 100 waliopona watu 14 wanaweza kuambukizwa tena.

"Kwa hiyo usiseme mimi nilipata corona nimepona sitapata tena, hili ndilo angalizo tunataka kulitoa. Serikali hatuna mchezo na suala la karantini, wageni wote wanaotoka nje ya nchi wataendelea kukaa katika hosteli za Magufuli."

Waziri Ummy alisema yeye na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, juzi walilala saa saba ya usiku kwa sababu wametambua zipo changamoto kadhaa ambazo watazitatua.

"Lakini, hakuna mbadala wa mtu kutokaa katika hosteli za Magufuli, kipaumbele chetu kama serikali ni kuhakikisha maambukizi yaliyopo ndani hayasambai kwa jamii.

Alisema wataendelea kuhimiza wananchi kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji yanayotiririka na kuepuka mikusanyiko.

Pia Waziri Ummy alisema serikali haitaki kuingiza kesi mpya ya corona kutoka nje ya nchi hivyo watu watakaa kwenye karantini.

"Ninafahamu kuna mjadala yule wa Dubai alipitaje wakati aliingia tarehe 24, ufafanuzi wake ni kwamba ushauri kwa wataalam tulioutoa Machi 23 ulisema, wasafiri wote kutoka nchi zilizoathirika zaidi hatukusema nchi zote," alisema.

Alisema kadri serikali ilivyokuwa ikitafakari na kuangalia tathmini ya hali halisi, ndipo maana Aprili nne, serikali ilitoa ushauri mwingine.

Alisema ushauri huo ulieleza kuhusu wasafiri wote wanaotoka nje ya nchi kuingia nchini watakaa karantini kwa gharama zao kwa siku 14.

"Hili naomba lielekewe, ndiyo maana akapita, na kesi ya Mwanza inaendelea kutupa nguvu wote serikali na jamii, suala la karantini siyo suala la mchezo, kama tunataka kuilinda Tanzania isipate maambukizi," alisema.



Takataka zikiwa zimetelekezwa pembeni mwa soko la Magomeni, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, na kusababisha kero kwa wafanyabiashara na watumiaji wa soko hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kagera yatajwa kiwango kikubwa ukatili

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKOA wa Kagera umetajwa kuwa miongoni mwa mikoa inayokabiliwa na vitendo vya ukatili kwa kiwango kikubwa.

Imeelezwa katika kipindi cha miezi mitatu ya kuanzia Oktoba hadi Desemba mwaka jana, zimeripotiwa kesi 1,160 za ukatili.

Akizungumza na wanahabari, Ofisa Ustawi wa Jamii mkoa wa Kagera, Rebeca Gwambassa, alisema ukatili wa kisaikolojia ndio unaoongoza kwa kesi 580, ukifuatiwa na ukatili wa kimwili kesi 316, ukatili wa kiuchumi kesi 191 na wa kingono kesi 73.

"Wilaya ya Muleba ndiyo inayoongoza kwa kuripotiwa kesi nyingi za ukatili ambazo ni 689, na Wilaya ya Biharamulo ndiyo ina kesi chake za ukatili zilizoripotiwa," alisema.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa wanapobaini uwapo wa watu wanaofanyiwa vitendo hivyo katika jamii, ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.

"Kuna shida sana ya kupata taarifa za ukatili kutokwa kwenye jamii hasa matukio ya ukatili wa kijinsia... kwa kweli wananchi wa mkoa wa Kagera wamekuwa wagumu kutoa taarifa, wanapaswa kubadilika ili kutuwezesha kufikia malengo ya kutokomeza vitendo hivi," alisema.

Mshauri wa kitengo cha haki za binadamu kilichoko chini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Bukoba, Jowab Rwezaula, alisema asilimia kubwa ya vitendo vya kikatili vinachangiwa na baadhi ya vijana kuingia katika ndoa bila maandalizi na hali ya uchumi kuyumba katika familia.

"Mtu anaingia kwenye ndoa bila hata kuwa na uelewa, kwa sababu tu kafikisha umri fulani anaona ni muda mwafaka kwake kuoa wakati msingi wa kutunza familia hana," alisema na kuendelea:

"Lakini hata mabinti wanaokwenda kuolewa siku hizi hawapati mafunzo muhimu yanayostahili, ambayo yatamwezesha kujua kuwa kaingia kwenye ndoa na anapaswa kuishi vipi."

Alisema pia uchumi ukiyumba kidogo hasa kwa baba, mama anaanza kulalamika kuwa mumwe amepata mke mwingine, na kuwa ugomvi unapoibuka familia zinaparaganyika na kuathiri pia watoto, matokeo yake wanakimbilia mitaani na kuongeza idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mmoja wa wananchi waliozungumza na Nipashe, Innocent Rwezaula, mkazi wa Manispaa ya Bukoba, alisema tatizo hilo linachangiwa na elimu duni katika jamii na watu kutoheshimiana.

"Ushauri wangu ili kumaliza tatizo hili, lazima elimu ya umuhimu wa kupendana na kuishi kama ndugu isisitizwe kwa watu... wafahamu kuwa binadamu wote ni sawa, na hakuna sababu ya kumnyanyasa mtu awe wa kike au wa kiume," alisema.

# BOATENG AGOMBEWA CHELSEA NA ARSENAL




**MUNICH,** Ujerumani

BEKI wa Bayern Munich, Jerome Boateng, anaweza kuondoka klabuni hapo kipindi kinachokuja cha majira ya joto, huku akipeleka vita ya kumuwania kati ya Chelsea na Arsenal.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 yupo anaingia kwenye miezi yake 12 ya mwisho katika mkataba wake pale Bayern na majaliwa yake yanaonekana kutojulikana na mkataba mpya bado haujafikiwa.

Uhusiano wa Boateng na Bayern sio mazuri baada ya kupigwa faini na klabu hiyo kwa kuvunja sheria ya kutulia ndani kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona, kwa kusafiri.

Beki huyo alidai alikuwa akisafiri kwenda Leipzig kumuona mtoto wake wa kiume ambaye alikuwa mgonjwa, lakini Bayern bado imeshikilia msimamo wa kumpiga faini na hilo litasababisha kufungua mlango wa kuondoka.

Kwa mujibu wa FootMercato, Arsenal na Chelsea zote zinawania kumsajili beki huyo wa kati mwenye uzoefu mkubwa kipindi cha majira ya joto.

Washikabunduki waliripotiwa kujaribu kumsajili Boateng Januari lakini hawakufanikiwa na sasa wanataka kujaribu kipindi cha majira ya joto yanayokuja.

Raia huyo wa Ujerumani, alijiunga na Bayern mwaka 2011 baada ya msimu mmoja pale Manchester City na amecheza mechi 310 na amefunga mabao nane kwa klabu hiyo.

Kwa kipindi chake alichocheza Bayern, Boateng amebeba taji la Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, mara saba, huku pia akishinda kombe la Dunia mwaka 2014 akiwa na kikosi cha Ujerumani.

## Son kuanza kulitumikia jeshi la Korea Kusini

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur, imethibitisha kwamba mshambuliaji wake, Son Heung-min, ataanza kutumikia jeshi la nchi yake ya Korea Kusini ikiwa ni sehemu ya kutimiza sheria ya lazima ya nchi hiyo, mwezi huu wakati ambao kuna mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Mshambuliajii huyo ataanza mafunzo ya wiki ya wiki nne ya kutumikia jeshi la nchi hiyo, huku akitarajiwa kurudi nchini England Mei mwaka huu.

Jumatatu wiki hii, Tottenham ilitoa taarifa ikisema: "Klabu inaweza kuthibitisha kwamba, Heung-Min Son atakwenda kujiunga na heshi la Korea Kusini kwa mujibu wa sheria mwezi huu.


"Mshambuliaji huyo alirudi nchini kwake Machi ambapo kwa sasa yupo karantini. Timu yetu ya madaktari wanawasiliana naye mara kwa mara kujua anavyoendelea baada ya kuvunjika mkono wakati wa mchezo wa ushindi wa 3-2 dhidi ya Aston Villa Februari 16 mwaka huu.

"Sonny alifanyiwa upasuaji wa mkono nchini Korea Kusini kabla kurudi Uingereza mwishoni mwa Februari kuendelea na kujiuguza, kabla ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya COVID-19. "

Son alitakiwa kulitumikia jeshi hilo kwa miezi 21, lakini alipata msamaha wa kupunguziwa siku mwaka 2018 baada ya kuwa kwenye timu ya Korea Kusini iliyoshinda kwenye michezo ya bara la Asia.




## Wan-Bissaka: Kumkaba Sterling si rahisi



**MANCHESTER,** England

AARON Wan-Bissaka, amemtaja winga wa Manchester City, Raheem Sterling, kama ndiye mchezaji mgumu zaidi kumkaba katika maisha yake ya soka hadi sasa.

Beki huyo wa kulia amekuwa na wakati mzuri pale Manchester United kwenye nafasi ya ulinzi msimu huu, tangu alipotua hapo akitokea Crystal Palace kwa ada ya pauni milioni 50 kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Muingereza huyo amesema licha ya kukutana na mawinga wengi, lakini amemtaja Sterling kuwa ndio mpinzani aliyekuwa mgumu zaidi kumkaba hadi sasa.

Wan-Bissaka ameiambia tovuti ya Manchester United: "Naweza kusema Raheem Sterling; ndio mpinzani mgumu kumbaka.

"Anakimbia kwa kasi. Mara zote nikicheza dhidi yake nakabiliwa na changamoto kubwa mno. Ndio maana nampenda."

Wan-Bissaka amekabiliana na Sterling mara mbili kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku Manchester United wakishinda mechi zote mbili na kumzima Sterling."

## HABARI MICHEZO

# Fifa kuongeza mwisho wa mikataba ya wachezaji

**LONDON,** England

DIRISHA la usajili la kipindi cha majira ya joto na mikataba ya wachezaji iliyokuwa imalizike Juni 30, mwaka huu, itaongezewa kwa muda mfupi baada ya kufikiwa makubaliano na washikadau wakubwa wa soka barani Ulaya.

Kwa mujibu wa BBC Sport, mazungumzo yaliyosimamiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), mashirikisho, klabu, wachezaji na ligi yamefikia makubaliano ya mambo kadhaa kutokana na mlipuko wa virusi vya Covid-19.

Pande zote sasa zimekubaliana kwamba msimu wa 2019-20 kwa ligi zote uwe umemalizika kufikia Juni 30.

Aleksander Ceferin, rais wa shirikisho la vyama vya soka vya Ulaya, Uefa, alipendekeza msimu wa ligi umalizike kufikia Agosti.

Pia tarehe mpya ya dirisha la usajili imepelekwa pia itaangaliwa upya na pia siku ya kufungwa kwake.

Fifa pia imetoa pendekezo la kuhakikisha mikataba ya wachezaji iliyokuwa inamalizika Juni 30 mwaka huu kusogezwa mbele.





# MAMA WA GUARDIOLA AFA KWA CORONA

**BARCELONA,** Hispania

MAMA mzazi wa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, Dolors Sala Carrio, mwenye umri wa miaka 82, amefariki dunia jijini Barcelona, baada ya kupata maambukizi ya viruzi vya corona (COVID-19).

"Kila mmoja anayehusika na klabu ametuma ujumbe wa rambirambi katika kipindi hiki kigumu kwa Pep, familia yake na marafiki zake wote ," umesema ujumbe wa timu ya Manchester City uliotumwa kwenye mitandao ya kijamii.

Ongezeko la Jumatatu la vifo 637 vya virusi vya corona linamaanisha kuwa hadi sasa watu 13,055 wamekwishafariki nchini Hispania kutokana na janga hilo.

Mwezi uliopita, Guardiola alitoa mchango wa euro milioni moja kwa ajili ya kusaidia katika vita dhidi ya mlipuko wa virusi vya corona.

fedha hizo zitatumika katika kununulia vifaa vya matibabu na kujikinga na maambukizi kwa ajili wahudumu wa tiba wanaowashughulikia wagonjwa waliolazwa hospitalini.

Barcelona iko katika jimbo la Katalunya, ambako ni moja ya maeneo nchini Hispania yenye idadi kubwa ya visa vya corona.

Manchester United ilituma ujumbe wake kwenye mtandao wa kijamii ikisema klabu hiyo "imesikitishwa sana kusikia taarifa hii mbaya" na kuongeza kuwa: "Tunatuma rambirambi zetu kwa Pep na familia yake ."

Guardiola ambaye ni Mhispania, mwenye umri wa miaka 49, amekua kocha wa Man City tangu Julai 2016 baada ya kuhudumu kama kocha katika timu za Barcelona na Bayern Munich.

# *Kocha Real Madrid awaonya Barcelona usajili wa Neymar*

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa zamani wa timu ya taifa ya Hispania na Real Madrid, Vicente del Bosque, amewaonya Barcelona katika mpango wake wa kumrudisha Neymar klabuni hapo akisema haoneshi "mfano mzuri."

Neymar alitumia miaka minne pale kwenye dimba la Camp Nou hadi mwaka 2017, wakati alipokwenda Paris Saint-Germain kama mchezaji ghali wa wakati wote kwa euro milioni 222.

Licha ya raia huyo wa Brazil kuonesha kiwano cha kuvutia kule Paris, akifunga mabao 47 na kutengeneza asisti 26 kwenye mechi 52 za Ligi Kuu ya Hispania, Ligue 1, ambako anaonekana hana furaha.

Sasa amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Hispania huku Barca na Real Madrid zikitajwa kumuwania, ingawa amekuwa akihusishwa zaidi na klabu yake ya zamani.

Del Bosque, alama ya Madrid na mshindi wa kombe la Dunia akiwa na Hispania, anafikiri Neymar ni tatizo na ameionya Barca kuwa makini na mahitaji yao ya kumrudisha Neymar kule Katalunya.

"Ni klabu ndio ambayo inaamua nani wa kumsajili," amesema Del Bosque akiliambia gazeti la Mundo Deportivo.

"Hutakiwi kusikiliza sana wachezaji wanachosema, kwani kuna wakurugenzi wa soka na wakurugenzi wa ufundi.

"Ni ngumu sana kwa mchezaji kumzungumzia vibaya mchezaji mwingine ambaye ni mchezaji mwenzake. Sikumbuki nani alishafanya hivyo.

"Neymar ni kijana msumbufu. Kwa upande wangu sio mfano mzuri."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK ATAKA KUZEEKEA LIVER

Ndiyo, ningependa kuwa mmoja miongoni mwa wachezaji watakaorudi Anfield baada ya...

**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk anataka kukumbukwa kama "nguli wa Liverpool" wakati siku zake za kucheza soka zitakapomalizika klabuni hapo.

**Beki huyo wa kati wa Uholanzi, amekuwa ufunuo tangu ajiunge na klabu hiyo Januari 2018, akibeba majukumu makubwa ya kuibadilisha Liverpool kutoka nafasi nne za juu kwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushikilia uongozi wa Ligi Kuu hadi sasa.**

Kabla ya kuibuka kwa janga la kidunia la virusi vya corona (COVID-19) na kusababisha kusimamishwa kwa masuala ya soka kwa muda usiojulikana, Liverpool walikuwa mbele kwa pointi 25 zaidi kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, wakiwa na uwezekano wa kushinda mechi mbili na kutwaa taji lao la kwanza tangu ianze kuitwa 'Premier League'.

Van Dijk anachukuliwa kuwa sababu kubwa ya mafanikio hayo, na kidogo atwae tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] dhidi ya Lionel Messi mwaka jana.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 28, anahisi uhusiano na klabu na anatumaini kuwa ataonekana kama mmoja wa wachezaji wakubwa wa Liverpool wakati atakapotundika buti zake.

Wakati alipoulizwa ni vipi anataka kukumbukwa wakati atakapohitimisha kazi yake ya kucheza soka, aliiambia Sport: "Kama nguli wa Liverpool. Nataka kufikia vitu vya kushangaza hapa.

"Tuna timu bora, hatupungukiwi chochote, tuna zana zote muhimu za kushinda, kocha ambaye tunatambulika naye, kikosi cha aina nyingi ya uchezaji ambao unazalisha ushindi, uwanja na mashabiki wanaocheza sehemu yao.

"Ndiyo, ningependa kuwa mmoja miongoni mwa wachezaji ambao watarudi Anfield baada ya kustaafu. Ninaona nguli wa klabu katika mechi na nahisi ukweli sehemu ya familia kubwa."

Ingawa taji lao la kwanza la ligi katika kipindi cha miaka 30 linaonekana wazi kuhitimishwa na COVID-19, Liverpool hawatatetea ubingwa wao wa Ulaya kwani walishaondolewa na Atletico Madrid kwenye mchezo wa mwisho kabla ya michuano hiyo kusimamishwa.

## ZISIKUPITE

### UTD YAJIAMINI KWA SANCHO

MANCHESTER United imeongeza kujiamini katika mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa England, Jadon Sancho, 20, kutoka Borussia Dortmund majira haya ya joto. ***(Standard)***

### BARCA KAMILI KWA MARTINEZ

BARCELONA ipo tayari kumsajili Lautaro Martinez, 22, kutoka Inter Milan lakini inajua inakabiliwa na ushindani kutoka Real Madrid na Manchester City kwa mshambuliaji huyo raia wa Argentina. ***(Marca)***

### ARSENAL JICHO KWA NUNEZ

ARSENAL Imemtaja beki wa Athletic Bilbao, Unai Nunez, 23, kama mchezaji wanaomuwinda majira ya joto. Nyota huyo wa kimataifa wa Hispania ana kipengele katika mkataba wake kinachomruhusu kuuvunja kwa pauni milioni 26. ***(La Razon - in Spanish)***

### TORRES AVUTIA VIGOGO EPL

LIVERPOOL, Manchester City na Manchester United zote zimeulizia kuhusu kupatikana kwa winga wa Valencia, Mhispania Ferran Torres, 20. ***(Goal)***

### LINGARD AIKATAA ARSENAL

KIUNGO wa Manchester United, Jesse Lingard, 27, hana lengo la kuondoka klabuni hapo majira ya joto. Nyota huyo wa kimataifa wa England hivi karibuni alihusishwa na kujiunga na Arsenal na Everton. ***(Metro)***

### LIVER KWA ZAKARIA, THURAM

LIVERPOOL inapanga kusajili wachezaji wawili kiungo Mswisi Denis Zakaria na mshambuliaji Mfaransa Marcus Thuram kutoka Borussia Monchengladbach. ***(Express)***

### GIROUD, CHELSEA WATETA

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Olivier Giroud, 33, amefanya mazungumzo ya awali na Chelsea ya mkataba mpya utakaombakisha hapo Stamford Bridge. ***(Football.London)***

### BOATENG AWINDWA ARSENAL

CHELSEA inajiandaa kutoa upinzani kwa Arsenal katika mbio za kumsajili beki Mjerumani Jerome Boateng, ambaye anaingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na Bayern Munich. ***(Mail)***

### NEYMAR KUIPOTEZEA BARCA

NEYMAR ameripotiwa anajiandaa kubaki Paris Saint-Germain majira haya ya joto, licha ya Barcelona kuvutiwa naye. ***(The Sun)***

### SOUTHGATE KUMTOSA WALKER

KYLE Walker hataichezea tena England chini ya kocha Gareth Southgate - kutokana na bosi huyo wa 'Three Lions' kukerwa na kitendo cha beki huyo kufanya pati wakati wa karanteni ya virusi cya corona. ***(Daily Mirror)***

### WOLVES: DAU LA TROARE HILI

WOLVES haitamuuza Adama Troare chini ya pauni milioni 70 katika dirisha la majira ya joto baada ya winga huyo Mhispania mwenye umri wa miaka 24 kuhusishwa na kujiunga na Liverpool. ***(Football Insider)***

## HABARI MICHEZO




Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola (kulia), akiwa na mama yake, Dolors Sala Carrio enzi za uhai wake kabla ya kufariki dunia jana kutokana na kushambuliwa na virusi vya corona (COVID-19). Wiki moja kabla Guardiola aliipa Hispania msaada wa euro milioni moja sawa na Sh. bilioni 2.4 kusaidia mapambano dhidi ya corona. **HABARI UK. 29**

# YANGA YAITWA MEZANI KUTETA NA SURE BOY

Habari na Saada Akida

UONGOZI wa Azam FC, umewataka Yanga kufuata taratibu kama ambavyo ulifanya wakati ikiwapa baraka za kumsajili mshambuliaji wao, Ditram Nchimbi, ambaye kwa sasa anaitumikia miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani.

**Kauli hiyo imekuja baada ya kuibuka taarifa za Yanga kuhitaji saini ya kiungo wa Azam FC, Salum Abubakar 'Sure Boy', ambaye hivi karibuni ameongeza mkataba wa mwaka mmoja unaomfanya kuitumikia timu hiyo ya Chamazi jijini Dar es Salaam hadi mwaka 2021.**

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema Sure Boy bado ana mkataba wa mwaka mmoja zaidi wa kukitumikia kikosi hicho, hivyo kama Yanga inamhitaji inakaribishwa mezani kufuata taratibu zote kama ambavyo ilifanya wakati walipohitaji huduma ya Nchimbi.

Alisema hawajakutana na wala kuwajafuatwa na klabu hiyo au timu yoyote ambayo inahitaji kufanya nao mazungumzo kwa lengo la kumsajili mchezaji huyo ama mwingine ndani ya kikosi cha timu yao.

"Sisi hatumzuii mchezaji yeyote kuondoka, ila Sure Boy ni mchezaji wa Azam, ana mkataba mrefu bado na sisi, kama Yanga inamhitaji ifuate taratibu walizofuata awali na kisha kutoa pesa kununua Nchimbi," alisema Popat.

Alisema kawaida ilivyo kwa klabu ama timu ikihitaji mchezaji mwenye mkataba, inafanya mawasiliano na klabu inayommiliki kwa ajili ya makubaliano ya pande zote tatu; zikianza klabu kwa klabu na baadaye mchezaji ambaye atakuwa na uamuzi wa kukubalia ama kukataa.

Popat alisema hawawezi kuweka thamani ya nyota huyo kutokana na ukweli kwamba hakuna timu ambayo imeonyesha dhamira ya kumhitaji licha ya kuona na kusikia katika vyombo vya habari kuwa Yanga inahitaji huduma yake.

# *Usajili Simba sasa kimya kimya*

WAKATI baadhi ya majina ya wachezaji wakihusishwa na Simba, uongozi wa klabu hiyo umesema tayari umepokea mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mbelgiji Sven Vandenbroeck na kuanza kuyafanyia kazi kimya kimya.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, alisema kwa sasa wanafanyia kazi mapendekezo ya benchi la ufundi kwa wachezaji ambao wataongezwa pamoja na watakaochwa kutokana na matakwa ya ripoti ya kocha huyo.

Msauzi huyo alisema mikakati yao mikubwa ni kufanya usajili kwa ajili ya kuandaa kikosi cha timu hiyo kuweza kutoa ushindani mkubwa kwenye Ligi ya Mabingwa ikiwamo kuvuka katika hatua ambayo waliishia msimu uliopita.

"Kwa sasa Sven ametoa mapendekezo yake ya wachezaji wa kusajiliwa na kuachwa, hili linafanyiwa kazi kwa umakini, hatuwezi kuweka wazi siri za klabu muda ukifika kila kitu kitajulikana," alisema Senzo.

Wachezaji ambao Simba inadaiwa kuanza kufanya nao mazungumzo ni beki wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto kwa kuchukua kiasi cha Sh. milioni 80 licha ya nyota huyo kudai thamani yake ni Sh. milioni 90.

Wengine waonatajwa ni Mghana James Kotei anayecheza soka la kulipwa Belarus, Emmanuel Okwi anayekipiga Al Ittihad ya Misri, pia kiungo wa Azam FC, Salum Abubakar ambaye jina linadaiwa linajadiliwa na kamati ya usajili ya vinara hao wa Ligi Kuu Bara.

## Mwadui: Corona itatutibulia ubora

WAKATI hatma ya kuendelea kwa Ligi Kuu Bara ikiwa bado haijulikani, uongozi wa timu ya Mwadui FC, umesema hauna imani na wachezaji wao kufanyia kazi ipasavyo maelekezo ya mazoezi waliyopewa kipindi cha mapumziko ili kurejea wakiwa fiti.

Ligi Kuu Bara imesimama kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), ambavyo tayari vimesababisha maelfu ya watu kupoteza maisha hadi sasa.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ramadhani Kilao alisema wanapambana kuhakikisha timu yao inabaki Ligi Kuu lakini mazingira magumu yaliyopo kwa sasa kutokana na kusimama kwa ligi hiyo, kunawatia hofu kwa wachezaji wao kuendelea na mazoezi kama walivyoelekezwa na benchi la ufundi.

Alisema wako katika mazingira magumu sana kwa ujumla, hakuna uangalizi mzuri wa wachezaji walipo majumbani licha ya kupewa program na mwalimu.

"Uhakika wa kwamba wanajitunza au wanafanya mazoezi binafsi haupo, nina imani wachezaji hawatakuwa fiti endapo ligi itaendelea na hivyo itategemea kama Bodi ya Ligi (tplb) itatoa muda kabla ya mechi kuanza walau yafanyike mazoezi ya pamoja.

Alisema makocha wanafanya kazi kubwa kuwapa program ya mazoezi wachezaji wao kipindi hiki cha mapumziko haya ya corona ila hawana imani nao kama wanafanyia kazi ipasavyo maelekezo hayo.

Mwadui ipo nafasi ya 12 ikiwa na pointi 34 baada ya mechi 28, wakati huu Simba ikiwa kileleni na alama 71, huku Singida United ikiburuza mkiana na pointi zake 15 zilizotokana na michezo 29.

Michezo
Jumatano Aprili 8, 2020
Nipashe



Van Dijk ataka kuzeekea Liver

UKURASA 30

HAKUNA KULALA...




Kipa namba moja wa Simba na timu ya Taifa, Taifa Stars, Aishi Manula, akijifua peke yake nyumbani kwake Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, kipindi hiki klabu yake ikiwa imesitisha mazoezi kwa mwezi mmoja tangu Machi 17, mwaka huu, kufuatia agizo la serikali kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), vilivyoua jumla watu 76,383 duniani kote hadi kufikia jana jioni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mnigeria kinara wa mabao aiita Yanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KINARA wa kucheka na nyavu Ligi Kuu Zanzibar, Mnigeria Shehu Magaji Bulama, anayeichezea JKU, ameiita Yanga mezani baada ya kueleza anatamani siku moja kuichezea timu hiyo anayoipenda na anayohisi itamfikisha mbali zaidi katika harakati zake kisoka.

Shehu ambaye alijiunga na JKU katika usajili wa dirisha dogo msimu wa 2017/18, ni miongoni mwa wachezaji wanaoongoza kwa kucheka na nyavu Ligi Kuu Zanzibar msimu huu akiwa na mabao 12, sawa na mchezaji wa KMKM, Optatus Yustin. Mchezaji huyo raia wa Nigeria, mwenye umri wa miaka 21, akizungumza na gazeti hili jana visiwani hapa, alisema matumaini yake makubwa ni kuona lengo lake la kuichezea Yanga linatimia na kuanza kuonyesha kipaji chake Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema yeye ni mchezaji mwenye malengo ya kufika mbali katika soka kama ilivyo kwa wachezaji wengi ambao hivi sasa wamekuwa na mafanikio makubwa kupitia soka na kufikia hatua ya kucheza soka la kulipwa.

"Kila mchezaji anakuwa na malengo pamoja na kwamba yanatofautiana, lakini mimi lengo langu kubwa ni kuhakikisha nafika hatua ya kucheza soka la kulipwa ingawa kwa sasa nawaza kwanza kuichezea Yanga kwa kuwa ni timu yangu pendwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kama itatokea timu nyingine ya ligi hiyo kunihitaji, tukikubaliana sitasita kwenda," alisema mchezaji huyo ambaye ameshaifungia JKU jumla ya mabao 19 katika mechi 25 alizoichezea tangu ajiunge na timu hiyo.

Aidha, akizungumzia JKU, alisema timu hiyo imempa mafanikio makubwa mpaka kuwa mchezaji tegemeo ndani ya kikosi hicho: "JKU ni miongoni mwa timu ambayo imechangia mafanikio yangu mpaka kufikia hapa nilipo, naitumikia timu hiyo kwa moyo wangu mmoja ili kuhakikisha tunafanya vizuri na hata kunyakuwa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu".

Hadi Ligi Kuu Zanzibar inasimama kutokana na kuibuka janga la virusi vya corona (COVID-19), JKU ipo nafasi ya pili katika msimamo ikiwa na pointi 45 baada ya mechi 20 ya ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

# Sven aishukia TFF kurejea Ligi Kuu

## Ageuka mtetezi wa timu zote 20 wakati zikisikilizia uamuzi wa serikali ligi kuanza...

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU majaliwa ya kurejea kwa Ligi Kuu ama la, yakitarajiwa kujulikana Ijumaa ijayo wakati agizo la serikali la kusitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu litakapomalizika, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amegeuka mtetezi wa timu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo akitaka zipewe muda zaidi wa kujifua kabla ya mtifuano huo kuanza rasmi.

**Machi 17, mwaka huu serikali ilipiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), ambavyo hadi jana jioni tayari vilisababisha jumla ya vifo 76,383 duniani kote huku jumla ya watu 1,363,678 wakiripotiwa kushambuliwa.**

Hata hivyo, katika kipindi hiki makocha wengi wamewapa wachezaji wao programu maalum ya mazoezi ya kutekeleza wakiwa nyumbani kwao, jambo ambalo Sven anaona bado haliwezi kuwasaidia kurejea moja kwa moja katika mikikimikiki ya Ligi Kuu endapo zuio hilo la serikali litamalizika wiki ijayo.

Akizungumza na mwandishi wetu jijini Dar es Salaam, Sven alisema kwa usalama wa wachezaji ni vema Shirikisho la Soka nchini (TFF), likatoa wiki mbili kwa timu kufanya mazoezi ya pamoja na wachezaji wao kabla ya ratiba ya ligi hiyo kuanza rasmi baada ya zuio hilo la serikali kumalizika.

Alisema kama ligi hiyo itaanza moja kwa moja kuna uwezekano mkubwa kwa timu kukabiliwa na wimbi kubwa la majeruhi kwa kuwa wachezaji wengi watakuwa hawapo fiti vya kutosha kuhimili pilikapilika za ligi kutokana na kutokuwa na mazoezi ya kutosha.

"Kwa sasa wachezaji wapo nyumbani, hakuna mechi wala mazoezi yanaendelea, ni vema kabla ya ligi kuanza TFF ikatoa wiki mbili ili kuwaweka wachezaji fiti kuepuka majeruhi," alisema Sven ambaye timu yake inahitaji pointi 14 tu katika michezo 10 iliyobakiza kabla ya kutawazwa mabingwa wa ligi hiyo.

Sven alisema licha ya makocha kutoa programu maalum za mazoezi kwa wachezaji wao, hakuna uhakika kama wanazitekeleza kipindi hiki wakiwa mapumzikoni nyumbani kuepuka kasi ya maambukizi ya corona.

Simba inayoongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 71 baada ya kushuka dimbani mara 28, hata kama serikali itaruhusu ligi hiyo kuendelea wiki ijayo na TFF kutoa majuma mawili kwa timu kujiandaa, bado itawakosa baadhi ya nyota wake wakiwamo kinara wa mabao, mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere, na kiungo mpishi, Mkenya Francis Kahata, ambao mipaka ya nchini mwao imefungwa kutokana na kukwepa maambukizi ya virusi vya corona.

Kagere anayeongoza kwa mabao 19 katika orodha ya wafungaji Ligi Kuu, na Kahata aliyecheka na nyavu mara nne na kutoa pasi za mwisho 'asists' tano, walirejea kwao kusalimia familia zao baada ya ligi hiyo kusimamishwa, kabla ya baadaye mipaka ya nchi zao kufungwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >